Bly (1990) anajadili kuwa nadharia hii inalenga kuhalalisha mila za kiume na kuleta muono mpya kuhusu ubabedume. Kando na kutumika kunyanyasa wanawake, ubabedume unaweza pia kutumika kuwajali wengine. Wanaume hutekeleza majukumu yao kulingana na mila na matarajio ya jamii yao.

Nadharia hii hutenganisha majukumu ya jinsia mbili. Mgawanyiko huu husaidia kufanikisha mahitaji ya jamii. Huchangia pia kutambulisha nafasi ya mwanamume katika miundo ya kijamii. Asasi za kijamii hubadilika kulingana na vipindi vya kihistoria. Bly (1990) anaeleza kuwa wimbi la pili la ufeministi lilishughulikia mamlaka ya kiume kama taasisi inayoyumba. Uyumbaji huu

ulichangiwa na wanaharakati wa kike. Bly anaamini kuwa Uwezo-Mkuu wa Kiume ni suala la mtagusano wa heshima kati ya mtu na jamii.

Izugbara (2005) anaeleza kuwa wanaume wapole mara nyingi huathiriwa na mfumo-dume. Jamii ya kiume ina mchanganyiko wa wanaume. Wengine wanapaswa kutumia jinsia yao kusaidia na kuinua wanawake na watoto. Wengine, wanaojizamisha katika ubabedume, huwakandamiza wanajamii wengine. Nadharia hii huwaashiria wanaume wapya kama waliobadilika. Hii inamaanisha kuwa maadili ya kiume yanaweza kubadilika kulingana na jamii na wakati.Janvan (2023) anaeleza kuwa nadharia hii hudhihirisha mabadiliko katika asasi za elimu, siasa na uchumi. Huzua pia mwamko mpya wa kutafakari hali ya wanaume jamiini. Wanapaswa kujikomboa kutoka mifumo hasi ya kitamaduni. Wanaume wanapaswa kuwa na mienendo inayoweza kuigwa na wengine.

Nadharia hii inatoa mtazamo tofauti wa ubabedume. Inamtazama mwanaume kama anayetumia hadhi yake kulinda wanawake na watoto. Hata hivyo, jamii huchangia sana maadili ya kiume, kupitia malezi na mila zake. Mawazo ya mtu binafsi hubadilika kulingana na jamii, mazingira, na wakati. Nadharia hii hutumika katika fasihi kuchambua usawiri wa wahusika wa kiume. Luyt (2017) anasema kuwa fasihi hushiriki kudhibiti au kuimarisha kanuni za nadharia hii kupitia wahusika na maudhui. Hivyo, riwaya, mashairi na hadithi zinaweza kuwaumba wahusika wa kiume. Zinaweza kuendeleza au kupinga maadili ya kibabedume.

Mohlala (2024) anasema fasihi ya Kiafrika imejaa mifano ya kibabedume. Hali hii huwashinikiza vijana wa kiume kuiga mifumo iliyowakandamiza wanawake. Hii huwafanya jinsia ya kiume kuonekana kama wakatili. Katika karne ya sasa, mabadiliko ya utawala wa kijinsia yamedhihirika. Makokha (2023) anaeleza kuwa katika riwaya nyingi, mwanaume mwenye udhaifu wa kihisia au asiyemiliki mali hupewa nafasi ya chini. Huchorwa kama mhusika dhaifu asiyefaa kuigwa. Hii inaafiki nadharia hii, inayoonesha jinsi jamii hujenga uanaume mmoja kuwa bora na mwingine duni. Wenye nguvu na ukakamavu ndio hutazamwa kama bora.

Nadharia hii huingiliana kwa karibu na fasihi. Fasihi hutumika kama kioo cha jamii katika kuonesha mitazamo ya kijinsia. Kwa kutumia nadharia hii, mchambuzi anaweza kuelewa jinsi

wahusika wa kiume wanavyowekwa katika nafasi za juu au za chini. Nadharia hii huipa fasihi uwezo wa kufichua mikakati ya udhibiti wa jinsia miongoni mwa vijana wa kiume.

Kwa madhumuni ya utafiti huu, mihimili minne iliteuliwa: (a) sifa za mwanaume hujengwa na imani, matarajio ya jamii na mazingira; (b) matarajio ya kijamii kuhusu uanaume huweza kuzalisha changamoto; (c) wanajamii huchangia kujenga hulka na maadili ya mtu; na (d) jamii hujenga na kugawa majukumu ya kijinsia. Mihimili hii ilitumika moja kwa moja katika Sura ya Nne na Tano.

(a) Sifa za mwanamume hutokana na misingi mbalimbali. Misingi hii ni imani yake, matarajio ya jamii, na maumbile yake ya kibayolojia (Connell, 1987). Mhimili huu unafaa lengo la kwanza la utafiti. Utafiti utachanganua usawiri wa vijana wa kiume katika riwaya za Mwenda Mbatia, ukiangalia mtangamano wao na jamii pamoja na mitazamo yao.

(b) Changamoto nyingi za jinsia ya kiume huletwa na jamii. Connell (1987) anajadili kuwa wanaume wasiodhihirisha ukakamavu hutazamwa kama hafifu. Mhimili huu utaufaa utafiti katika kuchambua changamoto za vijana wa kiume katika riwaya teule.

(c) Wanajamii huchangia hulka ya mtu. Mchango huu hutokana na mila, hadhi na mtazamo wa jamii. Malezi kutoka kwa wazazi huchangia maadili ya mtu. Mhimili huu utasaidia kuelewa mchango wa jamii katika maadili ya vijana wa kiume.

(d) Fikra za jamii huumba majukumu ya kijinsia. Majukumu ya wanawake na wanaume hutofautiana, na mafunzo yake huanzia familia. Jamii ina nafasi kubwa katika maisha ya mtu binafsi. Mhimili huu utaniongoza kuelewa sifa za vijana wa kiume na mchango wa jamii kwao.
Viunzi hivi vinne vilifaa sana utafiti huu. Vilitoa mwongozo wa uchambuzi wa malengo yake. Nadharia hii ina viunzi vingine pia:

(a) Majukumu ya binadamu hugawanywa kwa msingi wa kijinsia. Sherman na Wood (1982) wanaeleza kuwa mafunzo ya majukumu haya yalianzia familia, kisha yakawa sehemu ya jamii. Majukumu ya kiume na ya kike yalitofautiana.

(b) Wanajamii humtazama mwanaume kwa hadhi ya juu kuliko mwanamke. Connell (1987) anasema mawazo haya huchochewa na mila na desturi za jamii. Wakati mwingine hupitishwa kizazi hadi kizazi. Bly (1990) anaongeza kuwa wanaume weusi wamepinga desturi zinazojengwa kuhusu wanaume weupe, wakieleza kuwa hutazamwa duni zaidi.

(c) Jamii hubadilika kila wakati. Connell (2005) anasema tabia na maadili ya wanaume hubadilika kulingana na muktadha wa kijamii na wakati wa kihistoria. Mhimili huu huashiria mwamko mpya wa wanaume kutafakari nafasi yao jamiini.

(d) Jamii huundwa na makundi mbalimbali ya watu. Msanjila na wenzake (2011) wanaeleza kuwa wanajamii hugawika kitabaka: watawala na watawaliwa, wafanyakazi na waajiri, vijana na wazee, waliosoma na wasiosoma, wake kwa waume. Mhimili huu husaidia kuelewa uhusiano baina ya makundi hayo.

Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume ina nafasi muhimu katika kuchambua nafasi za kiume jamiini na katika fasihi. Husaidia kuchanganua mwingiliano wa wanaume na jamii, sifa zao, changamoto zao, na mchango wa wanajamii kwao.

Katika sura hii, utafiti ulionesha mapengo yaliyonuiwa kujazwa. Ilidhihirika kuwa watafiti wengi wamejikita katika nafasi ya jinsia ya kike, huku ile ya kiume ikitelekezwa. Hili ndilo pengo utafiti huu ulilonuia kuziba. Sura hii pia ilijadili kwa kina msingi wa nadharia hii, ikiangazia waasisi wake na mchango wao. Aidha, iliainisha mihimili mbalimbali na jinsi itakavyofaa utafiti huu.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.0. Utangulizi

Sura hii inawasilisha muundo na mbinu zilizotumika katika utekelezaji wa utafiti huu. Inaeleza muundo wa utafiti uliotumika, eneo la utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji, mbinu na vifaa vya ukusanyaji data, uchanganuzi na uwasilishaji wa data pamoja na uzingativu wa maadili ya utafiti. Aidha, sura inaeleza taratibu zilizofuatwa katika kupata, kupanga na kuchanganua data kutoka katika riwaya teule kwa kuzingatia malengo ya utafiti na mihimili ya Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume.

3.1. Muundo wa Utafiti

Muundo wa utafiti ni mpangilio unaoongoza hatua mbalimbali za utafiti. Unasaidia kufikia malengo yaliyokusudiwa. Akhtar (2016) anaeleza kuwa muundo wa utafiti unahusisha taratibu za ukusanyaji na uchanganuzi wa data. Taratibu hizi hulenga kujibu tatizo la utafiti. Enon (1998) anaeleza kuwa muundo wa kimaelezo hulenga kueleza sifa na hali ya jambo linalochunguzwa. Hutumia data za maelezo. Nassaji (2005) anaongeza kuwa muundo huu huwezesha mtafiti kutoa maelezo ya kina kuhusu jambo linalochunguzwa.

Utafiti huu ulitumia muundo wa kimaelezo. Ulilenga kueleza na kuchanganua usawiri wa vijana wa kiume. Ulichunguza pia changamoto zinazowakumba na mchango wa jamii katika kuwakuza, kama zinavyojitokeza katika Njozi Yapata Mtenzi (2018) na Utelezi (2023). Muundo huu ulifaa kwa utafiti kwa sababu mbalimbali. Uliwezesha mtafiti kuchunguza kwa kina wahusika, matukio na kauli. Uliwezesha pia uchunguzi wa mazingira na mahusiano yanayohusiana na vijana wa kiume. Aidha, ulisaidia data ya kifasihi kuelezwa na kufasiriwa. Ufasiri huu ulizingatia malengo ya utafiti na mihimili ya Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume.

3.2. Eneo la Utafiti

Creswell (2014) anajadili eneo la utafiti kama mazingira au eneo halisi ambako mtafiti hufanya uchunguzi. Uchunguzi huu hulenga kukusanya data. Eneo la utafiti huteuliwa kwa kuzingatia mada husika. Hutegemea pia uwezekano wa kupata data toshelevu. Eneo la utafiti huu ni riwaya. Utafiti huu unajadili uwakilishi wa vijana wa kiume. Unahusisha changamoto mbalimbali na nafasi

ya jamii katika kuwakuza kupitia matini za riwaya teule. Kifasihi, riwaya ni tanzu muhimu ya fasihi andishi. Humwezesha mwandishi kuwasilisha wahusika, matukio, mazingira na migogoro ya kijamii kwa upana (Wamitila, 2008). Sifa hii inaifanya riwaya kufaa kwa kuchunguza jinsi jamii inavyounda maisha ya vijana wa kiume.

Eneo hili lina mwelekeo wa kimuktadha na kithematiki. Kimuktadha, utafiti umezingatia mazingira ya kijamii katika Njozi Yapata Mtenzi (2018) na Utelezi (2023). Umeangazia mahusiano, matarajio ya kijinsia na mazingira yanayowazunguka vijana. Kithematiki, utafiti umejikita katika mada kuu tatu. Mada hizi ni taswira ya vijana wa kiume, changamoto zao, na nafasi ya jamii katika kuwakuza. Vipengele hivi vinaendana na malengo matatu ya utafiti. Vinawezesha uchunguzi wa vijana wa kiume kama wahusika waliojengwa ndani ya mazingira ya kijamii.

Uteuzi wa riwaya unatokana na nafasi yake katika Fasihi ya Kiswahili. Riwaya huweza kuibua na kuakisi masuala ya kijamii kupitia wahusika na matukio. Kwa msingi huo, riwaya teule zilitoa mazingira ya kimatini. Ndani yake, data kuhusu vijana wa kiume ilitambuliwa, kurekodiwa na kuchanganuliwa. Hivyo, eneo la utafiti halikuwa la kijiografia. Lilikuwa eneo la kitaaluma la Fasihi ya Kiswahili, likijikita katika matini za riwaya, na likiongozwa na mwelekeo wa kimuktadha na kithematiki.

3.3. Kundi Lengwa

Kundi lengwa la utafiti huu lilijumuisha riwaya za Kiswahili zilizoandikwa na Mwenda Mbatia. Kundi hili lilikuwa na riwaya kumi. Riwaya hizo ni Upotevu, Wimbo Mpya, Migogoro, Vipanya vya Maabara na Msururu wa Usaliti. Zinajumuisha pia Majira ya Tufani, Majilio ya Mkombozi, Njozi Yapata Mtenzi, Watoto wa Mwelusi na Utelezi. Kwa msingi huo, riwaya kumi ndizo zilizounda kundi lengwa la utafiti huu. Kundi hili lilikuwa msingi wa usampulishaji. Usampulishaji huu ulifanyika kupata riwaya zilizoteuliwa kwa uchanganuzi wa kina, kulingana na malengo ya utafiti.

3.4. Sampuli na Usampulishaji

Sampuli ya utafiti huu ilitokana na kundi lengwa la riwaya kumi za Mwenda Mbatia. Utafiti ulitumia usampulishaji wa kimakusudi. Njia hii ilisaidia kuteua riwaya zenye data inayohusiana na malengo ya utafiti. Usampulishaji ulizingatia uwepo wa wahusika vijana wa kiume. Ulizingatia pia matukio na mahusiano yanayowezesha kuchunguza taswira yao, changamoto zao, na nafasi ya jamii katika kuwakuza.

Kutokana na kundi hilo la riwaya kumi, riwaya mbili ziliteuliwa kama sampuli. Riwaya hizo ni Njozi Yapata Mtenzi (2018) na Utelezi (2023). Uteuzi wake ulizingatia uhusiano wa moja kwa moja na malengo matatu ya utafiti. Riwaya hizi zilitoa data ya kutosha kuchunguza usawiri wa vijana wa kiume, changamoto zao, na mchango wa jamii. Kwa hiyo, uteuzi haukufanywa kwa msingi wa uwakilishi wa kitakwimu. Ulifanywa kwa msingi wa ufaafu wa matini kwa malengo ya utafiti.

Uteuzi wa kimakusudi uliwezesha mtafiti kulenga matini zenye taarifa muhimu. Kwa kuwa utafiti huu ulikuwa wa kifasihi, riwaya mbili zilitosha kutoa data ya kina. Data hii ilihitajika kujibu maswali na kutimiza malengo ya utafiti. Aidha, uteuzi wa matini mbili uliwezesha uchanganuzi wa kina na ulinganisho. Ulinganisho huu ulizingatia vipengele vilivyobainishwa katika malengo na mihimili ya Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume.

3.5 Mbinu za Ukusanyaji Data

Data za utafiti huu zilikusanywa kwa njia mbili. Njia hizo ni usomaji wa karibu na unukuzi wa vifungu husika. Vifungu hivi vilitoka katika Njozi Yapata Mtenzi (2018) na Utelezi (2023). Usomaji wa karibu ulihusisha kuzisoma riwaya kwa kina na mara kadhaa. Lengo lilikuwa kutambua na kurekodi wahusika, matukio, kauli, mazingira na mahusiano. Vipengele hivi vilihusiana na taswira ya vijana wa kiume, changamoto zao, na nafasi ya jamii. Usomaji huu uliwezesha mtafiti kuchunguza data katika muktadha wa matini. Ulisaidia pia kubaini mifumo ya vipengele iliyohusiana na malengo ya utafiti.

Baada ya kubaini vifungu husika, mtafiti aliviunukuu na kuvirekodi. Aliambatanisha taarifa za mahali vilipopatikana, hususan ukurasa wa chanzo. Vifungu hivyo vilitumika kama ushahidi wa

msingi katika uchanganuzi wa data. Unukuzi uliwezesha kuhifadhi ushahidi kwa usahihi. Uliuhusisha pia na lengo husika la utafiti na mhimili wa Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume.

Usomaji wa karibu na unukuzi vilitosha kupata data iliyohitajika. Hii ni kwa sababu utafiti huu ulikuwa wa kifasihi. Vyanzo vikuu vya data vilikuwa riwaya mbili teule. Kwa hiyo, hakukuwa na haja ya hojaji au mahojiano. Mbinu nyingine za ukusanyaji data kutoka kwa wahojiwa nazo hazikuhitajika. Hata hivyo, mchakato wa ukusanyaji na upangaji wa data uliimarishwa kwa orodha ya uthibitishaji. Orodha hii ilisaidia kuhakikisha data iliyorekodiwa iliendana na malengo ya utafiti na mihimili ya nadharia.

3.5.1. Vifaa vya Kukusanya Data

Kifaa kikuu kilichotumika katika ukusanyaji na upangaji wa data kilikuwa Orodha ya Uthibitishaji (Checklist). Kifaa hiki kiliandaliwa kwa kuzingatia malengo matatu ya utafiti. Kilizingatia pia mihimili ya Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume. Orodha hiyo ilikuwa na vipengele kadhaa. Vipengele hivyo ni lengo la utafiti, kipengele kinachochunguzwa, mhusika au tukio, na dondoo la ushahidi kutoka riwayani. Ilijumuisha pia ukurasa wa chanzo na mhimili wa nadharia unaohusiana na data iliyobainika.

Katika ukusanyaji wa data, checklist ilitumika kurekodi vifungu husika. Vifungu hivi vilihusiana na usawiri wa vijana wa kiume, changamoto zao, na mchango wa jamii katika kuwakuza. Kila dondoo lilihusishwa na lengo husika la utafiti. Pale ilipohitajika, liliainishwa kwa mhimili wa nadharia uliotumika katika uchanganuzi. Utaratibu huu uliwezesha data kutoka riwaya mbili kupangwa kwa mfumo unaofanana. Ulirahisisha pia ulinganishaji wa ushahidi wa matini wakati wa uchanganuzi.

Aidha, kalamu na kitabu vilitumika kurekodi noti za awali wakati wa usomaji. Kipakatalishi kilitumika kuhamisha, kuhifadhi, kupanga na kuhariri data iliyokusanywa. Vifaa hivi vilikuwa vya usaidizi katika mchakato wa ukusanyaji na usimamizi wa data. Checklist ndiyo iliyobaki kuwa kifaa kikuu cha kurekodi na kupanga data ya utafiti.

3.6 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data

Data zilizokusanywa zilichanganuliwa kwa kuzingatia malengo matatu ya utafiti. Zilichanganuliwa pia kwa mihimili ya Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume. Baada ya vifungu husika kunukuliwa kutoka Njozi Yapata Mtenzi (2018) na Utelezi (2023), data zilipangwa katika makundi yanayolingana na malengo. Utaratibu huu ulihusisha kutambua, kupanga, kulinganisha na kutafsiri vifungu vya matini.

Kwa lengo la kwanza, data za usawiri wa vijana wa kiume zilitambuliwa na kupangwa. Zilipangwa kulingana na sifa, mienendo, mahusiano, kauli, matukio na mazingira. Data kutoka riwaya zote mbili zililinganishwa kubaini mifanano na tofauti. Vifungu vilivyobainishwa vilitafsiriwa kwa kuzingatia muktadha wa matini na mhimili wa nadharia husika.

Kwa lengo la pili, vifungu vya changamoto zinazowakumba vijana wa kiume vilitambuliwa na kuainishwa. Viliainishwa kulingana na aina za changamoto zilizojitokeza. Data hizo zililinganishwa katika riwaya zote mbili kubaini uwasilishaji wake. Uchanganuzi ulizingatia pia uhusiano wa matarajio ya kiuanaume na changamoto hizo, kwa mujibu wa nadharia.

Kwa lengo la tatu, data za mchango wa jamii zilitambuliwa na kuainishwa. Ziliainishwa kwa kuzingatia nafasi ya familia, rika, shule na mazingira mengine ya kijamii. Mchango huo ulichanganuliwa kama chanzo cha malezi na ujenzi wa tabia, au kama chanzo cha changamoto na shinikizo. Data za riwaya zote mbili zililinganishwa kubaini mfanano na tofauti.

Baada ya kuainisha data, mtafiti aliihusisha na mihimili husika ya nadharia. Lengo lilikuwa kufasiri maana ya ushahidi wa kifasihi. Uchanganuzi haukuzingatia tu kile kilichosemwa au kutendwa na wahusika. Ulizingatia pia muktadha wa matukio, mahusiano ya kijamii na matarajio ya kijinsia. Hatua hii iliwezesha mtafiti kwenda zaidi ya kunukuu vifungu. Alitoa ufafanuzi wa uhusiano wa ushahidi huo na malengo ya utafiti.

Data ziliwasilishwa kwa njia ya maelezo. Ziliwasilishwa chini ya mada na vijimada vilivyotokana na malengo ya utafiti katika Sura ya Nne. Dondoo kutoka riwayani zilitumika kama ushahidi wa

msingi wa hoja. Zilifuatiwa na uchanganuzi na mjadala wa mtafiti. Uwasilishaji huu ulionesha uhusiano kati ya ushahidi wa matini, malengo ya utafiti na mihimili ya nadharia.

3.7 Maadili ya Utafiti

Utafiti huu ulizingatia maadili ya kitaaluma katika hatua zote. Hatua hizi ni ukusanyaji, uhifadhi, uchanganuzi na uwasilishaji wa data. Kwa kuwa utafiti ulihusisha matini za kifasihi, mtafiti alihakikisha usahihi wa vifungu vilivyonukuliwa. Vifungu hivi vilihusishwa na vyanzo vyake. Aidha, mawazo na kazi za watafiti wengine zilitambuliwa. Zilitambuliwa kwa kutaja vyanzo husika, kuepuka wizi wa kitaaluma.

Data ya matini, noti za utafiti na nakala za kazi zilihifadhiwa kwa usalama. Zilitumika kwa madhumuni ya utafiti huu pekee. Mtafiti alihakikisha data haikubadilishwa wala kupotoshwa. Haikuwasilishwa nje ya muktadha wake kwa namna inayoweza kuathiri maana yake. Katika uwasilishaji wa matokeo, dondoo kutoka riwayani zilitambulishwa kwa usahihi. Zilirejelewa kulingana na vyanzo vyake.

Kwa upande wa vibali, mtafiti alipata ruhusa kutoka Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Afrika Mashariki. Aidha, NACOSTI ilitoa kibali cha kufanya utafiti. Kibali hiki kilizingatia taratibu na masharti ya mamlaka hiyo. Vibali hivyo vilizingatiwa katika utekelezaji wa utafiti. Kwa msingi huo, utafiti ulizingatia uadilifu wa kitaaluma, usalama wa data, na matumizi sahihi ya data.

SURA YA NNE

UCHANGANUZI NA UWASILISHAJI WA DATA

4.1. Utangulizi

Sura hii ilishughulikia uchanganuzi na uwasilishaji wa data. Ilijumuisha pia majadiliano ya matokeo ya utafiti. Katika sura hii, utafiti ulichanganua usawiri wa vijana wa kiume katika riwaya teule. Ulibainisha matatizo yanayowakumba. Ulibainisha pia mchango wa wanajamii katika kuwakuza. Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, iliyoasisiwa na Connell, R. (1987).

4.2. Vijana wa Kiume Walivyosawiriwa Katika Riwaya Teule.

Usawiri ni mbinu ya kifasihi. Mwandishi huitumia kuunda na kuwasilisha wahusika, mazingira, matukio au hisia. Lengo lake ni kufanikisha ujumbe wa kazi ya fasihi. Makokha (2011) anajadili usawiri kama chombo cha kuchambua uhalisia wa jamii ya Kiafrika. Anasisitiza umuhimu wa usawiri wa kimuktadha unaozingatia historia, utambulisho na mabadiliko ya kijamii. Usawiri husaidia kuibua maisha ya wahusika, muktadha wa kijamii, na dhamira ya kazi.

Wamitila (2008) anaeleza kuwa usawiri wa wahusika ni kitendo cha kuwachora na kuwafafanua. Ni pia kuwatambulisha na kuwajenga kwa maneno, matendo, hadhi na uwezo unaowiana nao. Watunzi hutumia mbinu mbalimbali kuwasawiri wahusika. Vijana wa kiume katika riwaya teule wamesawiriwa kwa njia tofauti kulingana na mtunzi.

Mhimili wa Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume unajadili chanzo cha sifa za mwanamume. Sifa hizi hutokana na mienendo yake, imani yake, na jinsi anavyotagusana na jamii (Connell, 1987). Katika kupambanua sifa hizo, mambo mengi huangaziwa. Mhimili huu umeongoza uchanganuzi wa jinsi Mwenda Mbatia amewasawiri wahusika wa kiume. Utafiti huu umeainisha sifa zao kama ifuatavyo:

4.2.1. Vijana wa Kiume kama Wasomi

Mwenda Mbatia anawasawiri vijana wa kiume kama wasomi wenye mwelekeo wa kufikia mafanikio kupitia elimu. Katika riwaya ya *Njozi Yapata Mtenzi* (2018), Kiguto anaoneshwa kuwa

kijana mwenye matarajio makubwa ya kielimu. Anatia bidii katika masomo yake kwa lengo la kufuzu na kujiunga na chuo kikuu. Connell (1987) anaeleza kuwa baadhi ya sifa zinazohusishwa na uanaume hujengwa kupitia imani, matarajio na mazingira ya kijamii. Kwa msingi huu, bidii ya Kiguto katika masomo inaweza kueleweka kama sehemu ya matarajio yake binafsi ya kujenga maisha yake kupitia elimu. Hatimaye, anafaulu mtihani wa kitaifa kwa kupata alama ya A, jambo linalovifanya vyuo vikuu vya nje ya nchi kuvutiwa na uwezo wake wa kitaaluma. Baada ya kushauriana na wazazi wake, anaamua kwenda Marekani kusomea uhandisi wa ndege.

> *Vyuo vikuu vya nje ya nchi ambavyo vilikuwa vikiwawinda wanafunzi bora kila mahali vilishindana kumsajilisha. Baada ya kuandikiana baruapepe kadha na babake na kushauriana na jamaa wengine, Kiguto aliamua kwenda Marekani kusomea uhandisi wa ndege. Alipata nafasi katika chuo kikuu ambacho kilikuwa tayari kumsajili. Lakini alilazimika kwanza kusoma kozi ya kiingilio ambayo ilichukua mwaka mmoja kumaliza. (uk. 160)*

Dondoo hili linaonesha kuwa usomi wa Kiguto hauishii katika kufaulu mtihani, bali unaendelea kuwa sehemu ya mchakato wa kujijenga na kutimiza matarajio yake ya baadaye. Uamuzi wake wa kusomea uhandisi wa ndege unaonesha kuwepo kwa azma ya kupata taaluma inayomuwezesha kujitegemea na kujenga hadhi yake. Kwa kuzingatia Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, hali hii inaendana na mhimili unaosisitiza kwamba sifa na mienendo inayohusishwa na uanaume hujengwa kupitia imani na matarajio ya mtu binafsi pamoja na mazingira yanayomzunguka. Hivyo, usomi wa Kiguto unajengwa kwanza na matarajio yake mwenyewe, kisha unawezeshwa na mazingira ya kifamilia na kielimu.

Mazingira ya kifamilia yanaonekana pia katika namna babake Kiguto anavyoweka msingi wa kufanikisha masomo yake. Hela zilizoachwa katika akaunti ya babake zinatumika kumsajili na kugharamia kozi aliyokusudia kufanya. Connell (1987) anasisitiza nafasi ya mazingira ya kijamii katika kujenga sifa na mienendo inayohusishwa na uanaume. Katika kisa hiki, malezi na maandalizi ya babake yanakuwa sehemu ya mazingira yanayomsaidia Kiguto kutimiza matarajio yake ya kielimu. Aidha, ami yake, jamaa na marafiki wanafurahia mafanikio yake na kusherehekea kufaulu kwake. Kwa hiyo, jamii ya karibu haijamwacha kijana huyu peke yake katika safari yake ya elimu, bali inampa uungwaji mkono unaochangia kuendeleza azma yake.

Usomi wa Kiguto unaendelea hata baada ya kuanza kazi ya polisi. Anaamua kujiandikisha katika chuo cha kutoa mafunzo ya polisi wa upelelezi ili kuongeza maarifa na ujuzi unaohitajika katika kazi yake.

> *Bila kupoteza wakati, Kiguto alienda moja kwa moja hadi katika chuo cha kutoa mafunzo ya polisi wa upelelezi. Akaonyeshwa ofisi iliyohusika na usajili. Humo alipewa maelezo kamili juu ya ratiba ya mafunzo, ada na muda wa kozi nzima. Alibaini kwamba iliwezekana kuhudhuria mafunzo sambamba na kazi yake. (uk. 5)*

Dondoo hili linapanua taswira ya Kiguto kama kijana anayeliona elimu kuwa mchakato unaoendelea hata baada ya kupata ajira. Kwa hiyo, mwandishi hamjengi kijana msomi kwa kumwonesha tu kama anayefaulu shuleni, bali pia kama anayejitahidi kuongeza maarifa na uwezo wake kulingana na mahitaji ya maisha na kazi. Kwa maoni ya mtafiti, taswira hii ni muhimu kwa sababu inaonesha kwamba usomi wa vijana wa kiume katika riwaya haujengwi kwa msingi wa ufaulu pekee, bali kama mkakati wa kujenga uwezo, hadhi na mustakabali wa kijana. Hivyo, elimu inakuwa nyenzo inayomsaidia Kiguto kujenga nafasi yake katika jamii.

Taswira kama hiyo inajitokeza pia kupitia Aroni. Aroni na Kiguto ni marafiki wa dhati tangu walipokuwa shuleni. Wote ni wanafunzi wenye uwezo mkubwa kitaaluma na hushindana katika kuongoza darasa lao. Ushindani huu unawachochea kuongeza bidii katika masomo yao.

> *Wote wawili walikuwa hodari masomoni. Katika mitihani ya mwisho wa muhula, Kiguto aghalabu aliongoza darasa lake la watu arobaini, huku akifuatwa na Aroni. (uk. 118)*

Dondoo hili linaonesha kwamba usomi wa vijana hawa unahusishwa pia na mahusiano yao na wenzao. Kwa mujibu wa Connell (1987), jamii na mahusiano ya kijamii huchangia katika ujenzi wa sifa zinazohusishwa na uanaume. Ushindani wa kitaaluma kati ya Kiguto na Aroni kwa hiyo unaonesha namna mazingira ya kijamii yanavyoweza kuwachochea vijana wa kiume kujenga uwezo na kujitahidi kufikia viwango vya juu. Aroni hatimaye anafaulu mtihani wake wa kitaifa na kupata nafasi ya kujiunga na chuo kikuu kusomea famasia. Baadaye anaonekana akiwa mwaka wa tatu katika masomo hayo.

Katika *Utelezi* (2023), taswira ya vijana wa kiume kama wasomi inajitokeza kupitia Tony na Filipo. Vijana hawa ni wanafunzi wa Shule ya Upili ya Baraka mjini Nakuru, shule ya kibinafsi ambayo inawalipisha wanafunzi karo ya kiwango cha juu.

Likizo iliisha haraka, shule zikafunguliwa kwa muhula wa kwanza. Tony na Filipo sasa walikuwa kidato cha nne. Wote wawili walisomea Shule ya Upili ya Baraka, mjini Nakuru. Hii ilikuwa shule ya kibinafsi ambayo ililipiwa karo ya maelfu ya pesa. (uk. 5)

Tony na Filipo wanaendelea kuonyeshwa kama wanafunzi wenye uwezo na matarajio makubwa ya kielimu. Wanapata tuzo za wanafunzi bora katika masomo mbalimbali na wanatarajia kujiunga na vyuo vikuu. Mwandishi anasema:

Somo la pili katika orodha yetu ni fizikia. Naye mwanafunzi bora zaidi katika somo hilo ni Tony Maselu! (uk. 14)

Aidha, mafanikio yao yanaendelea katika mihula inayofuata:

Katika mihula miwili tangu ule wa kwanza, waliendelea kupata tuzo za wanafunzi bora katika masomo mbalimbali. Ajabu ni kwamba masomo waliyopania kutuzwa kwayo, hususan hisabati kwa upande wa Tony na biolojia kwa upande wa Filipo, yalidhihirisha Utelezi mkubwa. (uk. 49)

Dondoo hizi zinaonesha kuwa Tony na Filipo wanawakilisha vijana wanaotambua elimu kama njia ya kufikia matarajio yao ya maisha. Hata hivyo, mwandishi haonyeshi usomi wao kama hali isiyoweza kuyumba. Tony anakumbwa na msiba wa kumpoteza babake wiki mbili kabla ya mtihani wa kitaifa. Pigo hilo linaathiri hali yake ya kisaikolojia na uwezo wake wa kukumbuka yale aliyokuwa ameyasoma.

Hatimaye, Tony alirudi shuleni. Lakini pigo la kumpoteza babake liliivuruga akili yake vibaya. Kweli alikuwa amejiandaa vizuri kwa mtihani. Hata hivyo, uchungu na majonzi yalifuta mengi ambayo alikuwa amehifadhi akilini katika kudurusu kwake. Mtihani ulianza akili yake ikiwa bado haijatulia. (uk. 51-52)

Hali hii ni muhimu katika kuielewa taswira ya kijana wa kiume kama msomi kwa sababu inaonesha kuwa uwezo wa kitaaluma huathiriwa na mazingira anayopitia kijana. Tony anapofanya mtihani akiwa katika hali ya majonzi, anapata alama ya C na kulazimika kurudia kidato cha nne. Hata hivyo, hakati tamaa. Ami yake anamshauri arudie mtihani akiwa private candidate na amhamie Nakuru ili aweze kupata mazingira yanayofaa ya kusoma.

Je, kuna mlango mwingine wa kuingilia chuo kikuu kusomea uhandisi ujenzi? Jawabu ni kwamba upo, japo utahitaji jitihada na ujasiri kuufikia. Napendekeza kwamba ujisajilishe kama private candidate wa KCSE mwaka huu na uanze kujiandaa kuufanya tena mtihani huo mwishoni mwa mwaka. (uk. 59)

Ushauri huu unaonesha kuwa mazingira ya kijamii yanaweza kuwa na nafasi katika kumsaidia kijana kukabiliana na kikwazo kinachohatarisha matarajio yake. Tony anakubali ushauri huo na baadaye anafanikiwa kujiunga na Chuo Kikuu cha Nairobi kusomea uhandisi. Filipo naye anapata nafasi ya kusomea uanasheria. Tony anaendelea na masomo yake hadi mwaka wa mwisho wa uhandisi ujenzi, huku Filipo akihitimu na kupata shahada ya uanasheria.

Jina langu ni Tony Maselu, mwanafunzi wa uhandisi ujenzi wa mwaka wa kwanza. Nina maswali mawili. (uk. 72)

Tony Maselu aliingia katika mwaka wake wa tano na wa mwisho katika masomo ya uhandisi ujenzi. Alikuwa na matumaini ya kufuzu mwishoni mwa mwaka huo wa 2010. Kwa jumla, maisha yake kama mwanafunzi katika Chuo Kikuu cha Nairobi yalikuwa mazuri... Wakati huu, binamuye, Filipo, alikuwa amemaliza masomo yake na kupata shahada ya uanasheria ambayo ilichukua muda wa miaka minne. Tayari alikuwa amejiunga na KSL (Kenya School of Law) kupata mafunzo ya uwakili. (uk. 92)

Taswira ya usomi inaendelezwa pia kupitia Rugwe na Michuki. Rugwe anahitimu chuo kikuu na kupata shahada ya kwanza katika historia na siasa, huku Michuki, ambaye ni kifungua mimba wa kina Ashime, akihitimu na kuwa mwalimu wa shule ya msingi. Kwa hiyo, riwaya inapanua taswira ya vijana wa kiume kwa kuwaonesha katika taaluma mbalimbali zinazotokana na mafanikio yao ya kielimu.

Kwa kuzingatia mifano hii kutoka katika riwaya zote mbili, mtafiti anaona kwamba Mbatia anajenga taswira ya kijana wa kiume msomi kupitia muunganiko wa matarajio binafsi, bidii, ushindani wa kitaaluma na msaada wa mazingira ya kijamii. Hivyo, usomi katika riwaya hizi hauwasilishwi kama sifa ya kuzaliwa nayo au sifa inayojitokeza bila sababu, bali kama matokeo ya mchakato wa kijamii na kibinafsi. Jambo la msingi linalojitokeza ni kwamba vijana wa kiume wanaoneshwa wakitumia elimu kama nyenzo ya kujenga maisha yao, kujitegemea na kupata nafasi katika jamii. Kwa misingi ya Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, hali hii inaafikiana na hoja

kwamba sifa na mienendo inayohusishwa na uanaume hujengwa kupitia imani, matarajio na mazingira ya kijamii. Kwa hiyo, taswira ya vijana wa kiume kama wasomi katika riwaya hizi inadhihirisha uhusiano kati ya matarajio ya kijana, mazingira yanayomzunguka na namna jamii inavyotambua mafanikio ya kielimu ya vijana wa kiume.

4.2.2. Vijana wa Kiume kama Wenye Bidii

Bidii ni juhudi anazoweka mtu ili kutimiza lengo fulani, hasa anapokabiliwa na vikwazo vinavyoweza kuzuia mafanikio yake. Duckworth (2016) anaeleza kuwa bidii huhusisha shauku na uvumilivu wa muda mrefu katika kufikia malengo. Katika muktadha wa utafiti huu, bidii inajitokeza kama sifa inayotumiwa na Mbatia kujenga taswira ya vijana wa kiume wanaojitahidi kufikia matarajio yao ya kielimu, kikazi na kijamii. Kwa hiyo, bidii ya vijana hawa haionekani tu kama juhudi binafsi, bali pia kama njia ya kufikia mafanikio yanayotarajiwa na wao wenyewe pamoja na jamii inayowazunguka.

Katika riwaya ya *Njozi Yapata Mtenzi* (2018), Kiguto anaoneshwa kuwa kijana mwenye bidii tangu akiwa mwanafunzi. Juhudi zake katika masomo zinamwezesha kupata mafanikio makubwa na kufikia matarajio yake ya kielimu. Mwandishi anasema:

> *Kila mtu aliyemfahamu Kiguto alitarajia kwamba angepita kwa alama za juu. Lakini alama zake zilikuwa hata juu kuliko matarajio ya wengi. Alipata A katika masomo yote. (uk. 159)*

Dondoo hili linaonesha kuwa bidii ya Kiguto inathibitishwa kupitia matokeo yake ya kitaaluma. Hata hivyo, kinachojitokeza zaidi ni kwamba mafanikio yake yanazidi matarajio ya watu waliomfahamu. Hivyo, Mbatia hamwonyeshi Kiguto kama kijana anayefanya juhudi bila mwelekeo, bali kama kijana mwenye matarajio yanayoeleweka na anayeyafikia kupitia kujituma. Mafanikio haya yanakuwa sehemu ya utambulisho wake na yanamwezesha kupata heshima na kutambuliwa na jamii.

Kiguto anaendeleza bidii yake hata baada ya kuamua kusomea uhandisi wa ndege. Mwandishi anaeleza:

> *Kiguto akajisajilisha na kuanza masomo. Kama kawaida, alitia bidii masomoni, akiwa na azma ya kutimiza ndoto yake ya kuwa mhandisi wa ndege. Mamake alishaubariki uteuzi wake wa taaluma. (uk. 160)*

Dondoo hili linaonesha uhusiano kati ya bidii, matarajio binafsi na msaada wa familia. Kiguto ana azma ya kutimiza ndoto yake, huku mamake akiunga mkono uchaguzi wake wa taaluma. Kwa kuzingatia Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, hali hii inaweza kuhusishwa na hoja kwamba mienendo na sifa zinazohusishwa na uanaume hujengwa katika mwingiliano wa matarajio binafsi na mazingira ya kijamii. Katika kisa cha Kiguto, bidii yake inaendeshwa na matarajio yake ya baadaye na wakati huo huo inaungwa mkono na familia.

Bidii ya Kiguto haikomei katika masomo. Baada ya kubadili mwelekeo wa maisha na kujiunga na mafunzo ya polisi, anaendelea kujitahidi hadi kuwa kurutu bora na baadaye kupandishwa cheo. Mwandishi anaeleza:

> *Kiguto sasa alikuwa inspekta mwenye umri wa chini zaidi katika jeshi zima la polisi. Jamaa na marafiki zake waliungana naye kusherehekea mafanikio haya. Kila mtu alikubali kwamba alistahili kupanda ngazi haraka. (uk. 275)*

Hapa bidii inahamishwa kutoka katika mazingira ya elimu hadi katika mazingira ya kazi. Mafanikio ya Kiguto yanatokana na kujituma kwake na yanathibitishwa na kupandishwa cheo. Aidha, jamaa na marafiki zake wanasherehekea mafanikio hayo, jambo linaloonesha kwamba bidii yake inatambuliwa na jamii. Kwa maoni ya mtafiti, Mbatia anatumia kupandishwa cheo kwa Kiguto kuonesha kwamba bidii ya kijana wa kiume inakuwa na maana pana zaidi inapozalisha mafanikio yanayotambuliwa na jamii. Hivyo, bidii inahusishwa na kujenga hadhi na nafasi ya kijana katika jamii.

Kiguto anaonesha bidii pia katika utekelezaji wa majukumu yake ya kikazi. Anafika kazini mapema na kufanya kazi kwa ueleledi. Bidii na uaminifu wake vinawafanya wakubwa na wafanyakazi wenzake kumuamini. Hata anapochelewa kazini na kutoa sababu ya ugonjwa, bosi wake haoni haja ya kutilia shaka maelezo yake kwa sababu tayari amejijengea sifa ya kuwa mchapa kazi na mwaminifu. Hali hii inaonesha kuwa bidii yake imekuwa sehemu ya utambulisho wake wa kikazi.

Katika *Utelezi* (2023), taswira ya vijana wa kiume wenye bidii inajitokeza kupitia Tony na Filipo. Tangu wakiwa shule ya upili, vijana hawa wanaoneshwa wakijitahidi katika masomo na kupata tuzo katika masomo mbalimbali. Mwandishi anasema:

Somo la pili katika orodha yetu ni fizikia. Naye mwanafunzi bora zaidi katika somo hilo ni Tony Maselu! (uk. 14)

Mafanikio haya yanaendelea katika mihula inayofuata ambapo Tony na Filipo wanapata tuzo katika masomo mbalimbali. Hali hii inaonesha kuwa bidii yao ni endelevu na si tukio la mara moja. Kwa hiyo, Mbatia anajenga taswira ya vijana hawa kama wanafunzi wanaoweka juhudi katika masomo yao na wanaoweza kubadilisha juhudi hizo kuwa mafanikio yanayotambulika.

Hata hivyo, Mbatia anaonesha kwamba bidii ya kijana inaweza kujaribiwa na mazingira magumu. Tony anakumbwa na changamoto ya kumpoteza babake wiki mbili kabla ya mtihani wa kitaifa. Msiba huo unaathiri maandalizi yake na hatimaye anapata alama ya C. Pamoja na kushindwa huku, Tony hakati tamaa. Anaamua kurudia mtihani wa kitaifa ili kuendelea na ndoto yake ya kusomea uhandisi ujenzi. Ami yake anamshauri:

Je, kuna mlango mwingine wa kuingilia chuo kikuu kusomea uhandisi ujenzi? Jawabu ni kwamba upo, japo utahitaji jitihada na ujasiri kuufikia. Napendekeza kwamba ujisajilishe kama private candidate wa KCSE mwaka huu na uanze kujiandaa kuufanya tena mtihani huo mwishoni mwa mwaka. (uk. 59)

Ushauri huu unaonesha kwamba bidii katika riwaya haihusiani tu na kufanya vizuri wakati mambo yanaenda vizuri, bali pia na uwezo wa kuendelea kujitahidi baada ya kushindwa. Tony anakubali ushauri wa ami yake na baadaye anafanikiwa kujiunga na Chuo Kikuu cha Nairobi kusomea uhandisi ujenzi. Filipo naye anafaulu na kujiunga na chuo kikuu kusomea uanasheria. Kwa mtazamo wa mtafiti, kisa cha Tony kinaifanya bidii ionekane kama uwezo wa kijana wa kiume kustahimili vikwazo na kuendelea kufuatilia lengo lake hata pale ambapo mazingira yanatishia kulivuruga.

Bidii ya Tony inaendelea hata baada ya kuhitimu. Anapokosa ajira nchini, anatafuta nafasi ya kufanya kazi nchini Sudan Kusini. Anaanza kufanya kazi katika shirika la Juba Road Construction na kujitahidi kutumia mapato yake kwa busara. Mwandishi anaeleza:

Mwanzoni mwa mwaka wa 2012, Tony alifika mjini Juba na kuanza kazi katika shirika la Juba Road Construction. (uk. 159)

Aidha:

Tony aliweza kuweka akiba ya nusu ya mshahara wake wa dola elfu tatu za Kimarekani. Alitambua kwamba kule nyumbani, wafanyakazi wachache sana walilipwa kiasi kikubwa kama hicho. (uk. 160)

Dondoo hizi zinaonesha mwendelezo wa bidii kutoka elimuni hadi kikazi. Tony hakubaki katika hali ya kukosa ajira. Alitafuta fursa nyingine na kujitahidi kuitumia kujenga maisha yake. Kuweka akiba ya mshahara kunaonesha mtazamo wa kupanga maisha ya baadaye. Kwa hivyo, bidii yake inaambatana na uwajibikaji na matarajio ya kujitegemea.

Kwa mujibu wa nadharia hii, bidii ya vijana hawa inaeleweka katika muktadha wa matarajio ya kiuanaume. Hata hivyo, data ya riwaya hizi inaonesha kuwa bidii haiwezi kuelezwa kwa matarajio ya jamii pekee. Vijana wenyewe wana matarajio binafsi yanayowasukuma kusoma na kufanya kazi. Yanawasukuma pia kuvumilia kushindwa na kutafuta fursa mpya. Mtafiti anaona kuwa Mbatia anajenga taswira ya vijana wenye bidii kama wanaotumia juhudi na uvumilivu kujenga maisha yao. Bidii inakuwa muhimu zaidi pale kijana anapokabiliwa na vikwazo, kwani ndipo uwezo wake wa kufuatilia malengo unapojitokeza wazi.

Kwa hiyo, taswira ya vijana wenye bidii inajengwa kupitia mambo matatu yanayohusiana. Mambo hayo ni matarajio binafsi, mazingira yanayowawezesha au kuwazuia, na hitaji la kufikia mafanikio yanayotambuliwa na jamii. Hii inaonesha kuwa bidii, kwa mtazamo wa Mbatia, si sifa ya mtu binafsi pekee. Ni sehemu ya mchakato mpana wa kujenga uwezo na nafasi ya kijana wa kiume jamiini.

4.2.3. Vijana wa Kiume kama Wenye Mapenzi ya Dhati

Mapenzi ya dhati ni kumpenda mtu kwa moyo wote na kujali ustawi wake. Katika riwaya teule, Mbatia anatumia sifa hii kujenga taswira ya vijana wa kiume wanaowathamini walio karibu nao. Mapenzi yao hujitokeza kupitia vitendo vya kujali, kusaidia na kuwajibika. Luyt (2017) anaeleza kuwa imani ya mtu binafsi ni miongoni mwa mambo yanayoathiri mienendo yake, kwa kuhusisha na nadharia hii. Kwa msingi huu, mapenzi ya dhati ya vijana hawa yanaeleweka kupitia imani na maamuzi yao binafsi, pamoja na mahusiano yao na wengine.

Katika Njozi Yapata Mtenzi (2018), Kiguto anaoneshwa kama kijana mwenye mapenzi ya dhati kwa watu wa karibu naye. Anayapenda hasa mamake Gasoya na mpenziwe Suzy. Mapenzi yake kwa mamake yanaonekana katika juhudi zake za kutafuta haki. Gasoya alifungwa kwa kosa asilolitenda. Baada ya kujiunga na polisi wa upelelezi, Kiguto anaendelea kufuatilia ushahidi wa kumsaidia mamake. Aidha, anamhusisha Suzy katika maamuzi muhimu ya maisha yake. Umuhimu wa Suzy katika maamuzi yake unaonekana katika kauli ifuatayo:

> *Kweli yalikuwa mafanikio makubwa, kwa sababu kati ya wote ambao alitafuta ushauri wao, Suzy ndiye aliyekuwa muhimu zaidi. Hata kama Aroni, ami yake na mamake wangekubali lakini Suzy akatae, angeacha. (uk. 225)*

Dondoo hili linaonesha kwamba mapenzi ya Kiguto kwa Suzy yanaathiri maamuzi yake binafsi. Anathamini maoni yake na kuyapa uzito katika maamuzi yanayohusu maisha yake. Kwa hiyo, mapenzi haya hayaishii katika hisia, bali yanajitokeza kupitia namna Kiguto anavyohusisha mtu anayempenda katika maamuzi yake muhimu. Kwa maoni ya mtafiti, jambo hili linaonesha kwamba Mbatia anajenga mapenzi ya dhati kama nguvu inayoweza kuathiri maamuzi na mienendo ya kijana wa kiume, badala ya kuyaonesha kama hisia za kimapenzi pekee.

Mapenzi ya Kiguto kwa watu wa familia yake yanaonekana pia katika namna anavyomsaidia mamake wa kambo katika shughuli za dukani. Ingawa bado ni mwanafunzi wa chuo kikuu, hutumia muda ambao hayuko shuleni kusaidia kazi za nyumbani na dukani. Mwandishi anaeleza:

Tena masomo yalikuwa ni ya siku tatu kwa juma. Jumatatu hadi Jumatano. Kwa hali hii, Kiguto alikuwa na nafasi tosha kusaidia kazi za nyumbani, na haswa dukani.

Hali hii inaonesha kwamba mapenzi ya Kiguto yanadhihirika kupitia kujitolea kwa watu wa familia yake. Anaunganisha majukumu yake ya masomo na wajibu wa kuwasaidia watu wa karibu naye. Kwa hiyo, taswira yake kama kijana mwenye mapenzi ya dhati inahusishwa na uwajibikaji na kujali ustawi wa wengine.

Mapenzi yake kwa mamake yanafikia kiwango cha juu zaidi anapochagua kufuatilia kesi iliyosababisha kufungwa kwake. Baada ya kuwa inspekta wa polisi, Kiguto anaanza upya uchunguzi wa kifo cha nyanyake na matukio yaliyohusishwa na kufungwa kwa mamake. Mwandishi anaeleza:

> *Mwavoya alikuwa dereva wa teksi aliyempeleka marehemu Nkitu - nyanyake Kiguto - mjini kuchukua kadi ya ATM. Ndiye aliyeshirikiana na wezi waliomteka nyara, kumwibia na kusababisha kifo chake. Ndiye aliyetoa ushahidi wa uongo mahakamani. Ilibainika kwamba wezi alioshirikiana nao walikuwa Wamoyo, Tonga na Kibetu. Huu ulikuwa ugunduzi muhimu sana. Sasa Kiguto alianza upya kufuatilia uhalifu huo uliofanyika miaka kadha iliyopita. (uk. 278)*

Uchunguzi huu unaonesha kwamba mapenzi ya Kiguto kwa mamake yanamsukuma kuchukua hatua ya kutafuta haki. Hivyo, mapenzi yanaunganishwa na ujasiri, kujitolea na uwajibikaji. Hatimaye, ushahidi anaokusanya unasaidia kubatilisha hukumu ya Gasoya na kumwezesha kuachiliwa.

> *Hatimaye, ushahidi uliotumiwa kumfunga Gasoya ulibomolewa, kisha ukateketezwa kama zile silaha za wapiganaji wa UHK. Mahakama ilibatilisha hukumu ya Gasoya, akaachiliwa. Alimshukuru Mungu kwa kutimiza ndoto yake. Ndoto ya kukombolewa na mwanawe. (uk. 279)*

Dondoo hili linathibitisha matokeo ya mapenzi ya Kiguto kwa mamake. Alijitolea katika kutafuta ushahidi na kufuatilia kesi hadi mamake akaachiliwa. Baada ya hapo, anaendelea kumsaidia kuanza maisha upya:

> *Kiguto alimsaidia mamake kuanza maisha upya. Kwa kuzingatia taaluma yake ya ualimu, alimnunulia shule ili aisimamie na kufundisha akitaka. Pia, alimjengea nyumba katika mtaa wa Ngomeni. (uk. 280)*

Kwa misingi ya Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, vitendo hivi vinaweza kueleweka kupitia nafasi ya imani binafsi katika kujenga mienendo ya mhusika. Kiguto anaamini kuwa anapaswa

kumsaidia mamake na kutafuta haki yake, na imani hiyo inamwelekeza kuchukua hatua. Mtafiti anaona kwamba katika kisa hiki Mbatia anavuka taswira ya kijana wa kiume kama mtu mwenye nguvu za kimwili pekee na kumjenga kama mhusika anayeweza kutumia uwezo wake, taaluma na mamlaka kumlinda na kumsaidia mtu mwingine. Hivyo, uanaume unaonyeshwa pia kupitia uwajibikaji na kujali wengine.

Katika *Utelezi* (2023), Tony anaoneshwa pia kuwa kijana mwenye mapenzi ya dhati kwa watu wanaohusika katika maisha yake. Mapenzi haya yanaonekana katika uhusiano wake na binamuye Filipo. Uhusiano wao unamwezesha Tony kumweleza Filipo tatizo linalomsumbua na kutafuta ushauri wake. Mwandishi anaeleza:

> *Uamuzi wa Tony kumtembelea Mwaguzi Kipofu ulitokana na mazungumzo kati yake na binamuye Filipo alipokwenda Nakuru na kumfichulia siri ya kugeuka kwake kuwa mkojozi katika utu uzima. Filipo ndiye aliyemsimulia juu ya mwanamke huyo aliyesemekana kwamba aliweza kuwatatulia watu shida ambazo ziliugomea utatuzi uliotumia njia za kikawaida. (uk. 217)*

Dondoo hili linaonesha kuwa uhusiano wa Tony na Filipo umejengwa juu ya kuaminiana na kusaidiana. Filipo anamjali Tony kiasi cha kumweleza kuhusu mtu anayeweza kumsaidia katika tatizo lake. Hivyo, mapenzi ya dhati katika riwaya hii yanajitokeza pia katika mahusiano ya kindugu na kifamilia, si katika mahusiano ya kimapenzi pekee.

Tony anaonesha mapenzi yake kwa wadogo wake kwa kuwahimiza kufanya vizuri katika masomo. Hata wakati wa likizo, yuko tayari kutumia muda wake kuwasaidia. Anasema:

> *Nimeshaongea nao, baba. Wameniahidi kwamba watajifunga kibwebwe na kuboresha maksi zao. Mbali na kubukua kwangu likizo hii, nitawasaidia katika masomo yao. Mambo yatakuwa mazuri. (uk. 34)*

Hapa mapenzi yanaonekana kupitia kujitolea kwa ajili ya maendeleo ya wengine. Tony hatumii muda wake wa likizo kwa manufaa yake pekee, bali anautumia pia kuwasaidia wadogo wake. Kwa maoni ya mtafiti, mfano huu unaonesha kwamba Mbatia anahusisha mapenzi ya dhati na malezi,

ushauri na uwezeshaji wa vijana wengine. Hivyo, kijana wa kiume anasawiriwa kama mtu anayeweza kuwa chanzo cha maendeleo kwa watu walio karibu naye.

Tony pia anawapenda na kuwaheshimu wazazi wake. Aidha, anaamua kufuata nyayo za babake katika taaluma ya uhandisi. Anamheshimu pia ami yake na kumhusisha katika maamuzi muhimu ya maisha yake. Anapopanga kwenda Sudan Kusini kutafuta ajira, anamshirikisha ami yake kwanza:

> *Akalijadili wazo lake na ami yake. Nkalai alikubaliana naye kwamba taaluma yake haikumfunga kutafuta riziki nchini mwake tu. Kama kulikuwa na nafasi za kazi Sudani Kusini, hapakuwa na ubaya wowote kutuma maombi huko. (uk. 159)*

Ushahidi huu unaonesha kwamba Tony anathamini ushauri wa watu wa familia yake na hujenga maamuzi yake kwa kuzingatia mahusiano hayo. Kwa hiyo, mapenzi ya dhati yanaonekana pia kupitia heshima, ushirikishwaji na kuthamini ushauri wa ndugu.

Mapenzi ya Tony yanaonekana pia katika uhusiano wake na Doris. Anapokuwa mjamzito, Tony anajitahidi kutafuta ajira ili aweze kuihudumia familia yake. Baada ya kupata kazi Sudan Kusini, anataka Doris na mwanawe wamsafiri ili waishi pamoja. Ingawa juhudi zake hazifanikiwi na baadaye Doris anamsaliti, kitendo cha Tony kutafuta ajira na kutaka familia yake iwe pamoja kinaonesha kujali ustawi wa watu anaowapenda.

Kwa kuzingatia ushahidi kutoka katika riwaya zote mbili, mtafiti anaona kwamba Mbatia anawasawiri vijana wa kiume wenye mapenzi ya dhati kama wahusika ambao hisia zao hubadilika kuwa vitendo vya uwajibikaji, msaada, ulinzi na kujitolea. Kiguto anatumia taaluma na uwezo wake wa kiupelelezi kumkomboa mamake, huku Tony akitumia muda na uwezo wake kuwasaidia wadogo zake na kushirikisha familia katika maamuzi yake. Hivyo, mapenzi ya dhati katika riwaya hizi hayaishii katika uhusiano wa kimapenzi, bali yanaenea katika mahusiano ya kifamilia, kindugu na kijamii.

Kulingana na Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, mifano hii inaonesha namna imani binafsi na mazingira ya mahusiano yanavyoweza kuchangia katika kujenga mienendo ya vijana wa kiume. Hata hivyo, uchanganuzi wa mtafiti unaonesha jambo pana zaidi: Mbatia anapanua dhana ya

uanaume kwa kuhusisha mafanikio ya kijana wa kiume si tu na uwezo wa kutawala au kuwa na mamlaka, bali pia na uwezo wa kujali, kuwajibika na kutumia nafasi aliyonayo kwa manufaa ya wengine. Kwa hiyo, taswira ya vijana wa kiume wenye mapenzi ya dhati katika riwaya hizi inadhihirisha uanaume unaodhihirishwa kupitia uwajibikaji na mahusiano ya kujenga, sambamba na matarajio ya kijamii yanayomzunguka kijana.

4.2.4. Vijana wa Kiume kama Wapelelezi

Upelelezi ni mchakato wa kuchunguza uhalifu au fumbo kwa kukusanya vidokezo, kuchambua ushahidi na kutumia mantiki ili kufikia ukweli. Link (2023) anaeleza kuwa upelelezi huhitaji uchunguzi makini unaomwezesha mpelelezi kufumbua siri iliyojificha. Katika riwaya teule, Mbatia anawasawiri baadhi ya vijana wa kiume kama wapelelezi wanaotumia uwezo wao wa kufikiri, kukusanya ushahidi na kufuatilia matukio ili kufikia ukweli. Taswira hii inajitokeza kwa kiwango kikubwa kupitia Kiguto katika *Njozi Yapata Mtenzi* (2018), huku katika *Utelezi* (2023), kipengele cha upelelezi kikijitokeza kupitia Tony katika jitihada zake za kutafuta suluhisho la tatizo linalomkabili.

Katika *Njozi Yapata Mtenzi* (2018), Kiguto anajengwa kama kijana mwenye uwezo wa kufanya upelelezi kwa kutumia mbinu mbalimbali na kwa kuzingatia taratibu za kisheria. Anapopewa jukumu la kumtafuta Onemi ili kupata pesa alizoachiwa na babake, hutumia mbinu mbalimbali za kumfuatilia. Onemi anajaribu kumtoroka kwa kubadilisha magari, lakini Kiguto anatumia mbinu nyingine na kuwashirikisha Chokora katika ufuatiliaji huo. Hatimaye, mpango wake unafanikiwa na Onemi anakamatwa. Mwandishi anaeleza:

> *Mpango wa Kiguto wa kuwashirikisha chokora katika kumtafuta Onemi ulifanikiwa sana. Alijaribu kila mbinu kukwepa, lakini baada ya majuma mawili, alipatikana. Mbinu ya kubadilishabadilisha magari aliyotumia kwa muda mrefu haikumsaidia. Akakabiliana na Kiguto uso kwa uso. Mwanzoni alikana kuwepo kwa kibweta cha almasi, lakini Kiguto akamtolea ushahidi wa ule mkataba ambao ulikuwa umetiwa sahihi na marehemu babake, Onemi na wakili. Onemi hakuwa na njia ya kukwepa tena. Hofu ilimsukuma zaidi kumpa Kiguto hela zake. Isitoshe, Kiguto alikuwa inspekta wa polisi wa upelelezi aliyeogopwa sana na wahalifu. Tena alikuwa na ushahidi kamili na aliweza kumshtaki Onemi. Akasalimu amri na kukubali kumgawia Kiguto shilingi milioni mia moja.* (uk. 277)

Dondoo hili linaonesha kuwa upelelezi wa Kiguto haukutegemea nguvu za kimwili pekee, bali ulihusisha uwezo wa kupanga, kufuatilia, kutumia taarifa na kukusanya ushahidi. Pia, anapowashirikisha Chokora katika kumtafuta Onemi, anaonesha uwezo wa kutumia watu na mazingira yanayomzunguka kufikia lengo lake. Hatimaye, ushahidi wa mkataba unakuwa muhimu katika kumfanya Onemi ashindwe kuendelea kukwepa.

Kwa kuzingatia Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, taswira hii inaweza kuhusishwa na namna mazingira ya kijamii yanavyoweza kujenga sifa na uwezo unaohusishwa na uanaume. Kiguto amepata mafunzo ya polisi wa upelelezi na anatumia taaluma hiyo katika kutatua matatizo yanayomkabili. Hivyo, upelelezi wake unaonesha uhusiano kati ya mafunzo, mazingira ya kikazi na uwezo binafsi wa kutumia maarifa katika kutatua matatizo. Kwa maoni ya mtafiti, Mbatia anamjenga Kiguto kama kijana wa kiume ambaye nguvu yake haionekani katika matumizi ya nguvu za mwili pekee, bali pia katika uwezo wa kufikiri kimkakati, kuchanganua ushahidi na kutumia maarifa kutafuta ukweli.

Uwezo huu wa Kiguto wa kupeleleza unaonekana kwa kiwango kikubwa zaidi katika suala la kesi ya mamake, Gasoya. Kiguto anaamini kuwa mamake alifungwa kwa kosa ambalo hakulitenda. Kwa hiyo, anaamua kufuatilia upya kesi hiyo licha ya muda mrefu kupita na baadhi ya wahusika wa awali kuwa wamefariki. Katika uchunguzi wake, anamtafuta Mwavoya ambaye alikuwa dereva wa teksi aliyehusishwa na uhalifu uliosababisha kifo cha nyanyake Kiguto. Mwandishi anaeleza:

> *Sasa Kiguto alianza upya kufuatilia uhalifu huo uliofanyika miaka kadha iliyopita. Kwa bahati mbaya, wale wahudumu katika shamba la marehemu nyanyake, walishakufa, lakini Mwavoya alipatikana. Bado alikuwa akiendesha biashara yake ya teksi ambayo ilikuwa maficho ya uhalifu. Kiguto alimkamata na kumpeleka katika kituo cha polisi. Mwavoya akatumbukizwa rumande kusubiri kufunguliwa mashtaka.* (uk. 278)

Uchunguzi huu unaonesha uvumilivu na umakini wa Kiguto katika kutafuta ukweli. Hata baada ya miaka mingi kupita, haachani na suala hilo kwa sababu anaamini kuwa haki haikutendeka. Anaendelea kukusanya ushahidi na kuwatafuta watu waliohusika katika tukio hilo. Baada ya kupata ushahidi wa kutosha, anamtafuta wakili wa marehemu babake na kumwelekeza kutumia ushahidi huo katika kufufua kesi.

Baada ya kukusanya ushahidi wa kutosha, Kiguto alimtafuta yule wakili wa marehemu babake. Alishahamia jijini baada ya kufanya kazi nchini Sierra Leone kwa miaka mingi. Alimpa maagizo ya kuifufua kesi ya mamake na kutumia ushahidi uliopatikana. (uk. 277)

Ushahidi huo hatimaye unasaidia kufufua kesi na kuthibitisha kuwa mashtaka dhidi ya Gasoya yalikuwa ya uongo. Mahakama inabatilisha hukumu yake na kumwachilia huru.

Hatimaye, ushahidi uliotumiwa kumfunga Gasoya ulibomolewa, kisha ukateketezwa kama zile silaha za wapiganaji wa UHK. Mahakama ilibatilisha hukumu ya Gasoya, akaachiliwa. Alimshukuru Mungu kwa kutimiza ndoto yake. Ndoto ya kukombolewa na mwanawe. (uk. 279)

Kwa mujibu wa Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, mienendo ya mwanaume inaweza kuhusishwa na mazingira ya kijamii na matarajio yanayomzunguka. Katika kisa hiki, Kiguto anatumia nafasi yake kama polisi na ujuzi wa upelelezi kutafuta haki kwa mamake. Mtafiti anaona kwamba upelelezi wa Kiguto unaonesha namna mamlaka ya kitaaluma inaweza kutumiwa kwa manufaa ya wengine. Kwa hiyo, Mbatia hamjengi kijana wa kiume mwenye mamlaka kama mtawala wa wengine, bali kama mtu anayeweza kutumia mamlaka na maarifa yake kutatua matatizo na kurekebisha hali ya ukosefu wa haki.

Katika *Utelezi* (2023), taswira ya kijana wa kiume anayechunguza tatizo lake mwenyewe inajitokeza kupitia Tony Maselu. Tony anakumbwa na tatizo la kuwa kikojozi akiwa katika ujana. Baada ya kwenda hospitalini bila kupata suluhisho, anaamua kutafuta njia nyingine ya kulielewa tatizo hilo. Anazungumza na binamuye Filipo, ambaye anamweleza kuhusu Mwaguzi Kipofu.

Uamuzi wa Tony kumtembelea Mwaguzi Kipofu ulitokana na mazungumzo kati yake na binamuye Filipo alipokwenda Nakuru na kumfichulia siri ya kugeuka kwake kuwa mkojozi katika utu uzima. Filipo ndiye aliyemsimulia juu ya mwanamke huyo aliyesemekana kwamba aliweza kuwatatulia watu shida ambazo ziliugomea utatuzi uliotumia njia za kikawaida. (uk. 217)

Uamuzi wa Tony wa kutafuta suluhisho unaonesha kuwa hakubali kubaki katika hali ya kutokujua chanzo cha tatizo lake. Anatafuta taarifa, anashauriana na mtu anayemwamini na hatimaye anafuata njia anayodhani inaweza kumsaidia. Juhudi zake zinafanikiwa na tatizo hilo linatoweka:

Shida yake ya kuwa mkojozi ilitoweka siku ile aliyotoka kwa mwuguzi. (uk. 222)

Ingawa upelelezi wa Tony unatofautiana na ule wa Kiguto kwa sababu hauhusiani na uchunguzi wa uhalifu, wote wana sifa ya kutafuta suluhisho kwa tatizo linalowakabili. Kiguto hutumia mafunzo yake ya polisi na ushahidi katika kutafuta ukweli, huku Tony akitumia mawasiliano na taarifa anazopata kutoka kwa Filipo katika kutafuta suluhisho la tatizo lake. Kwa maoni ya mtafiti, tofauti hii ni muhimu kwa sababu inaonesha kwamba Mbatia anatumia dhana ya upelelezi kwa upana, kama uwezo wa kijana wa kiume kutafuta majibu na suluhisho badala ya kukubali hali inayomkabili bila kuchukua hatua.

Kwa kuzingatia mifano kutoka katika riwaya hizi mbili, mtafiti anaona kwamba taswira ya vijana wa kiume kama wapelelezi inajengwa kupitia uwezo wa kuchunguza, kutafuta taarifa, kuvumilia katika mchakato wa kutafuta ukweli na kutumia maarifa kutatua matatizo. Kiguto anawakilisha upelelezi wa kitaaluma na kisheria unaolenga kupata haki, ilhali Tony anawakilisha utafutaji wa suluhisho la tatizo binafsi kupitia ushauri na uchunguzi. Kwa hiyo, taswira hii inapanua uelewa wa uanaume katika riwaya hizi kwa kuonesha kwamba uwezo wa kijana wa kiume unaweza kudhihirishwa kupitia akili, maarifa, uchunguzi, uvumilivu na matumizi ya mamlaka kwa madhumuni ya kutatua matatizo.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, mazingira ya kijamii na nafasi anazopewa vijana zinaweza kuchangia katika kujenga uwezo na mienendo yao. Hivyo, mtafiti anahitimisha kwamba Mbatia anawasilisha upelelezi kama mojawapo ya njia ambazo vijana wa kiume hujenga na kuonesha uwezo wao katika jamii. Taswira hii inadhihirisha kwamba uanaume katika riwaya teule hauhusishwi tu na nguvu au mamlaka, bali pia na uwezo wa kutumia maarifa na fikra katika kukabiliana na changamoto na kutafuta suluhisho.

4.2.5. Vijana wa Kiume kama Wenye kubadilika

Wenye kubadilika ni vijana wanaoweza kubadili mienendo au tabia zao. Mabadiliko hayo hutokana na uzoefu wanaoupata maishani. Yanaweza kuwa chanya au hasi, kutegemea mazingira yanayoyachochea. Katika utafiti huu, kubadilika kunahusishwa na uwezo wa kijana kuacha mienendo isiyokubalika. Kunahusishwa pia na uwezo wa kujenga mwenendo unaomwezesha kushirikiana vyema na jamii. Janvan (2023) anaeleza kuwa nadharia hii inatambua matarajio ya jamii kuhusu mwenendo wa mwanaume. Matarajio hayo yanaweza kumfanya mwanaume

kujirekebisha. Hivyo, mabadiliko ya tabia yanaweza kueleweka kama sehemu ya mchakato wa kijana kujenga upya hadhi yake jamiini.

Katika Njozi Yapata Mtenzi (2018), taswira ya kijana anayebadilika inajitokeza kupitia Kibetu. Awali, Kibetu anahusishwa na uhalifu pamoja na Okuti na Nyangwe. Hata hivyo, baada ya kulazwa hospitalini, anabadilisha mwenendo wake. Anaamua kuachana na uhalifu. Badala yake, anaanza kumsaidia Kiguto katika upelelezi unaolenga kukomesha uhalifu jamiini. Mabadiliko haya yanaonekana katika dondoo lifuatalo:

> *Kibetu alipotoka hospitalini baada ya kulazwa kwa juma moja, alianza kumsaidia Kiguto katika upelelezi. Ndipo inspekta huyo alipogundua kwamba mui huwa mwema. Kibetu aliamua kuachana kabisa na uhalifu. Akajaribu kulipia kwa mema yote ambayo Kiguto alikuwa amemtendea kwa kumsaidia katika upelelezi. Kiguto alifurahishwa sana na mabadiliko yake. Akamwajiri kama wakala wake katika usimamizi wa yale majumba ya Ngomeni.* (uk. 277-278)

Dondoo hili linaonesha mabadiliko ya Kibetu kutoka uhalifu kwenda uwajibikaji na ushirikiano. Mabadiliko yake hayaishii katika kuacha uhalifu. Yanaonekana pia katika hatua za kumsaidia Kiguto katika upelelezi. Baadaye, Kibetu anapewa jukumu la kusimamia majengo ya Ngomeni. Kwa hiyo, Mbatia anatumia mabadiliko yake kuonesha kuwa kijana wa kiume anaweza kujenga upya mwenendo na nafasi yake jamiini. Hii hutokea baada ya kupitia uzoefu unaomfanya kutathmini upya maisha yake.

Kwa mtazamo wa nadharia hii, mabadiliko haya yanahusishwa na athari za mazingira na mahusiano ya kijamii. Kibetu anapopata nafasi ya kushirikiana na Kiguto, anahamia kutoka mazingira ya uhalifu kwenda mazingira yanayompa fursa ya kutumia uwezo wake kwa manufaa ya jamii. Hivyo, mabadiliko yake si uamuzi wa mtu binafsi pekee. Ni matokeo ya mwingiliano wa matakwa yake, mazingira yake, na mahusiano yake na wengine.

Kwa mtazamo wa mtafiti, Mbatia anawasawiri vijana wenye kubadilika kama wanaoweza kujirekebisha kutokana na uzoefu na mazingira. Kibetu ni mfano wa kijana aliyeanza na mwenendo wa uhalifu, lakini akabadili mwelekeo wa maisha yake. Anatumia uwezo wake katika

shughuli zinazomnufaisha yeye na jamii. Taswira hii inapinga mtazamo kwamba kijana wa uhalifu hawezi kubadilika. Inasisitiza kuwa mazingira yanayompa kijana nafasi ya kujirekebisha yanaweza kuchangia mwenendo mpya.

Kwa jumla, taswira ya kubadilika inaonesha kuwa uanaume katika riwaya hizi haujengwi kwa sifa zisizobadilika. Vijana wanaweza kubadili tabia zao wanapokutana na uzoefu na mazingira yanayowachochea kutathmini upya mwenendo wao. Mbatia anapanua uelewa wa uanaume. Anaonesha kuwa uwezo wa kujirekebisha na kutumia uwezo binafsi kwa manufaa ya jamii ni sehemu muhimu ya taswira ya kijana wa kiume.

4.2.6. Vijana wa Kiume kama Wakatili

Ukatili katika muktadha wa utafiti huu haujitokezi kama kitendo cha mtu binafsi pekee, bali unaonekana pia katika mahusiano ya mamlaka, mazingira ya kijamii na matarajio kuhusu namna mwanaume anavyopaswa kujitenda. Carney na wenzake (2022) wanaonesha kuwa vitendo vya ukatili vinapoachwa bila kukemewa vinaweza kudhoofisha utu wa waathiriwa na kuathiri ustawi wa jamii. Kwa hiyo, katika kuchanganua taswira ya vijana wa kiume wakatili, ni muhimu kuangalia si tu vitendo wanavyofanya, bali pia mazingira yanayowezesha au kuchochea mienendo hiyo.

Katika *Njozi Yapata Mtenzi* (2018), taswira ya kijana wa kiume mkatili inajitokeza kupitia kijana mwenye klabu anayemfanyia Monika ukatili baada ya kukataa ombi lake la kufanya naye mapenzi. Kijana huyo anamnyanyasa kwa maneno na hatimaye kumpiga kiasi cha kuzimia. Mbatia anaeleza:

> *Mwanawe mwenye klabu aliingia klabuni, akanywa na kulewa. Halafu akaanza kumtongoza Monika. Kwa vile hakutaka kufanya mapenzi naye, kama alivyotaka, alimwita malaya mwenye maringo, kisha akampiga kofi. Wakaanza kupigana. Kijana huyo pandikizi la mtu alimpiga vibaya, akaanguka na kuzirai. Wahudumu wengine walimbeba na kumpeleka chumbani mwake, wakammwagia maji mpaka akapata fahamu. Bado alikuwa akihisi maumivu kifuani.* (uk. 148)

Dondoo hili linadhihirisha ukatili unaotokana na kijana kutaka kulazimisha matakwa yake kwa kutumia nguvu. Kukataa kwa Monika kufanya naye mapenzi kunamfanya kijana huyo kutumia

lugha ya kumdhalilisha na kisha nguvu za kimwili. Kwa mtazamo wa kijinsia, kitendo hiki kinaonesha namna baadhi ya matarajio kuhusu uanaume yanavyoweza kujengwa juu ya dhana ya mwanaume kuwa na mamlaka juu ya mwanamke. Hivyo, ukatili wake unaambatana na jaribio la kuthibitisha mamlaka na uwezo wake wa kutawala mwingine.

Taswira ya ukatili inaendelezwa kupitia Okuti na Nyangwe, ambao wanahusika katika wizi wa fedha benki na baadaye kumuua dereva aliyeshirikiana nao. Dereva huyo anapigwa risasi kwa sababu wahusika hao hawakutaka kugawana fedha walizoiba. Mhusika huyo anasema:

> *Alimkuta dereva wa gari chapa ya Range Rover aliyekuwa amepigwa risasi kifuani akiwa katika dakika za mwisho za uhai wake. Pindi alipomuona, alianza kububujikwa na maneno. "Wameniua! Mungu mmoja... wameniua na pesa wamechukua. Zote milioni tatu. Hawakutaka tugawane. Fisi hao wanataka kuzila peke yao. Wallahi hawatazila. Vile wameniua, ndivyo watauliwa..."* (uk. 11)

Ushahidi huu unaonesha kuwa ukatili wa Okuti na Nyangwe hauishii katika kuvunja sheria, bali unafikia kiwango cha kuondoa uhai wa mwenzao kwa ajili ya manufaa binafsi. Mbatia hivyo anajenga taswira ya vijana ambao tamaa ya mali na matumizi mabaya ya nguvu vinawafanya kuona maisha ya wengine kuwa kikwazo cha kutimiza malengo yao. Ukatili huo unaendelezwa zaidi katika riwaya pale ambapo inabainika kuwa vijana hao walihusika katika utekaji nyara, unyang'anyi, uuzaji wa mihadarati, ajira ya watoto na mauaji ya polisi. Hatimaye, wanahukumiwa kutiwa kitanzi:

> *Baada ya kesi ya Okuti na Nyangwe kuendelea kwa miezi miwili, hukumu ilitolewa. Ilithibitishwa kwamba walihusika na unyang'anyi, utekaji nyara, uuzaji wa mihadarati, ajira ya watoto na mauaji ya polisi. Walihukumiwa kutiwa kitanzi.* (uk. 228)

Aidha, Kibetu anaonekana katika mtandao wa ukatili kupitia ushiriki wake pamoja na Tonga, Mwavoya na Wamoyo katika utekaji nyara wa Nkitu, nyanyake Kiguto. Utekaji huo unaishia katika kifo cha Nkitu. Dondoo lifuatalo linaonesha nafasi ya Kibetu katika tukio hilo:

> *Mwavoya alikuwa dereva wa teksi aliyempeleka marehemu Nkitu, nyanyake Kiguto, mjini kuchukua kadi ya ATM. Ndiye aliyeshirikiana na wezi waliomteka nyara, kumwibia na kusababisha kifo chake. Ndiye aliyetoa ushahidi wa uongo mahakamani. Ilibainika kwamba wezi alioshirikiana nao walikuwa Wamoyo, Tonga na Kibetu.* (uk. 278)

Katika *Utelezi* (2023), taswira ya vijana wa kiume wakatili inajitokeza kupitia Kiragi, ambaye anakubali kushirikiana na shangazi yake katika kumuua mhandisi Maselu. Anatekeleza mpango huo kwa kumwangushia karai la chuma lililojaa zege ili kifo hicho kionekane kama ajali. Mpango huo unafichuka baada ya mazungumzo yao kunaswa na kifaa cha kurekodia sauti. Selina anagundua mpango huo kupitia ushahidi huo:

> *Tulipoondoka baada ya kunywa chai, alisahau juu ya tarakilishi Dictaphone yake ya kunasia na kuhifadhia sauti. Kifaa kidogo chenye umbo la flash disk ambacho unaweza kubeba mfukoni. Hamkukigundua wakati mkiongea na kukubaliana kiasi utakacholipwa kwa kutumika kama mkono wa mauti. Kumuua Maselu kwa kumwangushia karai la chuma lililojaa zege. Mkakubaliana kwamba utalipwa laki nne. Laki mbili kabla ya kutekeleza kitendo hicho, na laki mbili ukishatekeleza. Basi kinasasauti cha shogangu kilinasa kila kitu.* (uk. 125-126)

Dondoo hili linaonesha ukatili uliopangwa kwa makusudi na unaohusisha malipo ya fedha. Kiragi hakushiriki tu katika kutekeleza mauaji, bali alikubali kuwa sehemu ya mpango wa kumuondoa mtu mwingine kwa manufaa ya kifedha. Baada ya kutotekelezwa kwa makubaliano ya malipo, anaendelea na mienendo ya kulipiza kisasi kwa kupanga namna ya kumuondoa shangazi yake. Hali hii inaonesha kuwa ukatili kwa Kiragi unakuwa sehemu ya namna ya kukabiliana na migogoro na kutafuta masuluhisho kwa kutumia nguvu na mauaji.

Ukatili unaendelezwa pia na Kimuta, rafiki wa Kiragi, ambaye anakiri kumuua tajiri mmoja kwa sumu. Anasimulia jinsi alivyomfuatilia mtu huyo na kumpa sumu kwa siri:

> *Mara tajiri mwenye kitambi akainuka na kuelekea msalani. Sekunde chache baadaye, Kimuta naye akainuka. Aligeuka huku na huko kuhakikisha kwamba hamna mhudumu au mteja aliyekuwa karibu. Kisha akapita karibu na bilauri ya adui yake na kurusha ile punje ya sumu ndani.* (uk. 205-206)

Ushahidi huu unaonesha kwamba ukatili katika *Utelezi* hauhusishwi tu na matumizi ya nguvu za kimwili, bali pia na ujanja, mipango ya siri na matumizi ya mbinu mbalimbali za kumuondoa mwingine. Kiragi na Kimuta wanaonesha aina ya uanaume unaotumia uwezo na nguvu walizonazo kwa madhumuni ya kudhuru wengine. Kwa hivyo, Mbatia anapanua taswira ya ukatili kwa

kuonesha kwamba unaweza kujitokeza kupitia vitendo vya moja kwa moja kama kupiga na kuua, au kupitia mipango ya siri inayolenga kusababisha madhara.

Kwa kuzingatia Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, matukio haya yanaweza kufasiriwa kwa kuzingatia mhimili unaoonesha kuwa matarajio ya kijamii kuhusu uanaume na mazingira anayokulia au kuishi mwanaume yanaweza kuchangia katika kujenga mienendo yake. Wahusika kama kijana mwenye klabu, Okuti, Nyangwe, Kiragi na Kimuta wanatumia nguvu, vitisho, ujanja na mamlaka waliyonayo katika kukabiliana na wengine. Hata hivyo, vitendo hivi havimaanishi kwamba ukatili ni sifa ya asili ya wanaume. Badala yake, riwaya zinaonesha namna mazingira, tamaa, mahusiano, migogoro na mitazamo kuhusu uwezo wa mwanaume vinaweza kuhusishwa na ujenzi wa mienendo ya ukatili.

Kwa mtazamo wa mtafiti, Mbatia anawasawiri baadhi ya vijana wa kiume kama wahusika wanaotumia nguvu na uwezo wao kutawala, kulazimisha, kulipiza kisasi au kujipatia manufaa binafsi. Taswira hii inaonesha upande hasi wa ujenzi wa uanaume ambapo uwezo wa mwanaume haujielekezi katika uwajibikaji au ulinzi wa jamii, bali unageuzwa kuwa chombo cha kumdhuru mwingine. Mtafiti anaona kwamba tofauti muhimu kati ya taswira hii na taswira nyingine za vijana wa kiume katika riwaya hizi ni namna uwezo unavyotumiwa: wakati baadhi ya vijana hutumia uwezo wao kutatua matatizo na kuwasaidia wengine, wahusika wakatili hutumia uwezo huo kuzalisha hofu, madhara na vifo.

Kwa jumla, taswira ya vijana wa kiume wakatili katika riwaya teule inaonesha namna uanaume unavyoweza kujengwa kwa misingi ya matumizi mabaya ya nguvu, mamlaka na uwezo binafsi. Mbatia hata hivyo haoneshi ukatili kama sifa ya vijana wote wa kiume, bali anautofautisha na taswira nyingine chanya kama usomi, bidii, mapenzi ya dhati, upelelezi na uwezo wa kubadilika. Kwa kufanya hivyo, mwandishi anaonesha kuwa namna kijana wa kiume anavyotumia uwezo alio nao ndiyo inayoweza kuamua ikiwa uanaume wake utakuwa wa kujenga au wa kuleta madhara katika jamii.

4.2.7. Vijana wa Kiume kama Watumizi wa Mihadharati

Mihadarati ni kemikali hatari zinazoweza kubadilisha akili na tabia ya mtu, na zinaweza kudhuru afya yake. Vijana wengi huweza kujikuta katika matumizi ya mihadharati. Tatizo hili huweza kuwakumba watu wa jinsia yote. *Njozi Yapata Mtenzi* (2018), inawasawiri baadhi ya vijana wa

kiume kama watumizi wa mihadharati. Rejwa na Mwogi hata walipokuwa katika shule ya upili walianza kushiriki katika matumizi ya mihadharati hata katika maisha yao ya ujana.

> *Pia, haijulikani walijifunzia wapi uvutaji sigara na unywaji pombe, na sasa walikuwa waraibu wakubwa. Kulikuwa na tetesi kwamba hata bangi walivuta. Walifanya mambo haya machafu kwa sababu daima walikuwa na pesa nyingi. (Uk 114)*

Dondoo hili linaonesha kuwa matumizi ya mihadarati kwa Rejwa na Mwogi yamekuwa sehemu ya mwenendo wao wa maisha. Jambo la muhimu hapa ni kwamba wahusika wanaanza matumizi hayo wakiwa bado vijana na wanaendelea nayo hadi wanapokuwa watu wazima. Aidha, uhusiano unaowekwa kati ya kuwa na pesa nyingi na kuendelea na matumizi hayo unaonesha kuwa mazingira ya kifedha yanaweza kumpa kijana uwezo wa kupata na kutumia mihadarati.

Taswira hii inaendelezwa kupitia Njoro na Dan, ambao wanapatikana katika mazingira ambamo matumizi ya kokeni yamekuwa sehemu ya shughuli za vijana. Kiguto anapofanya upelelezi katika kibanda fulani, anawasikia vijana hao wakizungumza kuhusu kujidunga kokeni:

> *"Relax Njoro. Acha kuteta. Una haraka gani? Kwani unaenda kunyonesha?" "Shika Dan umtilie yake. Ni kiu inamsumbua." Kiguto hakuhitaji kusikiliza zaidi. Ilikuwa wazi kwamba shughuli iliyokuwa ikiendelea ni kujitia kokeni kwenye mishipa ya damu kwa kujidunga sindano.* (uk. 26)

Ushahidi huu unaonesha mazingira ya marika ambayo matumizi ya mihadarati yanafanyika kama jambo la kawaida miongoni mwa vijana. Mazungumzo ya Njoro na Dan yanaonesha kuwa mmoja anamwelekeza mwingine katika matumizi ya kokeni, hali inayodhihirisha uwepo wa ushawishi wa rika katika kujenga mwenendo wa vijana. Hivyo, Mbatia haonyeshi mtumiaji wa mihadarati kama mtu anayefanya uamuzi akiwa peke yake, bali anamweka ndani ya mazingira ambayo tabia hiyo inaweza kujifunzwa na kuendelezwa kupitia mahusiano ya vijana.

Katika *Utelezi* (2023), taswira ya vijana wa kiume watumizi wa mihadarati inajitokeza kupitia Raiku na Kage. Baada ya Raiku kufeli mtihani wake wa kitaifa, mamake anamfungulia biashara ya kuuza spea za magari. Hata hivyo, biashara hiyo haifanikiwi kwa sababu Raiku anajihusisha na ulevi na maisha ya anasa. Maelezo ya riwaya yanaonesha:

Kage na Raiku walikuwa wapenda-raha. Hela zote ambazo zilipatikana na biashara yao, walizitumia katika ulevi na anasa nyingine halali na haramu. (uk. 93)

Aidha, matumizi yao ya mihadarati yanaelezwa wazi zaidi katika mazungumzo yafuatayo:

"Hufanyia nini hela zote wapatazo?" Karagi alishangaa. "Mihadarati. Wanatumia unga. Isitoshe, wana mashabiki chungu nzima. Wao ndio matajiri wa kuwagawia marafiki kokeni. Pia hunywa pombe kupindukia na kukamatwa mara kwa mara." (uk. 66)

Dondoo hili linaonesha kuwa matumizi ya mihadarati kwa Raiku na Kage yameambatana na matumizi ya fedha, ulevi na kutafuta hadhi miongoni mwa wenzao. Muhimu zaidi, wao si watumiaji pekee, bali pia huwapatia marafiki zao kokeni. Hivyo, tabia yao inaenea kutoka kwa mtu binafsi hadi katika kundi la vijana wanaoshirikiana nao. Matokeo ya mwenendo huu yanaonekana pale ambapo uraibu wa Raiku unamfanya kuzua rabsha katika klabu, kumpiga meneja na kumng'oa meno, jambo linalosababisha akamatwe na kuhukumiwa kifungo cha miaka mitatu.

Kwa kuzingatia Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, taswira hii inaweza kueleweka kupitia mhimili unaosisitiza kuwa sifa na mienendo ya wanaume hujengwa pia na mazingira na matarajio ya kijamii. Katika matini hizi, matumizi ya mihadarati yanaonekana katika mazingira ya marika, starehe, fedha na mahusiano ya kijamii. Kwa hiyo, baadhi ya vijana wanaweza kuingia katika matumizi ya mihadarati kutokana na mazingira yanayowazunguka na mienendo inayokubalika au kuhalalishwa na kundi lao. Hali hii inaonesha kuwa uanaume unaowasilishwa katika matukio haya unahusishwa na matumizi ya fedha, starehe na kujionesha mbele ya wenzao, badala ya uwajibikaji na kujidhibiti.

Kwa mtazamo wa mtafiti, Mbatia anawasawiri baadhi ya vijana wa kiume watumizi wa mihadarati kama wahusika ambao uanaume wao umeathiriwa na mazingira ya marika, upatikanaji wa fedha, starehe na shinikizo la kijamii. Kinachojitokeza si matumizi ya mihadarati pekee, bali mchakato ambao tabia hiyo hujengeka na kuimarishwa ndani ya mahusiano ya vijana. Rejwa na Mwogi wanaendeleza matumizi yao kwa muda mrefu, Njoro na Dan wanashirikiana katika matumizi ya kokeni, huku Raiku na Kage wakihusisha matumizi ya mihadarati na starehe na kuwashirikisha wenzao. Kwa hivyo, mtafiti anaona kwamba Mbatia anatumia wahusika hawa kuonesha upande

hasi wa ujenzi wa uanaume ambapo kuthibitisha hadhi mbele ya wenzao na kutafuta starehe kunaweza kusababisha vijana kuingia katika mienendo inayohatarisha maisha yao na ya wengine.

Kwa jumla, taswira ya watumizi wa mihadarati inaonesha kuwa baadhi ya vijana wa kiume katika riwaya teule hujengwa katika mazingira yanayoweza kuendeleza tabia hatarishi. Mbatia anahusisha matumizi hayo na marika, fedha, starehe na mahusiano ya kijamii, hivyo kuonesha kwamba mienendo ya vijana haiwezi kueleweka kwa kuzingatia sifa binafsi pekee. Taswira hii pia inaonesha kuwa uanaume unaweza kuchukua mwelekeo hasi pale ambapo matarajio ya hadhi na kujidhihirisha mbele ya wengine yanaunganishwa na matumizi ya mihadarati.

4.2.8. Vijana wa Kiume kama Wezi

Bufacchi (2005) anaeleza mwizi kama mtu anayechukua mali ya mtu mwingine bila idhini yake. Wizi unaweza kuambatana na dhuluma na ukatili. Katika utafiti huu, taswira ya vijana wa kiume wezi inaangaliwa kwa kuzingatia namna wanavyohusishwa na vitendo vya wizi. Inazingatia pia mazingira na mahusiano yanayochangia mwenendo huo.

Katika Njozi Yapata Mtenzi (2018), vijana kama Kim na Dan, wanafunzi wa Shule ya Upili ya Wavulana ya Madaraka, wanaingia katika wizi. Wanaingia kupitia mahusiano yao na Okuti na Nyangwe, wezi sugu. Baada ya masomo, Kim na Dan huenda barabara ya Mkomani, kwenye kioski cha Okuti na Nyangwe. Huko wanatangamana na wezi hao pamoja na mali walizoiba, ikiwemo simu ya Shukri. Walipaswa kuiuza simu hiyo. Kiguto anapoigundua, anawahoji vijana hao kuhusu chanzo chake.

> *Kiguto alichomoa ile rununu ya Shukri kutoka mfukoni akamwelekezea Kim. "Ulitoa wapi hii simu?" Yalimtoka maneno yaliyowaka moto kwa ukali. "Sema haraka! Usitupotezee wakati," moto uliendelea kurindima.*
>
> *"Okuti. Ali-ni-a-chi-chia ni-ni-muuzie," Kim aligugumia. sauti iliyokata kama kisu.*
>
> *"Peleka sisi kwake saa hii!" Majunju alisema kwa sauti iliyokata kama kisu.*
>
> *"Si-si-jui kwa-ke."*
>
> *Kofi kali la shavuni lililorushwa na kono la Majunju lilimfanya Kim ayumbeyumbe kama mlevi. "Utapeleka sisi kwa Okuti?"*

“D-Dan ndi-ndiye a-na-na-ju-jua kwa-ke.”

“Nyote wawili mtatupeleka huko. Sawa?” Kiguto alinguruma.

“Sawa!” Walisema kwa pamoja wale vijana wadogo waliokuwa wakitetemeka kama wagonjwa wa homa.

“Nyinyi nafanyia nani hii kazi?” Majunju alifyatua swali jingine.

Kim na Dan walitupiana jicho la kuulizana, tuseme tusiseme? Akili zao zilienda mbio kama risasi kutokana na hatari iliyowakabili. Hapakuwa uikatasi ya taahira wala uongo. Lakini ukweli pia ulikuwa na hatari zake. Kuwafichua majambazi sugu kilikuwa kitendo cha kuufungulia kifo mlango.

Majunju alikuwa karibu kuinua kono lake tena, jawabu lilipokuja. Alijibu.

“Okuti na Nyangwe. Hiki kioski ni chao.” (uk. 42)

Dondoo hili linaonesha kuwa Kim na Dan wameanza kuhusishwa na wizi kupitia mazingira wanayotangamana nayo. Ingawa wao ni wanafunzi, wanahusishwa na Okuti na Nyangwe ambao tayari wamejikita katika uhalifu. Kim anakiri kwamba simu aliyo nayo alipewa na Okuti ili aiuze. Hivyo, Mbatia anaonesha kuwa tabia ya wizi inaweza kuenea kwa vijana kupitia mahusiano yao na watu wanaojihusisha na uhalifu.

Aidha, hofu inayoonyeshwa na Kim na Dan wanapoulizwa kuhusu Okuti na Nyangwe inaonesha kwamba vijana hao wanatambua uzito wa mazingira waliyomo. Wanaogopa kuwafichua wezi hao kwa sababu wanajua kuwa kufanya hivyo kunaweza kuhatarisha maisha yao. Hali hii inaonesha kwamba vijana wanaoingia katika mazingira ya uhalifu wanaweza kujikuta katika mahusiano yenye vitisho na shinikizo yanayofanya iwe vigumu kujinasua.

Mbatia anaendeleza taswira hii kupitia Okuti na Nyangwe, ambao si wezi pekee bali pia wanawahusisha vijana wadogo katika shughuli zao za uhalifu. Kwa hiyo, matendo yao yanaonesha namna mazingira ya uhalifu yanavyoweza kuwafikia vijana na kuwafanya kuwa sehemu ya mtandao mpana wa wizi. Aidha, wezi hawa wanamwandama Shukri, ambaye ni wa asili ya Kihindi, kwa kuamini kwamba ana utajiri kwa sababu ya asili yake. Hivyo, wizi wao unaambatana pia na mitazamo potofu kuhusu utajiri na asili ya mtu.

Kwa kuzingatia Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, taswira hii inaweza kueleweka kupitia mhimili unaosisitiza kwamba sifa na mienendo ya wanaume hujengwa pia na mazingira, mahusiano na matarajio ya jamii. Katika matini hii, Kim na Dan wanaingia katika mazingira ya wizi kupitia uhusiano wao na Okuti na Nyangwe. Hali hii inaonesha kwamba mazingira ya kijamii yanaweza kuwa na nafasi katika kumjenga kijana na kumwelekeza katika mwenendo fulani. Kwa upande mwingine, Okuti na Nyangwe wanaonesha namna wahusika wenye mamlaka ndani ya mazingira ya uhalifu wanavyoweza kuwavuta vijana wadogo katika shughuli hizo.

Kwa mtazamo wa mtafiti, Mbatia anawasawiri vijana wa kiume wezi kama wahusika ambao mwenendo wao hauwezi kueleweka kwa kuzingatia uamuzi binafsi pekee, bali pia kwa kuzingatia mazingira na mahusiano yanayowazunguka. Kim na Dan ni mfano wa vijana ambao wameanza kuhusishwa na wizi kupitia uhusiano wao na Okuti na Nyangwe. Mtafiti anaona kuwa jambo muhimu katika taswira hii ni mchakato wa kuingizwa kwa vijana katika mazingira ya uhalifu, kwa sababu Okuti na Nyangwe hawawakilishi tu wezi binafsi, bali pia mazingira yanayoweza kuendeleza na kurithisha mienendo ya kihalifu kwa vijana wengine.

Kwa jumla, taswira ya wezi inaonesha upande hasi wa ujenzi wa uanaume ambapo mazingira ya uhalifu, mahusiano na tamaa ya mali vinaweza kumwelekeza kijana katika mwenendo usiokubalika kijamii. Kupitia Kim na Dan, Mbatia anaonesha athari za vijana kuingia katika mahusiano na wahalifu wakubwa, huku Okuti na Nyangwe wakionesha namna mazingira hayo yanavyoweza kuendelezwa na kuwahusisha vijana wengine. Hivyo, taswira hii inasisitiza umuhimu wa mazingira ya kijamii katika kuelewa mienendo ya vijana wa kiume.

4.2.9 Vijana wa Kiume kama Wapenda Raha

Wapenda raha mara nyingi ni watu wanaoonekana kuthamini starehe, anasa na maisha ya kujifurahisha kuliko kuwajibika katika masuala ya kazi, elimu au familia. Mara nyingi hutumia muda na rasilimali nyingi katika burudani, matumizi ya kupindukia na kutafuta sifa mbele ya wenzao. Kwa kuzingatia nadharia ya uwezo mkuu wa kiume, mwenendo huu unaweza kufasiriwa kama jitihada za baadhi ya wanaume kuthibitisha uanaume wao kupitia ishara za hadhi kama vile fedha, mavazi ya gharama, starehe na uwezo wa kuvutia wengine. Hata hivyo, mtazamo huu unaweza kuwafanya wajikute katika changamoto za kiuchumi, kupoteza mwelekeo wa maisha na kushindwa kutekeleza majukumu yanayotarajiwa na jamii

Katika riwaya ya *Utelezi* (2023), Raiku, ambaye ni mdogo wa Tony, anasawiriwa kama kijana anayependa raha. Baada ya kufunguliwa biashara ya kuuza spea za magari na mamake, Raiku anatumia fedha anazopata katika dawa za kulevya na maisha ya anasa. Yeye pamoja na dada yake, Kage, wanafuja fedha zinazotokana na biashara hiyo na kuzitumia katika starehe mbalimbali. Hali hii inaelezwa katika dondoo lifuatalo:

> *Kage na Raiku walikuwa wapenda-raha. Hela zote ambazo zilipatikana na biashara yao, walizitumia katika ulevi na anasa nyingine halali na haramu. Imani mojawapo iliyowafanya kufuja hela bila kujali ilikuwa kwamba mama yao alikuwa na hela nyingi kiasi kwamba hata wazitafune kiasi gani, haziingesha. Imani hiyo iliongezeka maradufu baada ya kifo cha baba yao waliposikia tetesi kwamba mama yao alirithi mamilioni ya pesa na majumba ya kukodisha. Kwa vile walifahamu fika jinsi Shija alivyo msiri, hawakujisumbua kutafuta ukweli kamili kuhusiana na tetesi hizo. Watoto hao walikuwa mfano wa wengine wengi nchini ambao walifuja mali ya wazazi wao kwa kutojua jinsi mali hiyo ilivyochumwa wala thamani yake. Wazazi wengi walikuwa kama Shija. Waliamini kwamba njia moja ya kutunza mali ni kudumisha usiri hata kwa familia zao. Kulikuwa na wazazi wachache sana.* (uk. 93)

Dondoo hili linaonesha kuwa Raiku na Kage hawatumii fedha walizopata kwa ajili ya maendeleo yao, bali wanazielekeza katika ulevi na anasa. Jambo muhimu ni kwamba mtazamo wao kuhusu mali unachangiwa na imani kwamba mama yao ana utajiri mkubwa ambao hauwezi kwisha. Kwa hiyo, wanatumia mali bila kujali thamani yake wala namna ilivyopatikana. Mbatia hivyo anaonesha kuwa mazingira ya kifamilia yanaweza kuchangia katika kujenga mtazamo wa kijana kuhusu matumizi ya mali na wajibu wa kuitunza.

Aidha, matumizi ya starehe kwa Raiku na Kage yanaambatana na matumizi ya mihadarati. Katika sehemu nyingine ya riwaya, Karagi anaeleza kuhusu matumizi yao ya fedha na mihadarati:

> *"Hufanyia nini hela zote wapatazo?" Karagi alishangaa. "Mihadarati. Wanatumia unga. Isitoshe, wana mashabiki chungu nzima. Wao ndio matajiri wa kuwagawia marafiki kokeni. Pia hunywa pombe kupindukia na kukamatwa mara kwa mara."* (uk. 66)

Ushahidi huu unaonesha kuwa starehe kwa Raiku na Kage haishii katika matumizi ya kawaida ya burudani, bali inahusisha ulevi na matumizi ya mihadarati. Zaidi ya hayo, kuwapa marafiki zao

kokeni kunaonesha kwamba mienendo yao inaathiri watu wengine wanaowazunguka. Hivyo, Mbatia anajenga taswira ya vijana ambao maisha ya anasa yanakuwa sehemu ya utambulisho wao wa kijamii na yanawaweka katika mazingira yanayoweza kuendeleza tabia hatarishi.

Kwa kuzingatia Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, taswira ya wapenda raha inaweza kuhusishwa na namna baadhi ya vijana wa kiume wanavyotafuta kuthibitisha hadhi yao kupitia mali, starehe na kujionesha mbele ya wengine. Katika mazingira haya, uwezo wa kutumia fedha na kupata starehe unaweza kuchukuliwa kama ishara ya mafanikio au hadhi. Hata hivyo, Mbatia anaonesha matokeo hasi ya mtazamo huo, kwa kuwa matumizi ya kupindukia ya fedha na mihadarati yanawafanya wahusika kupoteza mwelekeo wa maendeleo na kuwajibika kwa mali waliyopewa.

Kwa mtazamo wa mtafiti, Mbatia anawasawiri vijana wa kiume wapenda raha kama wahusika ambao mtazamo wao kuhusu mafanikio umejengwa zaidi katika matumizi na starehe kuliko uwajibikaji na maendeleo ya muda mrefu. Raiku na Kage wanaona mali kama chanzo cha kujifurahisha, jambo linaloonesha kwamba namna kijana anavyotumia rasilimali alizonazo inaweza kuathiri taswira yake na nafasi yake katika jamii. Mtafiti anaona pia kwamba Mbatia hakusawiri starehe kama jambo la mtu binafsi pekee, bali ameiunganisha na mazingira ya kifamilia, upatikanaji wa fedha na mahusiano ya vijana. Kwa hiyo, tabia ya kupenda raha inajengwa na mwingiliano wa mazingira hayo pamoja na mitazamo ya wahusika kuhusu maisha na mafanikio.

Kwa jumla, taswira ya wapenda raha inaonesha upande hasi wa ujenzi wa uanaume ambapo fedha, starehe na kujionesha vinaweza kupewa nafasi kubwa kuliko uwajibikaji, elimu na maandalizi ya maisha ya baadaye. Kupitia Raiku na Kage, Mbatia anaonesha madhara ya matumizi yasiyowajibika ya mali na namna mazingira ya kifamilia yanavyoweza kuchangia katika kujenga mtazamo huo. Hivyo, riwaya inaonesha kuwa hadhi ya kijana wa kiume haiwezi kupimwa kwa uwezo wake wa kutumia fedha au kujihusisha na starehe, bali inapaswa pia kuhusishwa na namna anavyotumia rasilimali na nafasi alizopewa kwa uwajibikaji.

4.2.10 Vijana wa Kiume kama Wenye Utu

Kulingana na Kimmel (2017), utu unahusisha kujitunza na kuwajali wengine, pamoja na uwezo wa kuhusisha hali ya mwingine na hali yako mwenyewe. Kwa mtazamo huu, utu hauishii katika

upole au ukarimu, bali hudhihirika kupitia matendo ya kujali, kusaidia na kuwajibika kwa wengine. Katika muktadha wa vijana wa kiume, sifa hii ni muhimu kwa sababu inapanua taswira ya uanaume kutoka katika nguvu, mamlaka na ukali hadi katika huruma, uwajibikaji na mshikamano wa kijamii. Janvan (2023) anaeleza kuwa Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume inazingatia pia namna matarajio na mazingira ya kijamii yanavyoweza kumwelekeza mwanaume kufanya maamuzi yanayozingatia maslahi yake na ya wengine. Kwa msingi huo, Mbatia anawasawiri baadhi ya vijana wa kiume kama wahusika wanaoweza kujali matatizo ya wengine na kuchukua hatua za kuyatatua.

Katika riwaya *Njozi Yapata Mtenzi* (2018), Kiguto anasawiriwa kama kijana mwenye utu kutokana na namna anavyowajali watu wanaomzunguka. Mbali na kujijali mwenyewe, anamsaidia mamake wa kambo katika shughuli za nyumbani na dukani. Pia, anafuatilia kesi ya mamake na kutafuta ushahidi unaomwezesha kuachiliwa huru. Baada ya kuachiliwa, Kiguto anamtafutia shule ambayo anaweza kuisimamia na kufundisha kwa mujibu wa uwezo na matakwa yake. Utu wa Kiguto unaonekana pia katika namna anavyomtendea Kibetu baada ya kubadili mwenendo wake. Badala ya kumtenga kwa sababu ya historia yake ya uhalifu, anamfungulia nafasi ya kuanza maisha mapya. Hili linathibitishwa na dondoo lifuatalo:

> *"Kibetu alipotoka hospitalini baada ya kulazwa kwa juma moja, alianza kumsaidia Kiguto katika upelelezi. Ndipo inspekta huyo alipogundua kwamba mtu huwa mwema. Kibetu aliamua kuachana kabisa na uhalifu. Akajaribu kulipia kwa mema yote ambayo Kiguto alikuwa amemtendea kwa kumsaidia katika upelelezi. Kiguto alifurahishwa sana na mabadiliko yake. Akamwajiri kama wakala wake katika usimamizi wa yale majumba ya Ngomeni."* (uk. 277-278)

Dondoo hili linaonesha kuwa utu wa Kiguto hauishii katika kumhurumia mwingine, bali unaambatana na hatua za kumsaidia kujenga upya maisha yake. Kumwajiri Kibetu kunampa fursa ya kujinasua kutoka katika mazingira ya uhalifu na kutumia uwezo wake kwa njia inayokubalika katika jamii. Kwa hiyo, Mbatia anaonesha kwamba kijana wa kiume anaweza kutumia mamlaka, nafasi na uwezo alionao kwa ajili ya kumwezesha mwingine badala ya kumdhibiti au kumtenga. Hapa ndipo mhimili wa nadharia unaohusu mchango wa mazingira na mahusiano ya kijamii unapopata umuhimu, kwa kuwa mabadiliko ya Kibetu yanaonekana kuchochewa pia na namna Kiguto alivyomhusisha na kumpa nafasi ya kujirekebisha.

Taswira ya utu inaonekana pia katika *Utelezi* (2023) kupitia mhusika Maselu. Anapopata habari kwamba Nakanase ameugua, anaonesha huruma kwa kuuliza hali yake na kueleza masikitiko yake. Zaidi ya huruma hiyo, anachukua hatua ya kumsaidia Syokim katika kukamilisha mradi wake ili usikwame kutokana na changamoto inayomkabili. Mazungumzo yao yanaonesha hali hii:

> *"Kuna nini cha mno?"*
>
> *"Nakanase ameugua."*
>
> *"Oo, poleni jamani! Vipi hali yake?" Maselu aliuliza.*
>
> *"Amezaliwa," Syokim alimuarifu.*
>
> *"Lo! Makubwa hayo."*
>
> *"Kweli. Yamenitumbukiza shimoni."*
>
> *"Kuhusiana na mradi wako?" Maselu aliuliza.*
>
> *"Barabara! Wajua nilichukua mkopo wa benki nikitarajia kwamba miezi mitatu kutoka sasa jumba litakuwa limekamilika na kupata wateja ili nitumie hela za kodi kulipa mkopo. Sasa haya yaliotokea yananilazimu kuniletea shida. Hatujui Nakanase atalazwa kwa muda gani. Nataka aje tuongee, nikupe kazi ya kumalizia sehemu iliyobaki ili mradi usikwame," Syokim alifafanua.*
>
> *"Sasa nakuelewa. Usitie shaka. Katika muda wa siku mbili zijazo nitakuwa nimerudi. Pindi nitofika nyumbani nitakupigia simu tupange kukutana," Maselu aliahidi.* (uk. 22)

Ushahidi huu unaonesha utu wa Maselu katika viwango viwili. Kwanza, anaonesha huruma kwa Nakanase anapoulizia hali yake baada ya kupata habari za ugonjwa wake. Pili, anachukua hatua ya kumsaidia Syokim kukamilisha mradi wake ili kukabiliana na tatizo lililotokea. Kwa hiyo, utu wake haujengwi na maneno ya pole pekee, bali na utayari wa kutumia muda na uwezo wake kumsaidia mwingine. Kwa kuzingatia Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, kitendo hiki kinaonesha namna uanaume unavyoweza kujengwa kupitia uwajibikaji na mahusiano ya kijamii badala ya kutegemea nguvu au mamlaka pekee.

Utu wa kijana wa kiume unaonekana vilevile kupitia Kage katika *Utelezi*. Anapompokea baba yake, anaonesha heshima na kujali hali ya familia. Anamfungulia lango, anaulizia hali ya shuleni na nyumbani, na anaendelea kukaa naye kwa mazungumzo baada ya chakula. Mbatia anaeleza:

> *"Karibu, baba! Pole kwa safari."*
>
> *Akaendelea kufungua lango zito la chuma kwa kulivuta upande wa ndani.*
>
> *"Ah, sante. Habari za shuleni na nyumbani?"*
>
> *"Nzuri tu, baba. Kila mtu mzima, wapo. Ni kama tulivyo utafika."*
>
> *Baada ya chakula cha mchana, hatukubanduka sebuleni bali tuliendelea kupiga soga," Kage alieleza haraharaka.* (uk. 31)

Sehemu hii inamjenga Kage kama kijana anayethamini mahusiano ya kifamilia. Matendo yake ya kumpokea baba, kumfungulia lango, kuzungumza naye kwa heshima na kuendelea kushirikiana naye yanaonesha kuwa utu unaweza kujidhihirisha katika matendo madogo ya kila siku. Kwa hiyo, taswira ya uanaume katika riwaya hii haihusishwi tu na uwezo wa kijana kujitegemea au kuwa na mamlaka, bali pia na namna anavyohusiana na watu wa karibu naye. Hali hii inaonesha kuwa malezi na mazingira ya familia yanaweza kuwa na nafasi katika kujenga mienendo ya kijana wa kiume.

Kwa mtazamo wa mtafiti, Mbatia anawasawiri vijana wa kiume wenye utu kama wahusika ambao uanaume wao unadhihirika kupitia kujali, kusaidia, kuheshimu na kuwajibika kwa wengine. Katika *Njozi Yapata Mtenzi*, utu wa Kiguto unaonekana zaidi katika kuwasaidia wahusika wengine kubadilisha maisha yao na kupata fursa mpya, huku katika *Utelezi* ukidhihirika kupitia huruma, mshikamano na mahusiano ya kifamilia. Tofauti hizi zinaonesha kwamba utu haujitokezi kwa namna moja, bali hujengwa kulingana na mahusiano na mazingira yanayomzunguka kijana.

Kwa hivyo, mtafiti anaona kwamba taswira ya vijana wa kiume wenye utu inapanua uelewa wa uanaume katika riwaya teule. Mbatia hapimi uanaume kwa nguvu, ukali au uwezo wa kutawala pekee, bali pia kwa uwezo wa kijana kujali wengine, kuwajibika na kutumia nafasi aliyonayo kwa manufaa ya watu wanaomzunguka. Hivyo, utu unakuwa sehemu ya ujenzi wa uanaume unaotambua mshikamano na uwajibikaji wa kijamii kama vipengele muhimu vya kuwa kijana wa kiume.

4.2.11. Vijana wa Kiume kama Wenye Ndoto na Matarajio Makubwa ya Maisha

Ndoto na matarajio ya maisha ni miongoni mwa mambo yanayompa kijana dira kuhusu mustakabali wake. Kwa vijana wa kiume, matarajio haya yanaweza kujikita katika elimu, taaluma, kujitegemea kiuchumi na kufikia hadhi fulani katika jamii. Connell (1995) anaonesha kuwa uanaume hujengwa katika mazingira ya kijamii ambamo wanaume hupewa matarajio na majukumu fulani kuhusu maisha yao. Kwa msingi huu, ndoto za vijana wa kiume haziwezi kutenganishwa na mazingira wanamoishi, mahusiano yao na matarajio yanayowekwa juu yao. Katika riwaya teule, Mbatia anawasawiri vijana wa kiume kama wahusika wenye maono kuhusu maisha yao ya baadaye na wanaotamani kutumia elimu na juhudi zao kufikia malengo hayo.

Katika *Utelezi* (2023), Tony na binamuye Filipo wanasawiriwa kama vijana wenye matarajio makubwa ya kitaaluma. Ndoto zao zinahusishwa na matumaini mapya yaliyotokana na mabadiliko ya kisiasa na kijamii yaliyokuwa yamejenga imani kwamba maisha yanaweza kubadilika. Wawili hao waliamini kuwa mafanikio katika elimu yangewawezesha kufikia taaluma walizozitamani. Mbatia anaeleza:

> *"Hali hii iliimarisha ndoto za vijana hao wawili. Waliamini kwamba wakijikakamua masomoni na kupasi vizuri katika mtihani wa KCSE (Kenya Certificate of Secondary Education) mwishoni mwa mwaka, watatimiza ndoto za kusomea taaluma walizopenda. Walimu wao walifahamu uteuzi wao wa taaluma za kusomea chuo kikuu na waliwatia moyo kila uchao wasilegee. Walikuwa wanafunzi hodari, na walitarajiwa kufuzu kwa alama za juu."* (uk. 7)

Dondoo hili linaonesha kuwa ndoto za Tony na Filipo zimejengwa katika muunganiko wa matarajio yao binafsi na mazingira yanayowazunguka. Wanaona elimu kama njia ya kufikia taaluma wanazozitamani, huku walimu wao wakiwa chanzo cha motisha katika mchakato huo. Hivyo, matarajio yao hayajitokezi kama mawazo binafsi pekee, bali yanaimarishwa na mazingira ya kielimu na matumaini mapana ya kijamii. Kwa kuzingatia mtazamo wa Messerschmidt (1993) kuhusu uanaume kama jambo linalojengwa na matendo na mazingira ya kijamii, matarajio ya Tony na Filipo yanaweza kueleweka kama sehemu ya mchakato wa kujenga utambulisho wao wa kijana wa kiume katika jamii.

Aidha, katika *Njozi Yapata Mtenzi* (2018), Kiguto anasawiriwa akiwa na maono makubwa kuhusu maisha yake ya baadaye kabla ya kukumbwa na changamoto zilizobadilisha mwelekeo wa maisha yake. Anatarajia kufanya vizuri katika masomo, kuingia katika taaluma yenye hadhi, kupata kipato kizuri na kuishi maisha bora. Mbatia anaeleza:

> *"Zamani, alifikiria jinsi atakavyosoma, afuzu kwa alama za juu iwezekanavyo, aingie katika taaluma mojawapo ya kifahari, apate hela nyingi na kuishi maisha ya kifalme."* (uk. 95)

Dondoo hili linadhihirisha kwamba Kiguto anajenga taswira ya mustakabali wake kupitia elimu, taaluma na mafanikio ya kiuchumi. Ndoto yake inaonesha matarajio ya kijana anayetamani kubadili hali yake ya maisha na kufikia hadhi anayoiiona kuwa bora. Hata hivyo, ndoto hiyo inaonesha pia namna matarajio ya mafanikio ya kijana wa kiume yanavyoweza kuhusishwa na vigezo vya jamii kama taaluma yenye hadhi, kipato kikubwa na maisha ya starehe. Kwa hiyo, matarajio ya Kiguto yanaweza kusomwa kama sehemu ya ujenzi wa uanaume unaomwandaa kijana kutafuta mafanikio na kujitegemea.

Kwa misingi ya Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, mazingira ya kijamii na matarajio yanayohusishwa na uanaume yanaweza kumwelekeza kijana katika namna anavyojenga malengo na kutathmini mafanikio yake. Katika mifano ya Tony, Filipo na Kiguto, elimu na taaluma vinajitokeza kama njia muhimu za kufikia mafanikio. Hata hivyo, Mbatia haonyeshi ndoto hizo kama matokeo ya sifa ya mwanaume pekee; anaziweka ndani ya mazingira ya familia, shule, siasa na matarajio mapana ya jamii. Hivyo, ndoto za vijana hawa zinajengwa katika mwingiliano kati ya matarajio binafsi na mazingira ya kijamii.

Kwa mtazamo wa mtafiti, Mbatia anawasawiri vijana wa kiume wenye ndoto na matarajio makubwa kama wahusika wanaotazama elimu, taaluma na mafanikio ya kiuchumi kama njia za kujenga mustakabali wao. Hata hivyo, uchanganuzi unaonesha kwamba matarajio haya hayaishii katika tamaa binafsi, bali yanaathiriwa na matarajio ya jamii kuhusu kile ambacho kijana wa kiume anapaswa kufikia. Tony na Filipo wanaongozwa na mazingira ya shule na matumaini ya mabadiliko ya kijamii, huku Kiguto akiongozwa na matarajio ya kupata elimu, taaluma na maisha bora.

Kwa hiyo, taswira ya vijana wenye ndoto na matarajio makubwa inaonesha upande mwingine wa uanaume unaojengwa na maono, juhudi, matarajio ya mafanikio na hamu ya kujenga maisha yenye hadhi. Mbatia hivyo anapanua uelewa wa kijana wa kiume kwa kumwasawiri si kama mhusika anayepaswa kuwa mwenye nguvu au mamlaka pekee, bali pia kama mtu anayepanga maisha yake, anaweka malengo na kutafuta njia za kuyafikia.

4.2.12. Vijana wa Kiume kama Wajasiri

Ujasiri ni sifa inayohusishwa na uwezo wa mtu kukabiliana na hatari, changamoto au mazingira magumu bila kuyumba. Katika muktadha wa uanaume, ujasiri unaweza kujitokeza kupitia uwezo wa kufanya maamuzi magumu, kutetea maslahi binafsi au ya wengine na kukabiliana na hali zinazoweza kuhatarisha usalama au hadhi ya mtu. Kimmel (2017) anaeleza kuwa vijana wa kiume hujifunza dhana mbalimbali za uanaume kutokana na mazingira yanayowazunguka, ikiwemo matarajio ya jamii kuhusu namna wanavyopaswa kukabiliana na changamoto. Katika riwaya teule, Mbatia anawasawiri baadhi ya vijana wa kiume kama wahusika wanaothubutu kukabiliana na hali ngumu hata pale ambapo kufanya hivyo kunaweza kuwa na madhara.

Katika *Utelezi* (2023), Karagi, anayefanya kazi kwa Shija, anaonesha ujasiri anapokataa kuendelea kudhulumiwa na shangazi yake. Baada ya kumsaidia Shija katika njama fulani na kutopata malipo aliyotarajia, Karagi anathubutu kudai haki yake licha ya hatari inayoweza kutokana na kufichuliwa kwa siri zao. Mbatia anaeleza:

> *"Shija alipigwa na butwaa. Ujasiri wa Karagi ulikuwa jambo geni. Hakujua kwamba ulitokana na kukataa kwake kulipa deni."* (uk. 167)

Dondoo hili linaonesha mabadiliko katika mahusiano kati ya Karagi na Shija. Karagi hakubali tena kubaki katika nafasi ya mtu anayenyamaza mbele ya dhuluma, bali anathubutu kusimamia kile anachoona kuwa haki yake. Ujasiri wake kwa hiyo unahusishwa na uwezo wa kukataa kunyonywa na kudai haki, badala ya kuogopa mamlaka ya mtu anayemzidi nguvu. Hali hii inaonesha pia kwamba ujasiri unaweza kujengwa kutokana na mazingira ambayo yanamlazimisha kijana kufanya uamuzi wa kujilinda na kutetea maslahi yake.

Vilevile, katika *Njozi Yapata Mtenzi* (2018), Kiguto anaonesha ujasiri kupitia kazi yake ya upelelezi. Ujasiri wake unaonekana hasa anapokabiliana na Onemi katika harakati za kufuatilia

ukweli na kudai urithi wa babake. Hatua hii inamweka katika mazingira hatarishi, lakini Kiguto haachi juhudi zake za kutafuta ukweli na kuhakikisha kuwa haki inapatikana.

Kwa kuhusisha ushahidi huu na Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, ujasiri wa Karagi na Kiguto unaweza kueleweka katika muktadha wa matarajio ya kijamii yanayomwelekeza kijana wa kiume kuonesha uwezo wa kukabiliana na changamoto. Hata hivyo, Mbatia hauwasilishi ujasiri kama nguvu ya kimwili pekee. Kwa Karagi, ujasiri unajidhihirisha katika kudai haki yake, huku kwa Kiguto ukidhihirika katika uthubutu wa kutafuta ukweli na kukabiliana na mazingira hatarishi. Hivyo, ujasiri unachukua maumbo tofauti kulingana na mazingira na changamoto anayokabiliana nazo mhusika.

Kwa mtazamo wa mtafiti, Mbatia anawasawiri vijana wa kiume wenye ujasiri kama wahusika wanaoweza kusimama dhidi ya mazingira yanayowadhoofisha, kufanya maamuzi magumu na kukabiliana na hatari katika kutetea maslahi yao au kufikia malengo yao. Ujasiri wa Karagi unatokana na kukataa kuendelea kudhulumiwa, wakati Kiguto anautumia katika kutafuta ukweli na haki. Kwa hiyo, tofauti na taswira ya ujasiri inayoweza kuhusishwa na ukali au matumizi ya nguvu, riwaya hizi zinaonesha kwamba kijana wa kiume anaweza kuwa jasiri pia kupitia msimamo, uthubutu na uwezo wa kukabiliana na hali ngumu kwa malengo maalumu.

Kwa msingi huo, taswira ya vijana wenye ujasiri inaonesha namna Mbatia anavyopanua dhana ya uanaume katika riwaya teule. Uanaume haujengwi kupitia uwezo wa kutumia nguvu pekee, bali pia kupitia uwezo wa kusimamia maamuzi, kutetea haki na kukabiliana na mazingira hatarishi. Hivyo, ujasiri wa vijana hawa unaeleweka kama matokeo ya mwingiliano kati ya sifa zao binafsi, mazingira wanamoishi na matarajio ya jamii kuhusu namna kijana wa kiume anavyopaswa kukabiliana na changamoto.

4.2.13. Vijana wa Kiume kama Wenye Kustahimili Changamoto za Kifamilia

Ustahimilivu ni uwezo wa mtu kuendelea kujitahidi na kusonga mbele licha ya kukumbwa na misukosuko au matatizo magumu ya maisha. Katika muktadha wa vijana wa kiume, ustahimilivu unaweza kujitokeza kupitia uwezo wa kukabiliana na misukosuko ya kifamilia bila kuacha malengo yao ya maisha. Katika riwaya teule, Mbatia anawasawiri baadhi ya vijana wa kiume kama wahusika wanaokabiliana na matatizo ya kifamilia kwa kuyageuza kuwa msukumo wa kuendelea mbele badala ya kukata tamaa.

Katika *Njozi Yapata Mtenzi* (2018), Kiguto anaonesha ustahimilivu mkubwa baada ya mamake kuhukumiwa kifungo cha maisha kwa kosa ambalo hakulitenda. Tukio hilo linabadilisha maisha yake na kumweka katika mazingira ya huzuni na changamoto. Hata hivyo, Kiguto haachi masomo yake wala kukubali hali hiyo imzuie kutafuta haki ya mamake. Badala yake, anaweka lengo la kumkomboa na anaendelea kujibidiisha katika masomo akiamini kuwa elimu itamwezesha kufikia azma hiyo. Mbatia anaeleza:

> *"Aliamini kwamba kwa njia moja au nyingine, atapata uwezo wa kumtoa mamake gerezani na kufuta dhuluma iliyomharibia maisha yake. Hivyo ndivyo maisha yake yalivyochukua mkondo tofauti. [...] Lakini sasa lengo lake maishani lilikuwa moja tu, kumwokoa mamake kutokana na balaa iliyomwangukia. Aliendelea kujitahidi masomoni akiamini kwamba masomo yatampa uwezo atakaohitaji kumsaidia mamake."* (uk. 95)

Dondoo hili linaonesha kwamba msukosuko wa kifamilia haukumfanya Kiguto akate tamaa. Kinyume chake, alitumia hali hiyo kama kichocheo cha kujenga lengo jipya la maisha. Kuendelea kwake na masomo licha ya maumivu ya kifamilia kunadhihirisha uwezo wa kuvumilia hali ngumu na kuendelea kutafuta suluhisho. Kwa hiyo, Mbatia anajenga taswira ya kijana wa kiume ambaye anapokumbwa na tatizo kubwa la kifamilia, hulikabili kwa kuweka malengo na kuchukua hatua zinazoweza kumwezesha kulitatua.

Ustahimilivu wa aina hii unaonekana pia katika *Utelezi* (2023) kupitia Tony. Baada ya kumpoteza babake wiki chache kabla ya mtihani wa kitaifa, Tony anapatwa na msukosuko mkubwa unaoathiri mwenendo wake wa masomo na hatimaye anafeli mtihani. Pamoja na kushindwa huko, hakukata tamaa kuhusu safari yake ya kielimu. Anaamua kurudia kidato cha nne ili kupata nafasi nyingine ya kufikia malengo yake. Hatua hiyo inaonesha kuwa kufeli kulikosababishwa au kuchangiwa na msiba wa kifamilia hakumfanyi Tony kuacha kabisa matarajio yake. Badala yake, anatumia nafasi ya pili kuendelea na safari yake ya elimu.

Ustahimilivu wa Kiguto na Tony unaeleweka katika muktadha wa Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume kwa kuzingatia namna mazingira na matarajio ya kijamii yanavyoshiriki katika ujenzi wa mienendo ya vijana wa kiume. Kwa Kiguto, matarajio yake ya kumsaidia mamake yanampa msukumo wa kuendelea na masomo, ilhali kwa Tony, kushindwa katika mtihani hakumalizi matarajio yake ya kielimu. Hivyo, katika mifano hii, uanaume hauwasilishwi kama kutokumbwa

na matatizo, bali kama uwezo wa kukabiliana na matatizo na kuendelea kutafuta njia ya kufikia malengo.

Kwa mtazamo wa mtafiti, Mbatia anawasawiri vijana wa kiume wanaostahimili changamoto za kifamilia kama wahusika wanaoweza kubadili misukosuko ya kifamilia kuwa msukumo wa kuendelea na maisha na kutafuta suluhisho. Kiguto anageuza kifungo cha mamake kuwa kichocheo cha kujitahidi katika masomo na kutafuta haki yake, huku Tony akitumia nafasi ya kurudia masomo baada ya kufeli kama njia ya kuendeleza matarajio yake ya kielimu. Mifano hii inaonesha kwamba ustahimilivu wao haujengwi na nguvu binafsi pekee, bali pia na malengo, mahusiano ya kifamilia na matarajio waliyojiwekea kuhusu maisha yao ya baadaye.

Kwa hivyo, taswira ya vijana wanaostahimili changamoto za kifamilia inaonesha upande wa uanaume unaohusishwa na uvumilivu, kujituma, kuwajibika kwa familia na uwezo wa kuendelea mbele licha ya misukosuko. Mbatia hivyo anapanua taswira ya vijana wa kiume kwa kuwaonesha kama wahusika wanaoweza kukumbwa na maumivu na kupoteza, lakini bado wakatumia uzoefu huo kujenga azma mpya na kutafuta mustakabali bora.

4.2.14. Vijana wa Kiume kama Wenye Vipawa vya Michezo

Vipawa vya michezo ni miongoni mwa sifa zinazowasawiri baadhi ya vijana wa kiume katika riwaya teule. Michezo huwapa vijana fursa ya kuonesha uwezo, kujenga nidhamu, kujiamini na kukabiliana na ushindani. Kimmel (2017) anaonesha kuwa mazingira ya kijamii huwafundisha vijana wa kiume dhana mbalimbali kuhusu uanaume, zikiwemo sifa zinazohusishwa na ushindani na uwezo wa kujitahidi kufikia mafanikio. Katika riwaya teule, Mbatia anatumia michezo kuonesha kwamba vipaji na uwezo wa vijana wa kiume vinaweza kuwa sehemu ya ujenzi wa utambulisho wao.

Katika *Utelezi* (2023), Tony na binamuye Filipo wanasawiriwa kama vijana wenye kipawa cha kuendesha baiskeli za michezo. Vipaji vyao vinapata nafasi ya kuendelezwa kupitia klabu ya Nakuru Riders inayomilikiwa na Alibhai. Alibhai anawawezesha vijana kupata vifaa na mafunzo kwa kuwanunulia baiskeli na kuajiri kocha. Aidha, anaandaa mashindano yanayowapa vijana nafasi ya kuonesha uwezo wao. Mbatia anaeleza:

> *"Alibhai ndiye aliyemiliki klabu ya Nakuru Riders. Aliwanunulia vijana baiskeli na kuajiri kocha wa kuwafunza stadi za kuendesha baiskeli za michezo. Kisha aliandaa mashindano yaliyowashirikisha waendeshaji hamsini."* (uk. 3)

Dondoo hili linaonesha kuwa kipawa cha Tony na Filipo hakijengwi na uwezo wao binafsi pekee, bali kinaendelezwa na mazingira yanayowapa fursa ya kukitumia na kukikuza. Uwekezaji wa Alibhai katika vifaa, mafunzo na mashindano unawawezesha vijana hao kuonesha vipaji vyao. Hivyo, Mbatia anaonesha umuhimu wa mazingira ya kijamii katika kuibua na kuendeleza uwezo wa vijana wa kiume.

Pamoja na kushiriki katika mashindano, Tony na Filipo wanaonesha moyo wa ushindani na azma ya kuendelea kujiboresha hata baada ya kutopata ushindi katika mashindano yao ya kwanza. Mbatia anaeleza:

> *"Japo Tony na Filipo walijikakamua mpaka wakamaliza mizunguko yote kumi na miwili, hawakupata ushindi. [...] Asiyekubali kushindwa si mshindani - Tony na binamuye walijituliza wakiwa na matumaini ya kufanya vyema zaidi fursa nyingine ya mashindano itakapotokea."* (uk. 3)

Ushahidi huu unaonesha kuwa kipawa cha michezo kinaambatana na uvumilivu na uwezo wa kukabiliana na kushindwa. Tony na Filipo hawaruhusu kutopata ushindi katika mashindano ya kwanza kuwakatishe tamaa. Badala yake, wanaendelea kuwa na matumaini ya kupata matokeo bora katika mashindano yajayo. Kwa hiyo, Mbatia anawajenga kama vijana wenye mtazamo wa maendeleo ambao hutumia kushindwa kama fursa ya kujifunza na kujiandaa kwa mafanikio yajayo.

Kwa kuzingatia Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, michezo inaweza kuchukuliwa kama mojawapo ya mazingira ambamo matarajio kuhusu uanaume hujitokeza kupitia ushindani, uthubutu na uvumilivu. Hata hivyo, katika mfano wa Tony na Filipo, ushindani hauwasilishwi kama matumizi ya nguvu au kutawala wengine. Badala yake, unajidhihirisha kupitia kujituma, kukubali matokeo na kuwa na azma ya kuendelea kujiboresha. Hivyo, Mbatia anatoa taswira ya uanaume inayohusisha uwezo wa kijana kushindana kwa njia inayomjenga na kumwezesha kukuza kipawa chake.

Kwa mtazamo wa mtafiti, Mbatia anawasawiri vijana wa kiume wenye vipawa vya michezo kama wahusika ambao uwezo wao hujengwa na muunganiko wa kipawa binafsi, mazingira wezeshi, mafunzo na utayari wa kukabiliana na ushindani. Tony na Filipo hawasawiriwi kama wenye kipawa kwa ajili ya kujionesha pekee, bali wanapewa mazingira ya kukiendeleza kupitia mafunzo na mashindano. Kutopata ushindi katika mashindano ya kwanza pia kunawapa nafasi ya kuonesha uvumilivu na azma ya kufanya vizuri zaidi.

Kwa hiyo, taswira ya vijana wenye vipawa vya michezo inaonesha kwamba Mbatia anahusisha uanaume pia na uwezo, ushindani wa kujenga, nidhamu, uvumilivu na kujitahidi kukuza kipaji. Muhimu zaidi, riwaya inaonesha kuwa vipawa vya vijana haviwezi kustawi bila mazingira yanayowawezesha kuvitumia. Hivyo, ujenzi wa taswira hii unadhihirisha mwingiliano kati ya uwezo binafsi wa vijana na mazingira ya kijamii yanayowazunguka.

4.2.15. Vijana wa Kiume kama Wenye Ufahamu wa Kisiasa na Kijamii

Vijana wa kiume katika riwaya teule pia wamesawiriwa kama wenye ufahamu wa masuala ya kisiasa na kijamii yanayoendelea katika jamii zao. Ufahamu huu unajitokeza kupitia uwezo wao wa kufuatilia matukio yanayoathiri jamii na kuelewa maana na athari zake hata kabla ya kuwa na nafasi rasmi ya kushiriki katika maamuzi. Kimmel (2017) anaeleza kuwa mazingira ya kijamii yana mchango katika kuwajengea vijana wa kiume mitazamo kuhusu wajibu wao wa sasa na wa baadaye katika jamii. Katika riwaya teule, Mbatia anaonesha ufahamu huu kupitia Tony, ambaye anafuatilia kwa karibu matukio ya kisiasa nchini akiwa bado hajafikisha umri wa kupiga kura.

Katika *Utelezi* (2023), Tony anaoneshwa akiwa na ufahamu kuhusu matukio ya kisiasa yaliyokuwa yakitokea nchini. Ingawa hakuwa na haki ya kushiriki rasmi katika uchaguzi, alikuwa akifuatilia matukio hayo na kuelewa matumaini yaliyohusishwa nayo. Mbatia anaeleza:

> *"Tony alivutiwa na matukio ya kisiasa ambayo yalitetemesha nchi wakati huo, pamoja na matumaini yaliyohusiana nayo. Hata hivyo, aliyashuhudia akiwa kando mithili ya mpita njia. Hii ni kwa sababu hakuweza kushiriki. Hakuwa mpiga kura kwa sababu hakuwa ametimiza umri wa kupata kitambulisho cha kitaifa."* (uk. 1)

Dondoo hili linaonesha tofauti kati ya kuwa na uwezo wa kufikiri na kuelewa masuala ya kisiasa na kuwa na haki rasmi ya kushiriki katika mchakato wa kisiasa. Tony hana umri unaomwezesha kupiga kura, lakini hali hiyo haimzuii kufuatilia na kuvutiwa na matukio yanayoendelea nchini.

Kwa hiyo, Mbatia anamjenga kama kijana anayefahamu mazingira yake ya kisiasa na kijamii na anayeanza kujenga mtazamo wake kuhusu mustakabali wa jamii yake.

Kwa kuhusisha ushahidi huu na Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, ufahamu wa Tony unaweza kueleweka katika muktadha wa mazingira yanayomzunguka na matarajio ya kijamii kuhusu nafasi ya kijana wa kiume katika jamii. Hata hivyo, ni muhimu kutomchukulia ufahamu wa kisiasa kama sifa ya kimaumbile ya wanaume. Badala yake, riwaya inaonesha kwamba ufahamu huo hujengwa kupitia uzoefu, mazingira ya kijamii na matukio ya kihistoria anayoshuhudia kijana. Kwa Tony, mazingira ya kisiasa ya wakati huo yanakuwa sehemu ya uzoefu unaomsaidia kuelewa jamii yake kabla ya kupata haki rasmi ya kushiriki katika uchaguzi.

Aidha, Luyt (2017) anaonesha kuwa fasihi inaweza kushiriki katika kujenga na kuimarisha mitazamo kuhusu uanaume kupitia namna wahusika wa kiume wanavyosawiriwa. Kwa mtazamo huu, usawiri wa Tony kama kijana anayefuatilia masuala ya kisiasa unaonesha kuwa Mbatia amempa mhusika nafasi ya kuwa na mchango wa kifikra katika jamii hata kabla ya kufikia umri wa kushiriki rasmi katika maamuzi ya kisiasa. Hivyo, ufahamu wa kisiasa na kijamii unakuwa sehemu ya utambulisho wa Tony na unaonesha uwezo wa vijana wa kiume kushiriki katika maisha ya jamii kupitia fikra na uelewa wao.

Kwa ujumla, uchanganuzi wa sifa mbalimbali za vijana wa kiume katika riwaya teule umeonesha kuwa Mbatia anawajenga kwa namna mbalimbali kulingana na mazingira, mahusiano na uzoefu wao. Ujenzi huu hauwezi kueleweka kwa kuzingatia sifa binafsi pekee, kwa sababu mazingira ya kijamii, matarajio ya jamii, vipindi vya kihistoria na mahusiano wanayoshiriki pia yana nafasi katika kujenga mienendo yao. Hili linaendana na msingi wa Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume kwamba namna uanaume unavyojitokeza huhusishwa na mazingira na matarajio ya kijamii yanayomzunguka mwanaume.

Kwa mfano, Tony na Filipo wanaishi katika kipindi ambacho matumaini ya mabadiliko ya kisiasa yanaathiri matarajio yao kuhusu elimu na maisha ya baadaye. Kwa upande mwingine, wahusika wengine wanajengwa kutokana na mazingira ya kifamilia, kielimu na kiuchumi wanamoishi. Hivyo, tofauti za mazingira na vipindi vya kihistoria zinaweza kuathiri namna vijana wa kiume wanavyofikiri, kufanya maamuzi na kujenga matarajio yao. Aidha, mazingira ya kazi na nafasi wanazopata katika jamii yanaweza kuwajengea vijana uwajibikaji, bidii na uwezo wa kushirikiana au kuwaweka katika mazingira ya shinikizo na changamoto.

Kwa mtazamo wa mtafiti, Mbatia anawasawiri vijana wa kiume wenye ufahamu wa kisiasa na kijamii kama wahusika wanaoweza kutambua, kufuatilia na kutafakari masuala yanayoathiri jamii zao hata kabla ya kupata mamlaka rasmi ya kushiriki katika maamuzi. Usawiri wa Tony unaonesha kwamba vijana hawapaswi kuchukuliwa kama watazamaji tu wa matukio ya kijamii na kisiasa. Wanaweza kuwa na uelewa, mitazamo na matarajio kuhusu jamii yao kabla ya kufikia nafasi rasmi za uamuzi.

Kwa hiyo, taswira hii inapanua uelewa wa uanaume katika riwaya teule kwa kuonesha kwamba uwezo wa kijana wa kiume haujengwi kupitia nguvu, ushindani au uthubutu pekee, bali pia kupitia ufahamu, uwezo wa kutafakari na utayari wa kuelewa masuala yanayoendelea katika jamii. Hivyo, kwa mujibu wa mtafiti, ufahamu wa kisiasa na kijamii wa vijana hawa ni zao la mwingiliano kati ya uwezo wao wa kibinafsi na mazingira ya kihistoria, kijamii na kisiasa yanayowazunguka.

4.3. Changamoto Zinazowakumba Vijana wa Kiume Katika Riwaya Teule.

Vijana wa kiume hukumbwa na changamoto mbalimbali katika mazingira ya kijamii, kiuchumi na kisaikolojia, ambazo huathiri mwelekeo wao wa maisha. Mabadiliko ya kijamii yamechangia kupungua kwa nafasi zao za kijadi kama watoa maamuzi au walezi wa familia, hali inayopelekea mkanganyiko wa majukumu na utambulisho. Mwangi (2021) anasema kuwa Ukosefu wa fursa na miundo thabiti ya malezi kumezidisha mkanganyiko wa utambulisho miongoni mwa vijana wa kiume na kuwasukuma kuishi kwa maamuzi ya muda mfupi. Kwa mujibu wa Connell (2005), mifumo ya uwezo mkuu wa kiume huendeleza dhana zinazowazuia wanaume kuonesha udhaifu, kutafuta msaada wa kihisia au kukabiliana na changamoto kwa njia zenye afya. Hali hii huongeza mzigo wa kisaikolojia na kijamii kwa vijana wa kiume na kuathiri ustawi wao kwa ujumla.

Ni wazi kuwa Vijana wa kiume hukumbwa na changamoto zinazoweza kuhusiana na maisha ya kisasa. Ukosefu wa ajira na vyanzo thabiti vya kipato huwakatisha tamaa na kuathiri maendeleo yao. Wengi hupata ugumu wa kuelewa au kuelekeza maisha yao kwa sababu ya ukosefu wa msaada wa kihisia. Shinikizo la kufanikisha maisha mapema huwafanya wajihisi kushindwa. Baadhi yao hujikuta wakijihusisha na uraibu au vitendo visivyofaa wakitafuta faraja ya muda. Hali hii huathiri ustawi wao wa kisaikolojia na kiutu kwa ujumla. Mwandishi Mwenda Mbatia amewatumia wahusika wa vijana wa kiume kuweza kuweka wazi baadhi ya changamoto hizo.

Connell (1987) anasema kuwa katika kudhihirisha sifa za jinsia ya kiume, changamoto nyingi huweza kujitokeza ambazo huletwa au huchangiwa na jamii yake. Ni wazi kuwa kila mwanajamii huweza kukumbwa na changamoto. Hata hivyo, vijana wa kiume huweza kukumbwa na matatizo chungu nzima ambazo husababishwa na mambo mbalimbali. Mhimili huu umeufaa utafiti huu kwani umesaidia katika kuzidondoa changamoto hizo kutoka kwenye riwaya teule za Mwenda Mbatia. Changamoto hizo ni pamoja na;

4.3.1. Changamoto za Vifo

Kifo ni hali ya kiumbe chenye uhai kupoteza uhai uhai na hivyo kuwa mwisho wa maisha. Ni tukio lisiloweza kuepukika na hivyo huenda ikawa na madhara hasa ya kisaikologia kwa watu waliokaribu na yule aliyefariki. Kupoteza mtu wa karibu kama vile mzazi huweza kumuathiri sana mtoto kisaikolojia. Hii ni kwa sababu wazazi huwa na mchango muhimu sana katika maisha ya watoto wao.

Kiguto katika riwaya *Njozi Yapata Mtenzi* (2018), anathirika na kifo cha babake mzazi. Babake anaaga akiwa Siera Leone shughuli zake za kikazi. Baba mtu alikuwa nguzo kuu katika maisha yake. Sasa alilazimika kujitahidi awezavyo katika kuilinda familia yao akiwa angali kijana. Hali hii pia iliweza kumfanya kuanza kikiria na baadaye kuchukua mkondo mpya wa maisha yake.

> *Aliyeathirika zaidi ni Kiguto. Alimpoteza- maga baba na nguzo kuu ya maisha yake. Sasa alibaki akitapatapa kama kuku aliyedenguliwa. Baada ya mazishi ambayo karibu yageuzwe kuwa burudani na mbwembwe za kijeshi, aliwaza na kuwazua juu ya mustakabali wa maisha yake. Alihisi kwamba alihitaji kufuata mkondo mpya. (Uk 215-216)*

Aidha katika *Utelezi* (2023), Tony anapigwa na changamoto kubwa maishani anapompoteza babake wiki chache kabla ya kufanya mtihani wake wa kitaifa. Jambo hili lilimuathiri vikubwa na kusababisha kufeli kwa mtihani wake wa kitaifa. Aidha, Tony alikuwa akitazamia sana kufuata nyayo za babake ya kuwa mhandisi ujenzi, hivyo alikuwa amepoteza nguzo kuu katika maisha (yake ukurasa 54)

> *Naamini kabisa kwamba alama ya C uliyoambulia katika mtihani wa KCSE mwaka jana siyo uliyoitarajia. Kamwe siyo uliyostahili. Ulimwengu mima unafahamu kwamba stahiki yako ni tuzo ya A. Kila mtu anafahamu kwamba dharuba ya kumpoteza babako ndiyo*

iliyokupokonya tuzo yako. Najua kwamba bado una ndoto ya kufuata nyayo za marehemu mdogo wangu. Lakini sasa alama uliyopata haiwezi kukufungulia mlango wa kusomea taaluma ya uhandisi ujenzi.

Kwa upande wa uanaume, kifo cha mzazi wa kiume kinakuwa na uzito zaidi kwa sababu kinabadilisha pia nafasi na majukumu anayotarajiwa kuyatekeleza kijana katika familia. Kiguto anapopoteza babake, anaanza kutafakari mustakabali wake na wajibu wa kuilinda familia, ilhali Tony anapompoteza babake hupoteza pia kielelezo cha kitaaluma alichokuwa akikifuata. Kwa hiyo, changamoto ya kifo katika riwaya hizi haijitokezi kama huzuni ya kawaida pekee, bali inahusiana na kuvurugika kwa matarajio na majukumu yaliyokuwa yamefungamanishwa na uanaume wao.

Kwa kuzingatia Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, changamoto ya vifo inaeleweka kupitia mihimili ya pili na ya tatu, inayosisitiza uhusiano kati ya mazingira ya jamii na changamoto za vijana wa kiume. Ushahidi wa riwaya unaonesha kuwa changamoto hii haiwezi kutenganishwa na mazingira na mahusiano yanayomzunguka kijana. Kwa mtazamo wa mtafiti, hoja muhimu hapa ni kwamba matarajio ya jamii na mazingira ya kijamii yanaweza kuongeza uzito wa changamoto anayopitia kijana wa kiume, badala ya changamoto hiyo kuwa suala la mtu binafsi pekee.

4.3.2. Changamoto za Ukosefu wa Ajira

Ukosefu wa ajira kwa vijana ni changamoto kubwa. Unaathiri maisha yao na maendeleo ya taifa kwa jumla. Vijana wengi wanaomaliza shule wanakosa kazi kutokana na ukosefu wa nafasi. Wanakosa pia kwa sababu ya ujuzi usioendana na soko au upendeleo katika ajira. Hali hii husababisha wengine kukata tamaa. Wengine hujiingiza katika uhalifu na uraibu wa dawa za kulevya. Kinyua (2024) anajadili kuwa ukosefu wa ajira si tatizo la mtu mmoja. Ni bomu linalosubiri kulipuka lisipotatuliwa haraka. Kuna haja ya mipango madhubuti ya kuwapa vijana ujuzi na mitaji. Hii itawawezesha kujiajiri na kuchangia uchumi wa nchi. Tatizo hili linawakumba vijana wa jinsia zote. Hata hivyo, linawaathiri zaidi vijana wa kiume, hasa wanaopanga kuingia ndoa.

Mwenda Mbatia amemulika changamoto hii katika riwaya zake. Ameainisha baadhi ya viini vya ukosefu wa ajira. Fasihi ni kioo cha jamii, hivyo haijaandikwa kwa ombwe tupu. Mwandishi amewatumia wahusika vijana wa kiume kujadili changamoto hii.

Tony anakosa ajira hata baada ya kufuzu chuo kikuu. Anajaribu awezavyo, lakini inamgumu kupata kazi. Janga hili halimuathiri yeye pekee, bali pia vijana wenzake. Wengi wa waajiri walitaka hongo. Tony aliathirika sana, kwani alihitaji kazi ili kujikimu yeye, Doris, na mwana wao waliyemtarajia. Ami yake anajaribu kumtafutia kazi, lakini juhudi zake hazizai matunda (Ukurasa 157–158).

> *Tony Maselu alitafuta kazi bila mafanikio kwa karibu mwaka mzima. Sio kwamba hakuwa na watu wa kumsaidia. Walikuwepo na walifanya juu chini kumtafutia kazi. Aliandika barua za maombi zaidi ya ishirini katika idara za serikali, makampuni na mashirika mbalimbali.*

Hata ingawa walijaribu wawezavyo ilikupata kupata ilikuwa vigumu sana. Tony aliamini kuwa chanzo cha ukosefu wa ajira huwenda ikawa uchumi dhaifu.

Kwa kuzingatia Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, changamoto ukosefu wa ajira inaeleweka kupitia mihimili ya pili na ya nne, inayohusisha matarajio ya kijamii na mgawanyo wa majukumu na fursa. Ushahidi wa riwaya unaonesha kuwa changamoto hii haiwezi kutenganishwa na mazingira na mahusiano yanayomzunguka kijana. Kwa mtazamo wa mtafiti, hoja muhimu hapa ni kwamba matarajio ya jamii na mazingira ya kijamii yanaweza kuongeza uzito wa changamoto anayopitia kijana wa kiume, badala ya changamoto hiyo kuwa suala la mtu binafsi pekee.

4.3.3. Changamoto za Ufisadi

Ufisadi ni tatizo kubwa linalozuia maendeleo na kuharibu maisha ya watu wengi. Unapotokea, huduma muhimu kama afya, elimu na miundombinu hubadilika kuwa duni kwa sababu pesa zinazopaswa kuwasaidia wananchi huibwa. Ufisadi huweza kuendelezwa katika sekta mbalimbali hasa za kiajira. Hali hii husababisha ukosefu wa usawa na kuongezeka kwa umaskini. Kulingana na Connell (2005), Ufisadi sio tu wizi wa mali ya umma, bali ni ukosefu wa maadili unaokandamiza haki na kuharibu imani ya wananchi kwa taasisi za serikali. Maoni yake yanaonesha kuwa mapambano dhidi ya ufisadi yanahitaji viongozi waaminifu, sheria kali, na wananchi wanaojitokeza kulinda haki zao kwa uwazi na ujasiri.

Ufisadi ulikithiri sana katika riwaya ya *Njozi Yapata Mtenzi* (2018) hasa miongoni mwa polisi. Jambo hili linapelekea maove mengi kukithiri katika eneo la Ikindu. Hali hii ya ufisadi iliweza

kuendelezwa pia na wahusika mbalimbali. Baba ya kina Rejwa na Mwogi alitoa hongo ili waeze kupata nafasi katika shule bora. Hali hii inawakosesha wengine ambao walistahili nafasi hio (ukurasa 98).

> *Mwishowe, aliwapeleka shule ya umma ambapo mpwa wake - Kiguto alisomea baada ya kumnunulia soda mkuu wa shule ili abuni nafasi ya wavulana wawili ambao walifeli.*

Watoto hawa wanaposhindwa kujitegemea, baba yao anaamua tena kujihusiha kwa kupitia mlango wa nyuma ili wajiunge na chuo cha mafunzo ya polisi (ukurasa 281).

Riwaya ya *Utelezi* (2023) imeweza kuashiria ufisadi kama changamoto mojawapo inayowakumba wanajamii hasa vijana wa kiume. Baada ya Tony kupanda teksi baada ya mtihani wa mwisho wa chuo kikuu, anapata nafasi ya kuzungumza na dereva. Mazungumzo yao ndio yanaweza kuashiria jinsi ufisadi ulivyosheni (ukurasa 111 – 112);

> *Uk. 111 "Sasa acha nikwambie maneno, kijana ujuage. Si unatamani ajira? Basi ujue zinauzangwa kama mikate na wakubwa serikalini. Wale wanajuanga kukula matunda ya uhuru. Kama huna mtu wa kukushika mkono, uwe na pesa za kununulia ajira. Nchi hii ilioza kitambo.*
>
> *Uk. 112 Ulikuwa ukweli wa kutisha kwamba kazi katika sekta ya umma zilikuwa zinauzwa. Je, wasiokuwa na hela walikuwa na mustakabali gani katika hali kama hiyo? Lilizuka akilini mwake swali la balagha.*

Hii ni ithibati tosha kwamba nchi hio ilifurikwa na ufisadi. Wengi wa vijana walikosa kazi kwa sababu walikosa hela ya “kununua kazi” kama alivyoeleza daktari.

Kwa kuzingatia Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, changamoto ya ufisadi inaeleweka kupitia mihimili ya pili na ya tatu, inayosisitiza uhusiano kati ya mazingira ya jamii na changamoto za vijana wa kiume. Ushahidi wa riwaya unaonesha kuwa changamoto hii haiwezi kutenganishwa na mazingira na mahusiano yanayomzunguka kijana. Kwa mtazamo wa mtafiti, hoja muhimu hapa ni kwamba matarajio ya jamii na mazingira ya kijamii yanaweza kuongeza uzito wa changamoto anayopitia kijana wa kiume, badala ya changamoto hiyo kuwa suala la mtu binafsi pekee.

4.3.4. Changamoto za Unyanyasaji

Unyanyasaji ni tabia ya kumtendea mtu vibaya kwa maneno, vitendo au hata kimya kimya, jambo ambalo huumiza moyo na mwili. Daktari wa saikolojia, Chesaina (2020), anasema kwamba athari za unyanyasaji kwa akili ya mtu ni kubwa sana na huweza kudumu kwa muda mrefu kuliko maumivu ya kawaida ya mwili. Kuelimisha jamii kuhusu madhara ya unyanyasaji ni hatua muhimu ya kuzuia tatizo hili. Wakati mwingine jamii huweza kuendeleza nyanyasaji hasa wa kijinsia bila kujua. Unyanyasi huo huenda ukawa na athari hasa kwa mwathiriwa.

Baadhi ya polisi kama vile Kiguto katika riwaya ya *Njozi Yapata Mtenzi* (2023) wananyanyaswa katika sehemu ya mishahara hata ingawa wao ndio alifanya kazi nyingi. Jambo hili liliwafanya wengi wao kushirikiana na wahalifu ili kupata zaidi. Makazi waliyotengewa yalikuwa chwara (ukurasa 27). Kiguto aliamini kuwa pesa zote zilikuwa za wazee wa ngazi ya juu huku hao wakipata mishahara duni.

Unyanyasaji unaendelezwa katika Riwaya ya *Utelezi* hasaa kwa vijana hawa wa kiume. Unaendelezwa sana na waajiri hasa wanapowalipa vijana hawa mishahara duni. Katika shule aliyofunza Ashira, walikuwepo vijana tisa wa kiume wa miaka kati ya ishirini na mbili na thelathini waliokuwa walimu. Mishahara yao ilikuwa duni sana. (Ukurasa 84)

> *Sababu ni kwamba walifahamu jinsi ajira ilivyoadimika miongoni mwa vijana, hivyo wakapata fursa ya kuwadhulumu wale waliotafuta kazi kwao. Walifahamu. fika kwamba vijana hao hawakuwa na njia ya kujitoa katika mtego wa uhitaji walimokuwa. Walionaswa mtegoni walikuwa watumwa wa kiuchumi ambao bwanyenye yeyote angeweza kujitwalia na kuwatumikisha alivyotaka. Wangefanyaje na asasi za serikali zilishindwa kuwaajiri?*

Ni wazi kuwa vijana hawa hawakunyanyaswa tu waajiri wao bali pia serikali iliwanyanyasa. Walitumikishwa walivyotaka kwa sababu waliona kuwa walikuwa na haja ya ajira na kuwalipa mishahara duni.

Kiragi katika riwaya hii ya *Utelezi (2023)* anaweza kunyanyaswa na shangazi yake Shija. Anamuahidi kuwa atampa laki mbili baada ya kutekeleza njama yao. Hata hivyo shangazi yake anamgeuka. Kila mara anapokwenda kudai pesa hizo shangazi yake anamzungusha kwa kuahidi kumpa siku nyingine. Aidha, Shija alitaka Kiragi amsaidie tena katika njama ya pili, lakini

anakataa. Hivyo ndivyo alivyoweza kugundua kuwa Shija hakuwa na mpango wa kumlipa hata ingawa alikuwa na pesa hizo. (Ukurasa 168)

> *Maneno hayo yalimwambia Karagi kwamba hatalipwa. Haikuwa kweli hata kidogo kwamba shangazi yake alisubiri kuuza magari ili amlipe shilingi laki mbili. Hata kama kiasi Karagi alichodai kilikuwa laki mbili mara kumi, Shija angemtolea kwenye akaunti yake ya benki na kumlipa. Karagi alichemka roho ukweli mchungu ulipomdhihirikia. Kimoyomoyo, akaanza kufikiria njia ya kumlipa Shija kwa ujeuri wake. "Dawa ya moto ni moto," alijiambia kimoyomoyo.*

Hii ni ishara ya unyanyasaji kwani Shija alitendea Kiragi mabaya. Unyanyasaji huu unamuathiri kiragi kiasi cha kuzaa chuki moyoni mwake. Chuki hii inamfanya kuanza kutafuta mbinu ya kumuangamiza Shija.

Kwa kuzingatia Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, changamoto ya unyanyasaji inaeleweka kupitia mihimili ya pili na ya tatu, inayosisitiza uhusiano kati ya mazingira ya jamii na changamoto za vijana wa kiume. Ushahidi wa riwaya unaonesha kuwa changamoto hii haiwezi kutenganishwa na mazingira na mahusiano yanayomzunguka kijana. Kwa mtazamo wa mtafiti, hoja muhimu hapa ni kwamba matarajio ya jamii na mazingira ya kijamii yanaweza kuongeza uzito wa changamoto anayopitia kijana wa kiume, badala ya changamoto hiyo kuwa suala la mtu binafsi pekee.

4.3.5. Changamoto za Mihadharati

Mihadarati ni kemikali hatari zinazoweza kubadilisha akili na tabia ya mtu, na zinaweza kudhuru afya yake. Vijana wengi hujiingiza kwenye matumizi ya mihadarati kwa kushawishiwa na marafiki au kutafuta suluhisho la matatizo ya maisha. Kwa mujibu wa Carney na wenzake (2022), matumizi ya mihadarati huathiri vibaya ubongo wa vijana na huwafanya kupoteza mwelekeo wa maisha. Hii inaonesha kuwa ni muhimu kuelimisha jamii, hasa vijana, kuhusu madhara ya mihadarati na kuwa na msaada wa kisaikolojia kwa waathiriwa. Waandishi na watunzi wa fasihi huweza kuwaumba wahusika walioathiriwa na mihadharati ili kutumika kama funzo kwa wasomaji. Hata ingawa wahusika wa jinsia yoyote huweza kuathirika na mihadharati, vijana wa kiume huweza kukumbwa sana na changamoto hii.

Riwaya ya *Njozi Yapata Mtenzi* (2018), inabainika wazi kuwa matumizi ya mihadharati ni changamoto mojawapo inayowakumba vijana wa kiume. Katika kile kibanda ambacho Kiguto

anafanyia upelelezi, anawasikiza vijana wa kiume kama vile Njoro na Dan ‘wakijitibu’ kwa kujidunga kokeni kwenye mishipa.

> *"Relax Njoro. Acha kuteta. Una haraka gani? Kwani unaenda kunyonesha?" "Shika Dan umtilie yake. Ni kiu inamsumbua." Kiguto hakuhitaji kusikiliza zaidi. llikuwa wazi kwamba shughuli iliyokuwa ikiendelea ni kujitia kokeni kwenye mishipa ya damu kwa kujidunga sindano. Alilipia chai, akainuka na kutoka. Akaenda, kufikiria la kufanya. Sasa alijua kile kioski kilikuwa maficho ya biashara ya mihadarati. (ukurasa 26)*

Kwa upande mwingine, mwandishi Mwenda mbatia katika *Utelezi* (2023) anamuumba Raiku na kuonesha changamoto za mihadhariti katika maisha yake. Raiku ni kaka mdogo wa Tony. Baada ya Raiku kufeli mtihani wake wa kitaifa, anafunguliwa biashara ya kuuza spea ya magari. Biashara hiyo inakosa kufuaulu kwa sababu anabugia maisha ya ulevi na majisifu akiwa na dadake.

> *Kage na Raiku walikuwa wapenda-raha. Hela zote ambazo zilitokana na biashara yao, walizitumia katika ulevi na anasa. nyingine halali na haramu. (Uk.93)*

> *Hufanyia nini hela zote wapatazo?" Karagi alishangaa. "Mihadarati. Wanatumia unga. Isitoshe, wana mashabiki chungu nzima. Wao ndio matajiri wa kuwagawia marafiki kokeni. Pia hunywa pombe kupindukia na kukamatwa mara kwa mara. (Uk 166)*

Mwishowe uraibu huu wa mihadharati unamfanya Raiku kuzua rabsha katika klabu moja kule Mlolongo. Akampiga na kumung’oa meno. Jambo hili lilimfanya kukamatwa na kuhukumiwa kifungo cha miaka mitatu. Hili ni changamoto hasa kwani inamuathiri sana Raiku na kumfanya kuwa mraibu wa unga. Hivyo kuanza kutumia mali ya wazazi wake vibaya.

Kwa kuzingatia Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, changamoto ya mihadharati inaeleweka kupitia mihimili ya pili na ya tatu, inayosisitiza athari za mazingira, jamii na matarajio ya uanaume. Ushahidi wa riwaya unaonesha kuwa changamoto hii haiwezi kutenganishwa na mazingira na mahusiano yanayomzunguka kijana. Kwa mtazamo wa mtafiti, hoja muhimu hapa ni kwamba matarajio ya jamii na mazingira ya kijamii yanaweza kuongeza uzito wa changamoto anayopitia kijana wa kiume, badala ya changamoto hiyo kuwa suala la mtu binafsi pekee.

4.3.6. Changamoto za Uongozi Mbaya

Uongozi mbaya unaweza kuwa chanzo kikuu cha matatizo mengi yanayowakumba vijana. Unapokosekana uwajibikaji na maadili miongoni mwa viongozi, vijana hukosa mifano mizuri ya kuigwa. Hupoteza pia imani katika mifumo ya kijamii na kisiasa. Connell (2005) anasema kuwa vijana wengi hukata tamaa kwa kukosa matumaini kutoka kwa viongozi. Hali hii huwachochea wengine kuingia uhalifuni na kutumia dawa za kulevya. Connell (2005) anaonya kuwa uongozi mbovu hujenga jamii isiyo na dira. Vijana ndio waathirika wakuu wa mkanganyiko huo. Kwa hivyo, kuwawezesha vijana kuwa na maisha bora kunahitaji uongozi unaowajibika na unaoweka maslahi yao mbele. Ni dhahiri kuwa uongozi mbaya huzaa matatizo mengi ya vijana.

Changamoto hii inajidhihirisha wazi katika riwaya ya Utelezi (2023). Vijana kama Tony walikuwa na matumaini makubwa na katiba mpya. Alidhani ingekuwa zana bora ya kutatua matatizo kama ukosefu wa ajira na ufisadi. Baadaye, dereva wa teksi anamfafanulia Tony kuwa ukosefu wa ajira ulichangiwa na uongo wa waliomadarakani.

> *Tumeahidiwa mangapi na wenye madaraka? Oo, ajira nusu milioni kila mwaka...Oo, nyumba za maskini kama mimi nusu milioni kila mwaka...Oo, masomo ya bure shule za msingi. Uongo unaonuka. Kama kuna kitu wanajua hao fisi, ni kudanganya mchana kweupe. Kama mchawi kuroga watu bila kujificha." (uk. 111)*

Hali hii imewaacha wengi wa vijana wakikosa ajira. Vijana hawa wanakosa hela za kuunua kazi hivyo inapelekea katika changamoto ya ufisadi. Hali hii inampelekea Tony kutafuta kazi kwenye nchi ya Sudan Kusini ambapo kuna vita.

Kwa kuzingatia Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, changamoto ya uongozi mbaya inaeleweka kupitia mihimili ya pili ya tatu, inayosisitiza athari za mazingira, jamii na matarajio ya uanaume. Ushahidi wa riwaya unaonesha kuwa changamoto hii haiwezi kutenganishwa na mazingira na mahusiano yanayomzunguka kijana. Kwa mtazamo wa mtafiti, hoja muhimu hapa ni kwamba matarajio ya jamii na mazingira ya kijamii yanaweza kuongeza uzito wa changamoto anayopitia kijana wa kiume, badala ya changamoto hiyo kuwa suala la mtu binafsi pekee.

4.3.7. Changamoto za Ubaguzi

Ubaguzi inaweza kujadiliwa kama kitendo cha kutowachukulia watu wote kwa usawa kutokana na tofauti za rangi, kabila, jinsia au hali zao za kijamii, Jambo hili huweza kuleta maumivu na kuvunja mshikamano wa kijamii. Vijana wanaoathirika na ubaguzi wakati mwingine hukosa fursa muhimu kama elimu, ajira na haki za msingi, jambo linalowarudisha nyuma kimaendeleo. Kwa mujibu wa Connell (2005), Ubaguzi hujenga ukuta wa hofu na chuki miongoni mwa vijana, na kuwafanya wajihisi kama wageni katika nchi yao wenyewe.

Tony katika *Utelezi* anakumbwa na changamoto la ubaguzi anapoenda Sudani Kusini kutafuta kazi. Wenyeji wa Sudani wanawabagua watu wanaotoka katika nchi iliyotofauti na yao. Ubaguzi huu unamkosesha Tony amani. Hakuwa amewahi kumbwa na tatizo hili. Analazimika kuwa mwangalifu kila mara ili aweze kuepukana nao. Aidha anakubali kuwa kitika nchi yake kuna ubaguzi ambao huendelezwa kwa misingi ya ukabila.

> *Tatizo la ukabila nchini mwake pia alilifahamu. Lakini hakuwahi kukabiliana na uhalisi wa kubaguliwa katika misingi ya kuwa mgeni katika nchi ya wenyewe. Wenyeji aliofanya kazi nao walionesha uhasama wa wazi dhidi ya wageni. Baadhi ya Wasudani walikuwa na mtazamo hasi wa kwamba wageni walikuja kuwanyang'anya wenyeji kazi zao. Llibidi awe mwangalifu na ajitahidi kuepukana nao kila ilipowezekana. (uk 160)*

Ubaguzi huwa na athari zake kwa mtu yeyote. Tony anaathirika kiasi cha kuwaogopa wenzake. Hata hivyo, anajikaza kwa sababu anahitaji kazi. Mhimili wa tatu wa nadharia hii unaonesha kuwa jamii ina mchango mkubwa katika changamoto za vijana wa kiume. Katika sehemu hii, Tony anapitia ubaguzi kutokana na ulegevu wake wa kutojitetea. Hii ni hali halisi inayowakumba vijana wanyonge jamiini. Vijana wa kiume wanatakiwa kuwa jasiri, na woga kidogo huwaletea shida kubwa.

Kwa mujibu wa nadharia hii, changamoto ya ubaguzi inaeleweka kupitia mihimili ya pili na ya tatu. Mihimili hii inasisitiza athari za mazingira, jamii na matarajio ya uanaume. Ushahidi wa riwaya unaonesha kuwa changamoto hii haiwezi kutenganishwa na mazingira yanayomzunguka kijana. Kwa mtazamo wa mtafiti, matarajio ya jamii yanaweza kuongeza uzito wa changamoto hiyo. Changamoto hii si suala la mtu binafsi pekee.

4.3.8. Changamoto za Usaliti

Hali ya kukosa uaminifu kwa mtu au kundi, na mara nyingi husababisha maumivu makubwa ya kihisia na kuvunjika kwa mahusiano ya kijamii au kifamilia ni usaliti. Usaliti, huweza kuleta msukosuko wa kihisia kama huzuni, hasira na kukosa kujiamini, hasa kwa vijana wanaojifunza kuamini wengine. Connell (2005) anasema, Usaliti huacha kovu la muda mrefu katika nafsi ya kijana, na mara nyingi husababisha matatizo ya kisaikolojia kama msongo wa mawazo na upweke. Hali hii huweza pia kuwa kikwazo katika maendeleo ya kijamii na kitaaluma endapo kijana atajifungia na kukosa msaada wa kihisia.

Vijana wa kiume kama vile Tony katika *Utelezi* (2023) anakumbwa na changamoto ya usaliti. Hii ni baada ya kuchumbiana na Doris na hata kumpata mtoto wa kike. Tony anapokosa kazi nchini Kenya na kuenda Sudani Kusini, alitaka waende na Doris ila wazazi wa Doris walipinga. Baada ya muda, Dorris anaamua kuolewa kama mke wa pili Mwalimu mkuu wa shule aliyokuwa akifundisha, Bwana Omar Malik. Huu ulikuwa usaliti wa hali ya juu kwani Tony alikuwa amempenda sana Doris na alitarajia kufunga ndoa naye siku moja. Tony anapopata Habari hii anavunjwa moyo na hata kulia sana.

> *Filipo alimwandikia barua ndefu kumjuza habari za Doris kumpeleka Eva kwa nyanyake huko Kitengela na kuolewa na Omar Malik. Tony alilia kwa uchungu. Akajaribu kuwasiliana na Doris, lakini ilikuwa kazi bure. Baada ya kuvunja uchumba wao, hata mawasiliano kati yao Doris aliyavunja. (ukurasa 190)*

Kwa upande wake Doris hakujutia kitendo chake cha usaliti kwania aliamini kuwa sasa amekuwa pragmatist. Usaliti huu unaathiri sana hisi za Tony.

Kwa upande mwingine ni wazi kuwa viongozi walioteuliwa waliwasalati wananchi kwa kukosa kutimiza ahadi walizotoa kabla ya uchaguzi. Wanaahidi kuunda nafasi za ajira kwa vijana ila wanakosa kutimiza. Wanaahidi kukomesha ufisadi laki ndio wanaokuwa kwenye mstari wa mbele kuiongoza. Hali hii ya usaliti unawatisha vijana wengi matumaini kwa viongozi wao.

Kwa kuzingatia Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, changamoto ya usaliti inaeleweka kupitia mihimili ya pili na ya tatu, inayosisitiza uhusiano kati ya mazingira ya jamii na changamoto za vijana wa kiume. Ushahidi wa riwaya unaonesha kuwa changamoto hii haiwezi kutenganishwa na

mazingira na mahusiano yanayomzunguka kijana. Kwa mtazamo wa mtafiti, hoja muhimu hapa ni kwamba matarajio ya jamii na mazingira ya kijamii yanaweza kuongeza uzito wa changamoto anayopitia kijana wa kiume, badala ya changamoto hiyo kuwa suala la mtu binafsi pekee.

4.3.9 Changamoto za Utelekezwaji

Utelekezwaji ni hali ambapo wahusika hukosa huduma, ulinzi na mazingira bora ya maisha licha ya kutarajiwa kupatiwa msaada na taasisi au watu wanaowajibika. Katika muktadha wa vijana wa kiume, utelekezwaji hujitokeza kupitia maisha duni, ukosefu wa miundombinu bora na hali zinazoathiri ustawi wao wa kimwili na kisaikolojia. Riwaya ya *Njozi Yapata Mtenzi* ya Mwenda Mbatia inaangazia namna vijana wa kiume wanavyoachwa wakikabiliana na maisha magumu bila msaada unaostahili, hasa katika mazingira ya kazi na makazi.

> *Kiguto alikubaliana naye, akaaga na kwenda kupumzika. Wakati huu alikuwa anaishi katika nyumba za polisi hapo kituoni. Vilikuwa vyumba uchwara vilivyojengwa katika safu ndefu kama madarasa ya shule. Chake kilikuwa nambari tano kwenye safu ya vyumba kumi na viwili. Bafu na vyoo vilikuwa nje, na wakazi wote kumi na wawili walishindania vyoo viwili na bafu mbili. Vyumbani, ilikuwa na nafasi ya kitanda, meza ndogo na viti viwili. Hapakuwa hata na kabati la nguo. Nguo ziling'inizwa kwenye misumari ya ukutani. (Uk. 27)*

Katika dondoo hili, utelekezwaji unaonekana wazi kupitia maisha ya Kiguto anayelazimika kuishi katika nyumba za polisi zilizo katika hali duni. Vyumba hivyo vinaelezwa kuwa "uchwara," vikiwa vimejengwa kwa mtindo wa madarasa ya shule na kukosa huduma muhimu kama kabati la nguo. Aidha, wakazi kumi na wawili wanalazimika kushindania vyoo viwili na bafu mbili, hali inayoashiria msongamano na ukosefu wa heshima kwa utu wa binadamu. Mazingira haya yanaonesha namna taasisi inayopaswa kumlinda na kumjali kijana wa kiume inavyomtelekeza, na kumwacha akiishi katika mazingira yasiyofaa. Hali hii inadhihirisha kuwa licha ya kujituma kwake kazini, Kiguto anakumbwa na utelekezwaji wa kijamii na kitaasisi unaodhoofisha maisha yake.

Kwa kuzingatia Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, changamoto ya utelekezwaji inaeleweka kupitia mihimili ya pili na ya tatu, inayosisitiza uhusiano kati ya mazingira ya jamii na changamoto za vijana wa kiume. Ushahidi wa riwaya unaonesha kuwa changamoto hii haiwezi kutenganishwa na mazingira na mahusiano yanayomzunguka kijana. Kwa mtazamo wa mtafiti, hoja muhimu hapa

ni kwamba matarajio ya jamii na mazingira ya kijamii yanaweza kuongeza uzito wa changamoto anayopitia kijana wa kiume, badala ya changamoto hiyo kuwa suala la mtu binafsi pekee.

4.3.10 Changamoto za Shinikizo la Marika

Shinikizo la marika ni athari hasi au chanya inayotokana na ushawishi wa rika katika tabia na maamuzi ya mtu. Kwa mujibu wa nadharia ya uwezo mkuu wa kiume, vijana wa kiume hukabiliwa na shinikizo la kuthibitisha uanaume wao. Hufanya hivyo kwa kuonesha nguvu, mamlaka na mafanikio ya kiuchumi. Hii hutokea hata pale uwezo huo haupo. Mara nyingi hali hii huchangiwa na wanarika wenzao, wanaotaka kufanana nao. Hali hii inaweza kuwaweka matatani. Baadhi yao hujihusisha na tabia hatarishi. Tabia hizo ni pombe, dawa za kulevya, na vurugu. Wengine huficha hisia zao ili waonekane "wanaume halisi". Shinikizo hili mara nyingi hujitokeza wakati vijana wanapotafuta utambulisho au kukubalika. Riwaya ya Njozi Yapata Mtenzi inaonesha kuwa shinikizo la marika huchangia mkengeuko wa tabia miongoni mwa vijana.

> *Tony alimfuata unyounyo. Aliweza kuchunguza ambapo mamake alikuwa nao. Alifahamu fika kwamba hata babake hafurahishwi na uzembe wa watoto wake hao. Walitoka hotelini na kurudi kando ya barabara walipopacha gari. Mama akafungua, kuingia kwenye kiti cha dereva na kuwasha gari. Tony alingia na kuketi kiti cha nyuma. Mamake alipindua gari, akalirudisha barabarani. Zilimia kumbukizi za miaka ya nyuma wakati alishika mimba na kumzaa Tony katika utata na hali iliyofaa kuzikwa katika kaburi sahau. Akaisha kuwa kifungua mimba katika familia yao. Moyo wa mama ukawa mgiza*. (Uk. 20)
>
> *"Nitaendelea kujitahidi kuwashauri ndugu zangu. Sikubali kwamba wana upungufu wa akili. Nionavyo, pengine wamepatana na marafiki wasiofaa," Tony alineno.*
>
> *"Babako alitamka maneno ambayo hayatofautiani na hayo kuhusu Raiku na Kage kupatana na marafiki wasiofaa. Alisema ni peer pressure, yaani shinikizo la marika," mamake alieleza na kuendelea kushughulikia uendeshaji wa gari. (UK.21)*

Katika dondoo la ukurasa wa 20 na 21, shinikizo la marika linaonekana kupitia mazungumzo kati ya Tony na mamake. Tony anatambua kuwa mienendo isiyofaa ya ndugu zake huenda inachangiwa na marafiki wanaowazunguka. Kauli yake kwamba "pengine wamepatana na marafiki wasiofaa" inaonesha uelewa wa athari za marika katika mienendo ya vijana. Aidha, mamake Tony

anathibitisha hoja hii kwa kunukuu kauli ya baba yao kwamba matatizo ya Raiku na Kage yanatokana na "peer pressure, yaani shinikizo la marika." Hii inaonesha wazi kuwa vijana wa kiume wamesawiriwa kama waathirika wa mazingira ya kijamii yanayowasukuma kuiga tabia zisizofaa ili kukubalika miongoni mwa wenzao. Kwa hivyo, shinikizo la marika linajitokeza kama changamoto inayohitaji uangalizi wa wazazi na jamii kwa ujumla.

Kwa kuzingatia Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, shinikizo la marika inaeleweka kupitia mihimili ya pili na ya tatu, inayosisitiza athari za mazingira, jamii na matarajio ya uanaume. Ushahidi wa riwaya unaonesha kuwa changamoto hii haiwezi kutenganishwa na mazingira na mahusiano yanayomzunguka kijana. Kwa mtazamo wa mtafiti, hoja muhimu hapa ni kwamba matarajio ya jamii na mazingira ya kijamii yanaweza kuongeza uzito wa changamoto anayopitia kijana wa kiume, badala ya changamoto hiyo kuwa suala la mtu binafsi pekee.

4.3.11. Changamoto za Umaskini na Hali Duni ya Kiuchumi ya Familia

Umaskini ni hali ya kukosa mahitaji ya kimsingi kutokana na ukosefu wa rasilimali za kutosha, na huweza kuathiri pakubwa mtazamo na maamuzi ya mtu maishani. Connell (2005) anaeleza kuwa umaskini wa kifamilia huwafanya baadhi ya vijana kuchukua njia za mkato ili kujinasua kutoka katika hali duni ya maisha, hata kama njia hizo si za haki. Katika riwaya teule za Mwenda Mbatia, umaskini unajitokeza kama changamoto iliyowahi kuwakumba baadhi ya vijana wa kiume katika utoto wao, na kuathiri maamuzi yao ya baadaye.

Katika *Utelezi* (2023), Gitunge, babake Doris, ni mfano wa kijana aliyekumbwa na umaskini mkali utotoni mwake, hali iliyokuja kuathiri mienendo yake ya baadaye alipokuwa mtu mzima.

> *Aliogopa umaskini kama panya amwogopavyo paka, na alifanya juu chini kuepukana nao. Kwa vile alitokana na familia ya wachochole, aliuonja umaskini utotoni mwake. (uk.118)*

Dondoo hili linaonesha jinsi hofu ya umaskini iliyojengeka ndani ya Gitunge tangu utotoni ilivyomfanya, alipokuja kupata nafasi ya kazi na mamlaka, kutumia njia za rushwa na ufisadi ili kujilimbikizia mali - akiogopa kurudi katika hali ile ile ya umaskini aliyoifahamu utotoni. Kwa mujibu wa Connell (1995), mazingira ya awali ya makuzi ya mwanaume, hasa yale yanayohusiana na uchumi wa familia yake, huchangia pakubwa katika kuunda mtazamo wake wa baadaye kuhusu mafanikio na jinsi ya kuyafikia. Ni wazi kuwa umaskini wa utotoni wa Gitunge ulichangia kuunda ndani yake mtazamo hasi uliomsukuma baadaye kutumia njia zisizofaa kujiepusha na hali hiyo,

jambo linaloonesha jinsi changamoto za kiuchumi za utotoni zinavyoweza kuathiri mienendo ya kijana hata anapokuwa mtu mzima.

Kwa kuzingatia Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, umaskini na hali duni ya kiuchumi ya familia inaeleweka kupitia mihimili ya pili na ya nne, inayohusisha matarajio ya kijamii na mgawanyo wa majukumu na fursa. Ushahidi wa riwaya unaonesha kuwa changamoto hii haiwezi kutenganishwa na mazingira na mahusiano yanayomzunguka kijana. Kwa mtazamo wa mtafiti, hoja muhimu hapa ni kwamba matarajio ya jamii na mazingira ya kijamii yanaweza kuongeza uzito wa changamoto anayopitia kijana wa kiume, badala ya changamoto hiyo kuwa suala la mtu binafsi pekee.

4.3.12. Changamoto za Ushindani Mkubwa wa Kupata Nafasi za Elimu ya Juu

Vijana wengi wa kiume katika riwaya teule wanakumbwa na changamoto ya ushindani mkubwa wa kupata nafasi chache za masomo ya juu, hali inayosababishwa na uchache wa asasi za elimu ikilinganishwa na idadi kubwa ya wanafunzi wanaohitimu. Mwangi (2021) anaeleza kuwa ukosefu wa fursa za kutosha za elimu ya juu huwafanya vijana wengi kukata tamaa hata kabla ya kujaribu, kwani wanajua uwezekano wa kufaulu ni mdogo.

Katika *Utelezi* (2023), Tony na Filipo wanakabiliwa na changamoto hii wanapotarajia kujiunga na vyuo vikuu kusomea taaluma walizozipenda.

> *Taaluma walizotaka kusomea ziliwachukua tu wanafunzi waliopata gredi ya A. Kwa hivyo kulikuwa na ushindani mkali miongoni mwa wale waliotaka kusajiliwa katika chuo kikuu kusomea taaluma hizo. Vitivo vilivyohusika viliteua asilimia arobaini hivi ya wale waliotuma maombi. Wengine waliambulia patupu. (uk.7)*

Takwimu hii ya asilimia arobaini pekee ya waombaji kupata nafasi inaonesha ukubwa wa changamoto hii kwa vijana wanaotaka kuendeleza masomo yao. Kwa mujibu wa Connell (2005), mifumo isiyowatengea vijana wa kiume fursa za kutosha za kujiendeleza kielimu huwafanya wajihisi kushindwa hata kabla ya kujaribu, jambo linaloathiri sana afya yao ya kisaikolojia. Ushindani huu unaonesha kuwa hata vijana wenye bidii na uwezo mkubwa masomoni, kama Tony na Filipo, wanaweza kukwamizwa na uhaba wa fursa za kitaifa zisizohusiana kabisa na uwezo wao binafsi.

Kwa kuzingatia Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, ushindani mkubwa wa kupata nafasi za elimu ya juu inaeleweka kupitia mihimili ya pili na ya nne, inayohusisha matarajio ya kijamii na mgawanyo wa majukumu na fursa. Ushahidi wa riwaya unaonesha kuwa changamoto hii haiwezi kutenganishwa na mazingira na mahusiano yanayomzunguka kijana. Kwa mtazamo wa mtafiti, hoja muhimu hapa ni kwamba matarajio ya jamii na mazingira ya kijamii yanaweza kuongeza uzito wa changamoto anayopitia kijana wa kiume, badala ya changamoto hiyo kuwa suala la mtu binafsi pekee.

4.3.13. Changamoto za Msongo wa Mawazo Unaotokana na Mtihani wa Kitaifa

Mfumo wa elimu unaomtegemea mtihani mmoja kama kigezo kikuu cha mafanikio ya maisha ya mwanafunzi huweza kuwa chanzo cha msongo mkubwa wa mawazo kwa vijana. Connell (2005) anaeleza kuwa shinikizo la kutaka kufaulu mtihani mmoja mkuu huwafanya wanafunzi wengi kuhisi kwamba thamani yao yote kama binadamu inapimwa katika muda mfupi wa siku chache, hali inayoweza kusababisha msongo mkubwa wa kisaikolojia.

Katika *Njozi Yapata Mtenzi* (2018), Mwenda Mbatia anaonesha wazi jinsi mtihani wa kitaifa ulivyokuwa chanzo cha wasiwasi mkubwa kwa vijana wa kiume kama Kiguto.

> *Muhula wa tatu ukafika, maandalizi ya mtihani wa Kitaifa wa kidato cha nne yakapamba moto. Nchi nzima iliugua homa ya wasiwasi juu ya mtihani huu. Kwa vijana wengi, hili lilikuwa jaribio kuu la maishani mwao. Walikabiliana na uhalisi wa kutisha juu ya nafasi ya mtihani kama nguzo kuu ya mfumo mzima wa elimu nchini. Uhalisi katili wa thamani ya binadamu kupimwa katika mizani ya mtihani uliodumu siku chache. Kufeli mtihani kulimaanisha kufeli katika maisha, na kufaulu katika mtihani kulimaanisha kufaulu katika maisha. (uk.115-116)*

Maneno 'uhalisi katili wa thamani ya binadamu kupimwa katika mizani ya mtihani' yanadhihirisha jinsi mfumo huu wa elimu unavyoweza kuwa mgumu na wa kikatili kisaikolojia kwa vijana. Kwa mujibu wa Connell (2005), mifumo ya uwezo mkuu wa kiume huwafunza wanaume kutoonesha udhaifu wala kutafuta msaada wa kihisia, hali inayowafanya vijana wengi kubeba mzigo huu wa msongo wa mtihani peke yao bila kuueleza wala kuutafutia msaada. Ni dhahiri kuwa mfumo wa elimu unaomtegemea mtihani mmoja unaweza kuwa chanzo cha changamoto kubwa ya

kisaikolojia kwa vijana wa kiume, hasa ikizingatiwa kwamba jamii huwatarajia wasionyeshe woga au wasiwasi wao waziwazi.

Kwa kuzingatia Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, msongo wa mawazo unaotokana na mtihani wa kitaifa inaeleweka kupitia mihimili ya pili na ya tatu, inayosisitiza uhusiano kati ya mazingira ya jamii na changamoto za vijana wa kiume. Ushahidi wa riwaya unaonesha kuwa changamoto hii haiwezi kutenganishwa na mazingira na mahusiano yanayomzunguka kijana. Kwa mtazamo wa mtafiti, hoja muhimu hapa ni kwamba matarajio ya jamii na mazingira ya kijamii yanaweza kuongeza uzito wa changamoto anayopitia kijana wa kiume, badala ya changamoto hiyo kuwa suala la mtu binafsi pekee.

4.3.14. Changamoto za Kuvunjika kwa Familia na Kunyimwa Malezi ya Wazazi Wote Wawili

Mojawapo ya changamoto kubwa zinazowakumba vijana wa kiume ni kunyimwa fursa ya kulelewa na wazazi wao wote wawili, hali inayoweza kutokana na kifo, kifungo au migogoro mingine ya kifamilia. Kimmel (2017) anaeleza kuwa kukosekana kwa mzazi mmoja au wote wawili katika hatua za mwanzo za makuzi ya kijana huweza kuathiri uwezo wake wa kujenga uhusiano thabiti wa kihisia na wengine baadaye maishani.

Katika *Njozi Yapata Mtenzi* (2018), Kiguto anakumbwa na changamoto hii pale mamake anapohukumiwa kifungo cha maisha kwa kosa ambalo hakulitenda, jambo linalomwacha bila malezi kamili ya kimzazi katika kipindi muhimu cha ujana wake.

> *Aliamini kwamba kwa njia moja au nyingine, atapata uwezo wa kumtoa mamake gerezani na kufuta dhuluma iliyomharibia maisha yake. (uk.95)*

Ni wazi kuwa Kiguto analazimika kukua bila uwepo wa mamake katika nyumba yao, akitegemea zaidi ami yake kwa malezi. Kwa mujibu wa Izugbara (2005), kunyimwa malezi ya wazazi wote wawili huweza kumfanya kijana kuchukua majukumu ya kimaisha kabla ya wakati wake, jambo linaloonekana wazi kwa Kiguto anayelazimika kuwa na mtazamo wa kutafuta suluhu za kisheria akiwa bado kijana mdogo. Changamoto hii ya kuvunjika kwa familia inaonesha jinsi mifumo ya kisheria na kijamii isiyofaa inavyoweza kuwaathiri vijana wasio na hatia, na kuwafanya wabebe mizigo mizito kabla ya wakati wao.

Kwa kuzingatia Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, kuvunjika kwa familia na kunyimwa malezi ya wazazi wote wawili inaeleweka kupitia mihimili ya pili na ya tatu, inayosisitiza uhusiano kati ya mazingira ya jamii na changamoto za vijana wa kiume. Ushahidi wa riwaya unaonesha kuwa changamoto hii haiwezi kutenganishwa na mazingira na mahusiano yanayomzunguka kijana. Kwa mtazamo wa mtafiti, hoja muhimu hapa ni kwamba matarajio ya jamii na mazingira ya kijamii yanaweza kuongeza uzito wa changamoto anayopitia kijana wa kiume, badala ya changamoto hiyo kuwa suala la mtu binafsi pekee.

4.3.15. Vitisho vya Kudhuriwa Vinavyotokana na Migogoro ya Kifedha

Vijana wengi wa kiume, hasa wanaofanya kazi za vibarua au shughuli zisizo rasmi, hukumbwa na hatari ya kutishiwa maisha yao pale wanapodai stahiki zao za kifedha kutoka kwa waajiri au watu wenye mamlaka juu yao. Connell (2005) anaeleza kuwa migogoro ya kifedha isiyoshughulikiwa ipasavyo mara nyingi huweza kuzaa uhasama wa hatari, hasa pale ambapo pande zinazohusika zina siri za pamoja zinazoweza kufichuka.

Katika *Utelezi* (2023), Karagi anajikuta katika hatari kama hiyo baada ya kudai malipo yake kutoka kwa Shija, mwenye njama naye, ambaye anapuuza madai yake mara kwa mara.

> *Nilipe kwanza. Safari hii sitakubali ahadi tupu. Basi kama hutaki hela, nitatafuta mtu mwingine. Usifikirie ni wewe tu unayeweza kufanya kazi kama hiyo, Shija aliendelea kumshinikiza Karagi. (uk.167)*

Kutokana na jinsi Shija anavyomtishia kumtafutia mtu mwingine wa kufanya kazi ile ile waliyoifanya kwa siri, Karagi anajikuta katika mazingira hatarishi ambayo yangeweza kumletea madhara endapo angeamua kuchukua hatua kali zaidi. Kwa mujibu wa Connell (2005), migogoro ya kifedha inayohusisha watu wenye siri za pamoja huweza kuwa hatari zaidi kuliko migogoro ya kawaida, kwani upande mmoja unaweza kuamua kuchukua hatua za kutisha ili kulinda usiri wao. Hali hii inaonesha kwamba vijana wa kiume wanaojihusisha katika mipango ya kificho na watu wenye mamlaka zaidi ya wao mara nyingi hujikuta wakiwa katika nafasi dhaifu, wasiokuwa na uwezo kamili wa kudai haki zao bila kuhatarisha usalama wao wenyewe.

Kwa kuzingatia nadharia ya uwezo mkuu wa kiume, vijana wa kiume hukumbwa na matatizo mbalimbali. Matatizo haya hutokana na mambo mbalimbali ya kimazingira. Mambo hayo huwafanya baadhi yao kuamini kuwa mwanaume wa kweli ni mwenye nguvu, jasiri na mwenye

mamlaka wakati wote. Kutokana na hali hiyo, wengi hupitia msongo wa mawazo. Hushindwa pia kueleza hisia zao na huogopa kutafuta msaada. Wengine hujihusisha na tabia hatarishi. Tabia hizo ni pombe, dawa za kulevya, vurugu na uhalifu. Wanajihusisha nazo ili kuthibitisha uanaume wao mbele ya wenzao na jamii.

Aidha, nadharia hii inaonesha kuwa si vijana wote wanaoweza kufikia viwango vinavyowekwa na jamii kuhusu uanaume. Hali hiyo husababisha baadhi yao kukumbwa na matatizo ya kiuchumi, kukosa ajira, kushuka kwa hali ya kujiamini, kutengwa kijamii na migogoro katika mahusiano ya kifamilia na kijamii. Kadhalika, shinikizo la kutaka kudumisha hadhi ya uanaume linaweza kuwafanya wapuuze elimu, wajibu wao au fursa za maendeleo kwa kuhofia kuonekana dhaifu. Kwa hivyo, matatizo haya yanaonesha kuwa dhana ya uwezo mkuu wa kiume inaweza kuwa chanzo cha changamoto zinazozuia vijana wa kiume kujijenga kikamilifu na kushiriki kwa ufanisi katika maendeleo yao binafsi na ya jamii.

Kwa kuzingatia Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, vitisho vya kudhuriwa vinavyotokana na migogoro ya kifedha inaeleweka kupitia mihimili ya pili na ya tatu, inayosisitiza uhusiano kati ya mazingira ya jamii na changamoto za vijana wa kiume. Ushahidi wa riwaya unaonesha kuwa changamoto hii haiwezi kutenganishwa na mazingira na mahusiano yanayomzunguka kijana. Kwa mtazamo wa mtafiti, hoja muhimu hapa ni kwamba matarajio ya jamii na mazingira ya kijamii yanaweza kuongeza uzito wa changamoto anayopitia kijana wa kiume, badala ya changamoto hiyo kuwa suala la mtu binafsi pekee.

4.4. Nafasi ya Jamii Katika Kukuza Vijana wa Kiume Katika Riwaya Teule.

Jamii ina nafasi muhimu katika kuwakuza vijana wa kiume. Inaweza kuathiri tabia, maadili na mtazamo wao kuhusu maisha. Familia, shule, dini na vyombo vya habari huchangia kumwelekeza kijana kuwa na maadili mema. Kimmel (2017) anasema kuwa jamii inayowekeza katika malezi ya vijana hujenga kizazi chenye nidhamu na ujasiri. Bila usaidizi wa jamii, vijana wa kiume huweza kupotea na kuathirika na vishawishi vya maisha ya kisasa.

Kwa mujibu wa nadharia ya uwezo mkuu wa kiume, jamii hujenga na kusambaza mitazamo ya uanaume. Hufanya hivyo kupitia familia, shule, dini na makundi ya rika. Connell (1995) anaeleza kuwa jamii huweka viwango vya mwanaume bora. Viwango hivyo ni uwajibikaji, uongozi, na

uwezo wa kutunza familia. Hata hivyo, Connell anasisitiza kuwa viwango hivyo havipaswi kutumika kutawala wengine. Vinapaswa kuwa msingi wa kujenga vijana wenye maadili mema. Jamii inapaswa kuwapa vijana malezi ya nidhamu, heshima, na uwajibikaji. Malezi haya huwasaidia kutambua kuwa uanaume wa kweli haujengwi kwa ukatili au ubabe. Unajengwa kwa tabia njema.

Messerschmidt (1993) anaeleza kuwa uanaume hujengwa kupitia matendo na mazingira ya kijamii. Jamii ina wajibu wa kuwaongoza vijana kwenye mienendo inayokuza maendeleo. Kimmel (2017) anabainisha kuwa vijana hujifunza maana ya uanaume kutoka kwa wazazi na walimu. Wanapopata mifano bora, hujenga mtazamo chanya kuhusu maisha. Kwa hiyo, jamii inapaswa kuwahimiza vijana kuthamini elimu na kufanya kazi kwa bidii. Inapaswa kuwahimiza kuheshimu usawa wa kijinsia na kueleza hisia zao ipasavyo. Hivyo, jamii si tu chanzo cha matarajio ya uanaume. Ni pia nguzo muhimu ya kuwalea vijana wenye maadili na mchango chanya.

Izugbara (2005) anaeleza kuwa jamii ina mchango mkubwa katika kuwakuza vijana wa kiume. Huchangia sana katika maadili na mtazamo wao. Hali hii hubadilika kulingana na jamii na vipindi vya kihistoria. Vijana hawakui kwa upekee pekee. Mienendo yao huchangiwa na mazingira yao. Jamii ni sehemu ya mazingira hayo, hivyo huwaathiri kwa njia moja au nyingine.

Aidha, jamii inapaswa kutoa fursa sawa kwa vijana kushiriki katika maamuzi na maendeleo. Wasitazamwe kama watu wasiohitaji msaada wa kijamii. Wanapaswa kuhusishwa kikamilifu katika mijadala ya kijamii. Kimmel (2017) anasisitiza kuwa jamii inayowatenga vijana katika malezi huandaa mazingira ya kuzalisha wanaume wasiojiamini. Kwa hivyo, ni jukumu la jamii kuwalea vijana kwa upendo na uwajibikaji ili wawe watu bora wa kesho.

Katika tamaduni mbalimbali, vijana na watoto walikuwa sehemu muhimu ya jamii. Jamii ilikuwa na jukumu la kukuza maadili mema miongoni mwao. Ni wazi kuwa jamii ilikuwa na mchango hasi au chanya katika maisha yao. Waandishi wa fasihi huumba na kuwasilisha hali hii kupitia kazi mbalimbali.

Mara nyingi jamii huipa jinsia ya kiume majukumu kulingana na mila na desturi zake. Hii ni njia mojawapo ambayo jamii huwakuza vijana bila hata kujitambua. Janvan (2023) anaeleza kuwa asasi mbalimbali huchangia mienendo ya vijana. Asasi hizo ni elimu, siasa na uchumi. Asasi hizi huzua mwamko mpya kwa jinsia ya kiume. Jinsia hii inapaswa kutafakari nafasi yao jamiini, na kujikomboa kutoka mifumo hasi ya kitamaduni.

Connell (1987) anaeleza kuwa wanajamii huwa na mchango katika maisha ya mtu. Jamii huweza kujenga imani na mtazamo wa mtu. Malezi kutoka kwa wazazi na jamii huchangia maadili na mienendo yake. Mhimili huu ni muhimu katika sehemu hii. Umeongoza ufafanuzi wa mchango wa wanajamii katika kuwakuza vijana wa kiume katika riwaya teule za Mwenda Mbatia. Mchango huo unaweza kuwa hasi au chanya.

4.4.1. Mchango Chanya wa Jamii kwa Vijana wa Kiume.

Wanajamii wengi katika riwaya teule za Mwenda Mbatia wamekuwa na mchango chanya katika kuwakuza vijana wa kiume. Katika riwaya ya *Njozi Yapata Mtenzi* (2018), wahusika wengi hasa katika kitengo cha kifamilia wamechangia pakubwa katika kuwakuza vijana wa kiume. Kwanza Gasoya, mamake Kiguto anajitahidi katika kumtia moyo mwanawe hata ingawa yuko gerezani. Anamtaka mwanawe ajitahidi sana masomoni ili baadaye aweze kuja kumuokoa. Anamhimiza pia kuwa anapaswa kujifunza kijutegemea na kumpa maarifa yatakyomsaidia maishani. Hii inaonekana kupitia kwa barua ambayo Gasoya alimuandikia Kiguto.

> *Simaanishi kwamba uanze kujisumbua kwa kunifikiria. Hilo halitasaidia kamwe. Unavyoweza kunisaidia ni kusoma kwa bidii. Ufanisi wako ndio ufunguo utakaonifungulia nitoke humu. Jifunze kujitegemea ukifahamu kwamba wakupendao wanaweza kutoweka wakati wowote. (Uk. 94)*

Ni wazi kuwa mama alimtakia mema mwanawe na hivyo alitaka kuumba mtazamo Chanya maishani mwake kupitia kwa barua hiyo. Mama huyu pia alifahamu umuhimu wa masomo hivyo alimhimiza sana kujitahidi katika masomo yake. Kwa upande mwingine babake pia alijitahidi na kuwajibika katika kumlea mwanawe kwa njia iliyosawa. Kupitia kwa barua ambayo Joe alimwandikia Kiguto kabla ya kufanyiwa opareshen, alimhimiza mwanawe kuwa muwajibikaji na kuwatunza mama yake na wadogo zake. Alimuhitaji awe mvumilivu ajaribu awezavyo kudhibiti hisia zake ikiwa ataaga.

Nimeamua kukuandikia ili nawe uwe chonjo. Wewe sio mtoto tena, kwa hivyo lazima uyakabili machungu ya maisha kama mwanamume. Sitaki nikifa unifuate kaburini kwa sababu ya mshtuko au huzuni, uhitaji na mambo mengine yasiyo na maana. Endapo nitakufa, natakabuyadhibiti maisha yako ipasavyo. Uwaangalie mama zako wawili na wadogo wako Shaka na Koitalel. (UK. 210)

Joe alimtaka mwanawe aweze kijitahidi na kuwajibika maishani. Hata kabla ya kuiaga dunia babake Kiguto anamwuachia uridhi kupitia kwa Kapteni Onemi. Hii ilipaswa kumsaidia Kiguto katika maisha yake ya baadaye na wenzake. Ni wazi kuwa mzazi huyu alijukumika katika kumlea mwanawe na alitake awe na tabia njema na aweze kujukumika. Sio tu katika masomo bali pia katika kuwalea wadogo zake. Connell (1987) kwa kuangazia Nadhiria ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, anasema kuwa mwanaume anapaswa kuwa na sifa angama kama vile kulinda familia yake pamoja na kuwajibika. Hali hii inadhihirishwa babake Kiguto anapomkumbusha kuwa hela atakazozipata azitumie kulea familia na wale awapendao. Kwani alimtaka aweze kuwajibika na kuwa mkakamavu.

Nimeidhinisha ulipwe künuamgongo cha kazini kwangu kwa niaba yangu. Utaenda makao makuu ya jeshi usaidiwe ipasavyo. Muhimu zaidi ni kwamba nikiwa kazini, nilipata, kwa bahati, kibweta kilichojaa almasi yenye thamani ya shilingi milioni mia mbili. Tumesaini mkataba, mimi na ofisa mwenzangu aitwaye Kapteni Onemi. Unakuja kwa njia ya posta. Mkataba unasema baada ya kuiuza mali hiyo, achukue milioni laki moja, yaani nusu, aniachie milioni laki moja. Zangu upewe wewe. Utafuatilia haya pia makao makuu ya jeshi kwa sababu kikosi chetu kitarudi nchini hivi karibuni baada ya kukamilika kwa kazi tuliyojia huku. Ukipata shida yoyote juu ya kiinuamgongo au mgawo wangu kutoka kwa Onemi, muone bosi wangu. Anaitwa Kanali Idrisi. Ni muungwana, atakusaidia. Mwisho, utatajirika sana baada ya kupata pesa hizo zote. Zitumie vizuri kufanikisha maisha yako na ya wale uwapendao. (uk 210-211)

Ami yake Kiguto hata ingawa alikuwa na upungufu wake, alijitahidi awezavyo katika kumpa mkono kiguto. Kiguto alipohitaji karo za kulipia katika chuo cha askari wa upelelezi, alimlipia bila kusita. Ishara kwamba alielelewa umuhimu wa masomo kwa maisha ya kijana huyo (ukurasa 7).

“Wanataka kiasi gani katika chuo cha kutoa mafunzo ya upelelezi?"

"Kozi nzima ya mwaka mmoja itagharimu elfu arobaini. Inawezekana pia kulipa elfu kumi kwa awamu nne," Kiguto alijibu.

"Bora kulipa zote safari moja tusahau," ami yake alipendekeza.

"Kweli ba'mkubwa."

"Basi nitakutumia kesho kwa mtandao wa simu ili ukalipe," ami yake alisema.

"Ahsante sana ba' mkubwa," Kiguto alishukuru kwa dhati. (Uk.7-8)

Kando na hayo alijaribu sana kumsaidia Kiguto alipoifufua kesi ya mamake. Hii ilikuwa mbinu mojawapo aliyotumia akiwa na matumaini ya kufunga kurasa na sura mbaya katika ukoo wake. Hivyo alimfaa sana Kiguto katika hali hii.

Mark Bagite alishiriki kikamilifu katika jitihada za Kiguto za kumkomboa mamake. Alikuwa na matumaini kwamba sura hiyo ya kuchukiza katika ukoo wake itafungwa hatimaye. Aliwatambulisha polisi ambao walikula njama kumfungisha Gasoya. Ilikuwa njia ya kulipiza kisasi kwa jinsi marehemu Joe Bagite alivyowapiga wenzao waliojaribu kumkamata mkewe. (Uk 279)

Katika riwaya ya *Utelezi* (2023), familia mbali mbali hasa zilizo na vijana wa kiume wanajitolea katika kuwa sehemu ya mchango chanya ya maisha yao. Babake Filipo anaelewa umuhimu wa masomo hivyo, anajitahidi vyema kumuelekeza na kumuelimisha. Babake Tony anapoiga dunia, anajitolea katika muelekeza Tony. Anampa nasaha ya kurudi kurudia kidato cha nne na hata kumpa makazi. Alikuwa na Imani kuwa Tony alikuwa mwerevu na nafasi hiyo ya pili ingempa nafasi nyingine ya kujiunga na chuo kikuu. Hii inadhihirishwa kupitia kwa barua anayomuandikia Tony.

Je, kuna mlango mwingine wa kuingilia chuo kikuu kusomea uhandisi ujenzi? Jawabu ni kwamba upo, japo utahitaji jitihada na ujasiri kuufikia. Napendekeza kwamba ujisajilishe kama private candidate wa KCSE mwaka huu na uanze kujiandaa kuufanya tena mtihani huo mwishoni mwa mwaka… Pia udurusu wako utakuwa ukikatizwa na shughuli za nyumbani. Ili kuepukana na hayo, napendekeza uhamie kwangu Nakuru. (Uk 59)

Tony aliikumbatia nafasi hii na kupata nafasi ya kufuzu katika mtihani wake wa kitaifa. Kufuzu kwake kulichangiwa sana na ami yake. Babake Tony alikuwa wa mchango Chanya katika maisha

ya wanawe hasa Tony. Alihakikisha wanawe walipata elimu kwani alimini elimu ingeweza kufungua milango ya mbeleni. Kila mara alipokuwa na wanawe hasa Tony aliweza kumpa nasaha za kimaisha. Alipofanya vyema alimpongeza na wadogo wa Tony, aliweza kuwahimiza watie bidii kwenye masomo yao. Alimhimiza kuzungumza na wadogo zake kuhusu umuhimu wa kutia bidi masomoni.

"Hongera tena, Tony," Maselu alisema."

"Na nyie Raiku na Kage.Nataka kuona mabadiliko. Haya mambo ya kushika mkia katika matokeo ya mitihani ya mwisho wa muhula hayanipendezi hata kidogo. Yananifanya kuhisi kama napoteza hela zangu kuwalipia karo.""

"Nimeshaongea nao, baba. Wameniahidi kwamba watajifunga kibwebwe na kuboresha maksi zao. Mbali na kubukua kwangu likizo hii, nitawasaidia katika masomo yao. Mambo yatakuwa mazuri," Tony alimhakikishia babake.

Ni Dhahiri kwa Tony alipata maelekezo mazuri kutoka kwa babake ndiposa pia anaweza kuwaongoza wadogo zake hasa masomoni. Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume unasisitiza kuwa tabia na sifa za mtu binafsi huweza kuchangiwa na jamii. Katika nafasi hii tabia zake Tony hasa za kuwajibika na kuwa mwenye bidii iliweza kuchangiwa na babake.

Nkalia anachangia katika kuwatia vijana wake hamasa ya kujituma katika masomo yao. Anawasisitizia ya kwamba hata ingawa aliwaruhusu kushiriki katika michezo waliyoipenda kwa dhati haikamaanisha kwamba hayo ndio yatakuwa maisha yao ya kila siku, lazima wazingatie ndoto zao za siku za usoni.

Hatimaye, Nkalia alisafisha koo na kusema: “Hata kama tuliwaruhusu kwenda kushiriki katika mashindano hayo, haimaanishi kwamba tunataka uendeshaji baiskeli iwe ndiyo kazi yenu. Tunataka mmakinikie masomo yenu. Najua wewe Tony unataka kuwa mhandisi ujenzi kama babako. Nawe, Filipo unataka kuwa tabibu kama mjombako, kwa sababu unaichukia taaluma ya babako. Hamwezi kupata nafasi ya kusomea taaluma hizo bila kushinda katika mtihani wa kitaifa kwa alama za juu. Mmebakisha mwaka mmoja tu kufanya mtihani wenyewe. Au vipi Mama Filipo?” (Uk 4-5)

Mchango chanya wa jamii kwa vijana wa kiume pia unajitokeza kupitia watu wa nje ya familia wanaowekeza katika vipaji na maslahi ya vijana. Katika *Utelezi* (2023), Alibhai, mfanyabiashara tajiri wa Kihindi mjini Nakuru, anachangia pakubwa katika kukuza vipawa vya michezo miongoni mwa vijana wa eneo hilo, akiwemo Tony na Filipo.

> *Alibhai ndiye aliyemiliki klabu ya Nakuru Riders. Aliwanunulia vijana baiskeli na kuajiri kocha wa kuwafunza stadi za kuendesha baiskeli za michezo. (uk.3)*

Uwekezaji huu wa Alibhai unawapa vijana kama Tony na Filipo nafasi ya kujiendeleza kimichezo huku wakiendelea na masomo yao, jambo linalodhihirisha kuwa mchango chanya wa jamii kwa vijana wa kiume hauhitajiki kutoka kwa familia pekee, bali unaweza pia kutolewa na wanajamii wengine wenye nia njema. Kwa mujibu wa Kimmel (2017), jamii inayowekeza katika vipaji vya vijana - iwe ni vya kitaaluma au vya kimichezo - huwajengea vijana hao nidhamu na kujiamini, sifa muhimu katika ukuaji wao wa kiuanaume.

Aidha, walimu wa Tony na Filipo katika Shule ya Upili ya Baraka nao wanachangia kwa njia chanya katika maisha ya vijana hawa, kwa kuwahamasisha kujibidiisha masomoni licha ya vipawa vyao vya kimichezo.

> *Walimu wao walifahamu uteuzi wao wa taaluma za kusomea chuo kikuu na waliwatia moyo kila uchao wasilegee. (uk.7)*

Mchango huu wa walimu unaonesha kuwa taasisi za elimu, kama sehemu ya jamii pana, zina wajibu muhimu wa kuwaelekeza vijana wa kiume katika njia sahihi za kufaulu maishani. Kwa mujibu wa Kimmel (2017), vijana wa kiume hujifunza mengi kuhusu maana ya kujituma na kufanikiwa kutoka kwa walimu na viongozi wanaowazunguka, na wanapopata mwongozo huo mzuri, huwa na uwezekano mkubwa zaidi wa kujenga mtazamo chanya kuhusu maisha yao ya baadaye.

Kwa mtazamo wa mtafiti, mchango chanya wa jamii unaonesha utekelezaji wa mihimili ya tatu na ya nne ya Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, kwa kuwa jamii hujenga hulka na pia huweka matarajio kuhusu majukumu ya kijinsia. Hivyo, mchango wa jamii umejadiliwa kwa kuonesha pande zote mbili, yaani namna unavyoweza kumjenga kijana na namna unavyoweza kumdhoofisha.

4.4.2. Mchango Hasi wa Jamii kwa Vijana wa Kiume.

Baadhi ya wahusika katika riwaya za Mwenda Mbatia wameonesha mchango hasi katika maisha ya vijana wa kiume. Kwa mtujibu wa Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume, wanajamii wanaweza kuwa na mchango hasi katika malezi yao. Hili hudhihirika wanapoendeleza mitazamo inayohusisha uanaume na nguvu, ubabe na ukali. Hudhihirika pia wanapokosa kuwarekebisha vijana, hali inayoweza kuharibu maisha yao ya baadaye.

Connell (1987) anaeleza kuwa vijana hujifunza mengi kupitia familia, marika, vyombo vya habari na taasisi za kijamii. Wanajifunza kuwa mwanaume anapaswa kuficha hisia zake. Wanajifunza pia kutafuta mamlaka kwa njia yoyote na kuepuka kuonesha udhaifu. Matarajio haya huwafanya baadhi yao kuiga tabia mbaya. Tabia hizo ni pamoja na vurugu, matumizi mabaya ya pombe, na uhalifu. Zinahusisha pia dharau kwa wengine na kupuuza ushauri unaowajenga. Aidha, wanajamii wanapohalalisha mienendo hiyo kama ishara ya uanaume, huendeleza dhana potofu. Dhana hizo huwazuia vijana kujenga maadili mema na mahusiano ya heshima.

Kwa mujibu wa nadharia hii, jamii inaweza kuwa sehemu ya tatizo. Hii hutokea inapokuza mitazamo inayowasukuma vijana kuthibitisha uanaume wao kwa njia zinazowadhuru. Kwa mfano, Mark Bagite katika Njozi Yapata Mtenzi (2018) ana mchango hasi katika malezi ya wanawe Rejwa na Mwogi. Wanawe hawana bidii masomoni. Wanapofeli mtihani, baba yao anampa mwalimu mkuu soda ili wapate nafasi katika shule bora.

> *Licha ya pesa nyingi alizomwaga kuwapeleka shule bora za kibinafsi, hawakufanikiwa masomoni. Mwishowe, aliwapeleka shule ya umma ambapo mpwa wake - Kiguto alisomea baada ya kumnunulia soda mkuu wa shule. ili abuni nafasi ya wavulana wawili ambao walifeli. (uk 98)*

Pale shuleni, wafanyakazi kama vile yule mpishi wa kike anahusika katika kuwafichia rununu zao ambazo zimepigwa marufuku shuleni. Mlinda lango naye aliwaletea mihadharati kama vile bangi walipokuwa shuleni. Hawa ni baadhi ya jamii wanapaswa kurekebisha maadili ya pacha hawa ila wanaendeleza maadili hayo mabaya. Hali hii inaendeleza utundu miongoni mwa vijana hawa. Baba yao aliwatumia pesa nyingi kila mwezi na hizo ndizo pesa walizotumia kuwalipa waliowasaidia katika uhalifu wao.

Malezi ambayo baba yao alijua ni kuwapa watoto pesa. Kila mwezi, aliwatumia kichele kilicholingana na mshahara wa tarishi wa shule. Mbali na kuwapa hela nyingi, aliwanunulia kila walichotaka. Rununu, baiskeli, vipakatalishi vya kuchezea... Kwa hali hii, hawakuthamini hela na walizitumia ovyoovyo. Ziliwatumbukiza katika maovu chungu nzima. (uk 114).

Malezi haya waliyopata kutoka kwa baba yao ilizidi kuwafanya watundu kiasi kwamba walifeli kwenye mtihani wao wa kitaifa. Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume unahitaji jamii kuwa sehemu muhimu ya kurekebisha jinsia ya kiume hasa vijan. Jambo hili lisipofanywa, vijana hwa huishia kupotoka katika maadili. Hata baada ya kufeli anajaribu tena kuwanunulia nafasi ya pili katika shule hio. Mwishowe baba yao annamua kutumia mlango wa nyuma ili wanawe wapate nafasi katika chuo cha mafunzo ya polisi (uk 281)

Kabla ya kustaafishwa, baba yao aliwatafutia njia ya kuingia katika chuo cha mafunzo ya polisi. Kama kawaida yake, alitumia mlango wa nyuma. Wakamaliza mafunzo na kuanza kazi ya polisi.

Malezi haya yalikuwa na mchango hasi sana kwa maisha ya vijana hawa kwani utundu waliokuwa nayo ilitokana na hayo malezi. Pesa walizopewa ziliwafanya kujihusisha na mambo mengi kama vile matumizi ya mihadharati na kutoa hongo kwa wafanyakazi. Walifahamu kuwa baba yao angewa chochote walichotaka hivyo kukosa hata kutia bidii katika masomo yao. Mwishowe Rejwa alihusika katika alimpiga bosi wake na kufutwa kazi. Mwogi naye alipoteza silaha ya kazi kwa sababu ya ulevi.

Mwogi alipigwa kalamu kwa kupoteza silaha yake akiwa mlevi kazini. Naye Rejwa alimwaga unga kwa kumpiga bosi wake. Wawili hao walipata ajira katika biashara za baba yao. Rejwa alikuwa meneja wa shamba la kahawa, naye Mwogi alikuwa msimamizi wa majumba ya kukodisha. Mapato yao yote yaliishia ulevini. (ukurasa 281)

Kwa upande mwingine katika riwaya hiyo hiyo, kijana wa mwenye klabu Monika alikofanya kazi alikuwa mtukutu sana na alijihusisha katika uhalifu mbalimbali. Siku moja aimpiga na kumuumiza Monika mpaka kuzirai. Hali hii ilipelekea kufungwa kwa kijana huyo. Hata hivyo, babake alitumia pesa zake kumtoa mwanawe mashimoni. Baba mtu alikuwa na mazoea haya. Kila mara kijana huyu alipojikuta pabaya, babake alitoa hongo awachiliwe

Kilichomsumbua ni kwamba kijana aliyehusika alikuwa mwanawe wa pekee. Kwa hali hii, alikuwa tayari kufanya chochote ili aepukane na kifungo. Haikuwa mara ya kwanza kwa kijana huyo kukamatwa kwa jinai mbalimbali. Kila mara, babake alitumia hela kumtoa mashimoni. (ukurasa 167).

Mwishowe kijana huyu anakosa kusaidiwa na pesa za babake hivyo kuishia kukamatwa. Malezi ya baba huyu yanakuwa na madhara hasi kwa kijana huyu kwani anabugia ulevi na vitendo vya kikatili akijua kuwa iwapo atashikwa babake atamtoa shimoni. Malezi yanakuja kumuathiri kwa njia hasi wakati anafungwa kifungo cha miaka saba.

Kesi iliendelea kwa mwezi mmoja. Hatimaye, kijana alipatikana na hatia ya kumpiga na kumuumiza Monika. Alihukumiwa kifungo cha miaka saba. (uk 168)

Katika dondoo hili, mchango hasi wa jamii kwa vijana wa kiume unaonekana kupitia mgawanyo usio sawa wa majukumu ya malezi na ushiriki wa wazazi katika maisha ya watoto. Jamii inasawiriwa kuwaweka akina baba pembeni kwa kuhalalisha kutokuwapo kwao katika masuala muhimu ya malezi, kama kuhudhuria mikutano ya wazazi shuleni, kwa kisingizio cha kutafuta riziki. Matokeo yake, vijana wa kiume hukosa uangalizi wa karibu, mwongozo na mfano wa kuigwa kutoka kwa baba zao. Hali hii inaoneshwa pale ambapo wazazi wa kike wanatawala mkutano huku wanaume wakikosekana, kama ilivyo kwa Mhandisi Maselu aliyekuwa mbali kazini Kampala. Jamii kwa njia hii inachangia malezi pungufu ya vijana wa kiume kwa kuendeleza dhana kwamba malezi ni jukumu la mama pekee, hali inayoweza kusababisha vijana hawa kukua bila mwelekeo thabiti wa kimaadili na kijamii.

Miongoni mwa wazazi alikuwepo Shija, mamake Tony. Pia alikuwepo Maria, mamake Filipo. Kwa jumla, wazazi wa kike walikuwa wengi kuliko wale wa kiume. Hii ilikuwa ishara ya uhalisi wa mambo mintarafu malezi ya watoto kote nchini. Mara nyingi, akina mama ndio walioachiwa kazi ya kuhudhuria mikutano ya wazazi katika shule za watoto wao. Waume wao walihairi kwenda kuchuma. Mfano ni Mhandisi Maselu, ambaye alikuwa akimalizia kandarasi yake ya ujenzi wa barabara mjini Kampala, Uganda. Ilibidi mkewe afunge biashara yake mjini Kitengela na kuhudhuria hafla ya siku hiyo kwa ajili ya mwanao.

Katika sehemu hii, mchango hasi wa jamii kwa vijana wa kiume unajitokeza kupitia mazingira ya vurugu, hofu na uhalifu yanayowasukuma vijana kuhusishwa na vitendo hatarishi. Kim na Dan wanasawiriwa kama vijana wadogo waliokamatwa katika mnyororo wa uhalifu unaodhibitiwa na watu wakubwa kama Okuti na Nyangwe, jambo linaloashiria jamii inayoshindwa kuwalinda na kuwaongoza vijana wake. Vitisho, kipigo na matumizi ya nguvu yanayotumiwa na Majunju yanaonesha jamii inayotatua matatizo kwa ukatili badala ya haki na maadili. Hali hii inawafanya vijana kuishi kwa hofu, wakilazimika kuficha ukweli au kushiriki uhalifu ili kuokoa maisha yao. Kwa namna hii, jamii inachangia moja kwa moja kupotosha mwelekeo wa vijana wa kiume kwa kuwalea katika mazingira yasiyo na usalama, haki wala mifumo thabiti ya ulinzi na malezi bora.

"Okuti. Ali-ni-a-chi-chia ni-ni-muuzie," Kim aligugumia.

"Peleka sisi kwake saa hii!" Majunju alisema kwa sauti iliyokata kama kisu.

"Si-si-jui kwa-ke."

Kofi kali la shavuni lililorushwa na mkono la Majunju lilimfanya Kim ayumbeyumbe kama mlevi.

"Utapeleka sisi kwa Okuti?"

"D-Dan ndi-ndiye a-na-na-ju-ua kwa-ke."

"Nyote wawili mtatupeleka huko. Sawa?" Kiguto alinguruma.

"Sawa!" Walisema kwa pamoja wale vijana wadogo waliokuwa wakitetemeka kama wagonjwa wa homa.

"Nyinyi nafanyia nani hii kazi?" Majunju alifyatua swali jingine.

Kim na Dan walitupiana jicho la kuulizana, tuseme tusiseme? Akili zao zilienda mbio kama risasi kutokana na hatari iliyowakabili. Hapakuwa na nafasi ya tahadhari wala uongo. Lakini ukweli pia ulikuwa na hatari zake. Kuwafichua majambazi sugu kilikuwa kitendo cha kuufungulia kifo mlango. Majunju alikuwa karibu kuinua mkono lake tena, jawabu lilipokuja.

"Okuti na Nyangwe. Hiki kioski ni chao," Kim alijibu. (Uk. 42)

Katika upande mwingine, mchango hasi wa jamii kwa vijana wa kiume unaonekana kupitia mfano mbaya unaotolewa na maofisa waandamizi wanaotumia mamlaka yao vibaya kujinufaisha kinyume cha sheria. Mark Bagite, Babake mkubwa wa Kiguto, ambaye angetarajiwa kuwa mlezi na kielelezo cha maadili mema, anasawiriwa kama mshiriki wa mauaji. Pia anashiriki katika uporaji kwa lengo la kujipatia utajiri. Kitendo chake cha kuwaua wahalifu, kuficha ukweli wa mauaji, na hata kujipatia pesa kwa njia haramu kinaonesha jamii inayohalalisha ufisadi, ukatili na tamaa ya mali. Hali hii inamweka kijana wa kiume katika mkanganyiko wa kimaadili, kwani anashuhudia mafanikio yakipatikana kupitia njia chafu badala ya juhudi halali. Ingawa Kiguto anakataa mwenendo huo, mshangao na maumivu anayopata yanaonesha athari hasi za jamii inayoshindwa kulinda maadili na kuwalea vijana wake kwa misingi ya uadilifu, haki na utu.

> *Mtindo wa maofisa waandamizi kutumia njia chafu kupata utajiri uliozoleka. Alikikumbuka kile kisa cha mauzi ambacho alichukulia kwamba babake mkubwa ameenda kuwakamata wahalifu waliomuua tajiri mwenye Range Rover. Kumbe mzee huyo alienda kuwinda ngawira! Hakushughulikia hata kuripoti mauaji yaliyotokea. Alipomsimulia hadithi nzima siku chache baadaye, Kiguto alijicheka mwenyewe kwa ujinga wake. Kwaufupi, ami yake aliwaua wezi waliomnyang'anya yule mzee ngawira, akajipatia milioni tatu kimya kimya. Keshoye alienda akanunua nyumba katika mtaa wa Igunge na kuikodisha. Ukatili wa babake mkubwa ulimshangaza sana. 'Kama hii ndiyo njia ya kupata utajiri, wacha ukae!' Aliapa kimoyomoyo.*

Katika riwaya ya *Utelezi* (2023), malezi yaliyo na athari hasi kwa vijana wa kiume yanajitokeza. Ni wazi kuwa malezi mabovu huwa na athari mbovu kwa vijana haw ana huwenda ikaathiri maisha yao ya usoni. Vijana kama vile Raiku na dadake wanaathirika vibaya kutokana na malezi ya mamake mzazi. Raiku hakutia bidii masomoni kwani aliamini wazazi walikuwa na pesa za kutosha. Hii ilitokana jinsi mamake alivyowapa pesa kila mara walipoenda shuleni. Shija mama ya kina Tony hakupenda masomo hivyo kila mara alitoa kauli hasi kuhusu masomo (ukurasa 133).

> *Nao mchango mkubwa wa kuharibika kwao kitabia, hata kama hawakutambua hilo, ulitoka kwa mama yao, haswa kuwadekeza kwa mahela wakiwa shuleni. Pia kauli zake za mara kwa mara kuubeza usomi na wasomi kama mumewe.*

Mwishowe Raiku na dadake walifeli katika mtihani wao wa kitaifa. Mama yao hakuona shida kwani hakujali masomo sana. Aliamua kuwafungulia wanawe duka la kuuza spea za magari. Pesa zote walizopata walitumia kwa mihadharati. Duka lao lilipofilisika mara tatu kwa sababu ya kutowajibika kwao, mama yao hakusita bali alilijaza tena. Hali hii iliwafanya kina raiku kuwa na mazoea mabaya (ukurasa 166).

> *...wamefilisi duka nililowafungulia kwa mara ya tatu na sasa sijui nifanyeje…*
>
> *"Hufanyia nini hela zote wapatazo?" Karagi alishangaa."Mihadarati. Wanatumia unga. Isitoshe, wana mashabiki-chungu nzima. Wao ndio matajiri wa kuwagawia marafiki kokeni. Pia hunywa pombe kupindukia na kukamatwa mara kwa mara. Balaa tupu!"*

Ni wazi kuwa mama Raiku Aliona jinsi wanawe walivyopotoka lakini hakuwarekebisha. Hali hii inachangia Raiku kua akiwa na minendo mibaya hasa katika matimizi ya mihadharati. Raiku siku moja anakwenda kwenye klabu na kuzua rabsha. Alimpiga meneja wa klabu hio na kumtoa meno. Alitiwa mbaroni na kuhukimiwa kifungo cha miaka mitatu.

> *"Kama kawaida yake, Raiku alizusha rabsha ulevini, akampiga meneja wa klabu moja huko Mlolongo na kumng'oa meno." "Mungu wangu!" Tony alimkatiza kwa mshtuko.*
>
> *"Akaitiwa polisi, wakamtia ndani. Siku chache baadaye, alifunguliwa mashtaka. Alihukumiwa kifungo cha miaka mitatu..."*

Hii ilitokana na mamake Raiku kukosa kumrekebisha mwanawe tangia mwanzoni. Nadharia ya uwezo mkuu unajadili kuwa baadhi ya watu wa jinsia ya kiume huweza kujihusisha na uhalifu na mienendo mibaya katika jamii. Hata hivyo wana uwezo wa kubadili mienendo yao iwapo watapata mwongozo au watajirekebisha wenyewe Janvan (2023). Mwongozo ambao vijana wa kiume huhitaji hutoka katika jamii na familia yake. Raiku alipojishulisha na mihadharati mamake hakumkanya, badala yake alipokamatwa alitoa hongo. Walipofilisi duka alilijaza tena bila kujali hivyo kumfanya Raiku kuvimba kichwa na kuwa mtundu.

Mchango hasi wa jamii kwa vijana wa kiume pia unajitokeza kupitia mifumo ya rushwa inayowanufaisha baadhi ya vijana kwa njia zisizo za haki, hali inayowakosesha wengine fursa walizostahili. Katika *Njozi Yapata Mtenzi* (2018), Mwenda Mbatia anaonesha jinsi mwalimu mkuu

wa Shule ya Upili ya Wateule alivyopokea rushwa ili kuwaingiza wana wa Mark Bagite shuleni humo kinyume na taratibu za kawaida za kusajiliwa.

> *Kuingia kwa Mwogi na Rejwa katika shule hii kulivunja jadi ndefu ya kushindania nafasi za kujiunga nayo kihalali, na kwa uwazi, usawa na haki. [...] Mwalimu mkuu alikuwa amelipwa shilingi milioni moja kuwafungulia mlango wa nyuma watoto wa Mark Bagite kuingia shuleni humo. (uk.109-110)*

Kitendo hiki cha rushwa kinaonesha jinsi baadhi ya wanajamii wenye mamlaka wanavyoweza kuathiri vibaya maisha ya vijana wengine wenye sifa lakini wasio na uwezo wa kifedha wa kuhonga, kwa kuwanyima fursa halali walizostahili kupitia jitihada zao za kimasomo. Kwa mujibu wa Connell (2005), ufisadi wa aina hii hauathiri tu wale wanaonufaika kwa njia isiyo halali, bali pia unawakatisha tamaa wale wanaofuata njia sahihi za kufuzu, na kuwafanya wapoteze imani katika mifumo ya haki na usawa. Rejwa na Mwogi, waliopata nafasi kwa njia hii ya udanganyifu, baadaye wanaoneshwa wakijihusisha na matumizi ya mihadarati (tazama 4.2.7), jambo linaloonesha kuwa mafanikio yanayopatikana kwa njia ya udanganyifu badala ya jitihada za kweli hayana msingi imara wa kuwajenga vijana kimaadili. Connell (1995) anasisitiza kuwa jamii inapowapa vijana mafanikio yasiyotokana na jitihada zao wenyewe, huwajengea mtazamo potovu kwamba mafanikio ya kweli hayahitaji nidhamu wala uwajibikaji, jambo linalowaandaa vibaya kwa changamoto za maisha ya baadaye.

Kwa ujumla, Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume inaonesha kuwa jamii ndiyo msingi mkuu wa kuwakuza vijana wa kiume. Jamii huwaelekeza katika kujenga uanaume wenye tija. Kupitia malezi bora, elimu, na ushauri, jamii inaweza kuwasaidia vijana kujenga maadili ya uwajibikaji na heshima. Inaweza kuwajengea uadilifu na kujituma. Hii hufanyika badala ya kuamini kuwa uanaume hupimwa kwa nguvu au utajiri pekee. Jamii inapotekeleza wajibu wake ipasavyo, huwajengea vijana uwezo wa kukabiliana na changamoto. Huwajengea pia uwezo wa kufanya maamuzi ya busara na kuwa raia wenye mchango chanya.

Kwa mtazamo wa mtafiti, mchango hasi wa jamii unaonesha utekelezaji wa mihimili ya tatu na ya nne ya nadharia. Jamii hujenga hulka na pia huweka matarajio ya majukumu ya kijinsia. Hivyo, mchango wa jamii umejadiliwa kwa pande zote mbili. Umeonesha namna unavyoweza kumjenga kijana na namna unavyoweza kumdhoofisha.

Jamii yenye kuwarekebisha vijana wa kiume huwa na mchango Chanya katika maisha yao. Vijana hao hukuwa kwa njia bora na kuiga mfano unaotolewa na wanajamii. Wanapokuwa wao huwa na mienendo bora kama wenye bidii na wenye kuwajibika katika jamii. Wao huweza hata kutumika kama mfano bora. Kwa upande mwingine, wanajamii wasiowarekebisha vijana hawa huweza kutoa mchango hasi kwa maisha yao. Vijana hawa huishia kuwa watundu na wengine hata kuishia kubugia dawa za kulevya. Hali hii huwafanya watu wasio na dhamani katika jamii na wakati mwingine kuharibu maisha yao wenyewe.

4.5. Hitimisho

Utafiti huu umedhihirisha kuwa vijana wa kiume katika riwaya teule wamesawiriwa kwa njia mbalimbali. Mtunzi Mwenda Mbatia amewasawiri kwa kuangazia hulka zao. Amezingatia pia jinsi wanavyotagusana na wenzao. Imedhihirika kuwa vijana hawa hukumbwa na changamoto mbalimbali. Changamoto hizi mara nyingi huchangiwa na mazingira yao. Jamii nayo ina mchango katika mienendo yao. Hii ni kwa sababu jamii huhusika katika malezi yao kwa njia moja au nyingine.

SURA YA TANO

MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1. Utangulizi

Sura hii inatoa muhtasari wa tasnifu nzima. Inatoa pia hitimisho la utafiti na mapendekezo yaliyotokana na matokeo. Muhtasari huo unazingatia mchakato mzima wa utafiti. Unaanzia usuli wa mada na tatizo la utafiti. Unajumuisha maswali na malengo ya utafiti. Unahusisha pia mapitio ya maandishi na msingi wa kinadharia. Unaendelea na muundo na mbinu za utafiti. Unaishia na matokeo yaliyowasilishwa katika Sura ya Nne.Aidha, sura hii inatoa hitimisho kwa kuzingatia maswali matatu ya utafiti. Inaonesha jinsi Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume ilivyofaa kufafanua matokeo. Mwishoni, sura inatoa mapendekezo. Mapendekezo haya yanahusu utafiti wa vijana wa kiume katika Fasihi ya Kiswahili, hususan katika tanzu ya riwaya.

5.2. Muhtasari wa Tasnifu na Matokeo ya Utafiti

Tasnifu hii ilichunguza taswira ya vijana wa kiume katika Njozi Yapata Mtenzi (2018) na Utelezi (2023). Utafiti ulitokana na pengo lililobainika katika maandishi yaliyohakikiwa. Pengo hilo lilihusu haja ya kuchunguza kwa pamoja usawiri wa vijana wa kiume, changamoto zao, na nafasi ya jamii katika kuwaendeleza. Utafiti ulilenga vijana wa kiume kwa sababu uzoefu wao unahusiana kwa karibu na matarajio ya kiuanaume, majukumu ya kijinsia, na mazingira yao. Malengo matatu yalikuwa kubainisha usawiri wao katika riwaya teule, kujadili changamoto zao, na kuchanganua mchango wa jamii katika kuwakuza.

Sura ya Kwanza iliweka msingi wa utafiti. Ilijadili usuli wa mada, tatizo la utafiti, na maswali na malengo yake. Ilieleza pia sababu za kuchagua mada, umuhimu wa utafiti, na upeo na mipaka yake. Tatizo la utafiti lilijikita katika pengo la kielimu. Pengo hili lilihusu uchanganuzi wa vijana wa kiume kwa kuzingatia kwa pamoja taswira yao, changamoto zao, na nafasi ya jamii. Kwa msingi huo, maswali ya utafiti yaliundwa kuendana na malengo matatu.

Sura ya Pili ilihusu mapitio ya maandishi na msingi wa kinadharia. Mapitio yalipangwa kulingana na malengo ya utafiti. Kwanza, maandishi kuhusu usawiri wa vijana wa kiume yalihakikiwa. Pili,

maandishi kuhusu changamoto zao yalipitiwa. Tatu, maandishi kuhusu nafasi ya jamii katika kuwakuza yalichanganuliwa. Mapitio hayo yalionesha kuwa tafiti mbalimbali zimejadili uanaume, usawiri wa wahusika, na matarajio ya kijamii. Hata hivyo, kulibaki haja ya kuchanganua vipengele hivyo kwa pamoja katika riwaya teule. Sura hiyo pia ilijenga msingi wa kinadharia kwa Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume na mihimili yake.

Sura ya Tatu ilieleza muundo na mbinu za utafiti. Utafiti ulitumia muundo wa kimaelezo. Kundi lengwa lilihusisha riwaya za Kiswahili za Mwenda Mbatia. Kutokana na kundi hilo, riwaya mbili ziliteuliwa kimakusudi: Njozi Yapata Mtenzi (2018) na Utelezi (2023). Data zilikusanywa kwa usomaji makini na unukuzi wa vifungu husika. Orodha ya uthibitishaji ilitumika kupanga na kuhifadhi data. Data zilichanganuliwa kimaelezo na kimaudhui, zikiongozwa na malengo ya utafiti na mihimili ya nadharia.

Sura ya Nne iliwasilisha na kujadili matokeo ya utafiti kwa malengo matatu. Lengo la kwanza lilihusu usawiri wa vijana wa kiume. Lengo la pili lilihusu changamoto zao. Lengo la tatu lilihusu nafasi ya jamii katika kuwakuza. Matokeo ya kila lengo yalichanganuliwa kwa kuhusianisha matini na mihimili ya nadharia.

5.2.1. Usawiri wa Vijana wa Kiume Katika Riwaya Teule

Utafiti ulibaini kuwa vijana wa kiume katika riwaya teule wamesawiriwa kwa taswira mbalimbali. Miongoni mwazo ni wasomi, wenye bidii, na wenye mapenzi ya dhati. Wengine ni wapelelezi, wenye kubadilika, na wenye utu. Wengine wana ndoto na matarajio makubwa, ujasiri, na uwezo wa kustahimili changamoto za kifamilia. Wengine wana vipawa vya michezo na ufahamu wa kisiasa. Hata hivyo, baadhi yao wamesawiriwa kwa taswira hasi. Hizi ni pamoja na matumizi ya mihadarati, ukatili, uwizi, na kupenda raha. Kwa hiyo, taswira ya vijana wa kiume si ya aina moja. Ni changamano na inajumuisha mielekeo chanya na hasi.

Matokeo haya yanaafikiana na mawazo ya wataalamu waliopitiwa katika Sura ya Pili. Masibo (2009), Mutungi (2008), Kanwa (2022), na Kurgat, Oluoch na Mumo (2022) walionesha umuhimu wa kuchunguza usawiri wa wahusika wa kiume. Kiritu, Mwihia na Mwangi (2024) walisisitiza umuhimu wa matarajio ya jamii katika ujenzi wa wahusika hao. Francis, Wagumba na Ndung'u

(2025) walionesha kuwa taswira za uanaume hujengwa kupitia mitazamo ya kijamii. Kwa mtazamo huu, matokeo haya yanaunga mkono hoja kwamba taswira ya kijana wa kiume huathiriwa na mwingiliano wa sifa binafsi, mazingira, mahusiano, na matarajio ya jamii.

Aidha, matokeo haya yanaonesha kuwa Mbatia anapanua dhana ya uanaume. Anawasawiri vijana wa kiume zaidi ya dhana finyu ya nguvu na mamlaka. Usomi, bidii, utu, mapenzi ya dhati, ujasiri na vipawa vinaonekana katika ujenzi wa taswira yao. Kwa upande mwingine, mihadarati, wizi, ukatili na kupenda raha vinaonesha uhusiano wa mazingira na matarajio ya kijamii na mielekeo hasi. Hivyo, lengo la kwanza la utafiti limejibiwa. Taswira mbalimbali za vijana wa kiume katika riwaya teule zimebainishwa na kufafanuliwa.

5.2.2. Changamoto Zinazowakumba Vijana wa Kiume Katika Riwaya Teule

Utafiti ulibaini kuwa vijana wa kiume hukumbwa na changamoto mbalimbali. Changamoto hizi ni za kifamilia, kiuchumi, kielimu, kikazi, kijamii, kisiasa na kisaikolojia. Zinajumuisha vifo na ukosefu wa ajira. Zinajumuisha pia ufisadi, unyanyasaji, na matumizi ya mihadarati. Zinahusisha uongozi mbaya, ubaguzi, usaliti na utelekezwaji. Zinajumuisha shinikizo la marika, umaskini, na ushindani wa nafasi za elimu ya juu. Zinahusisha pia msongo wa mitihani ya kitaifa, kuvunjika kwa familia, na vitisho vya migogoro ya kifedha. Kwa ujumla, changamoto hizi zinahusisha nyanja mbalimbali za maisha. Zinaweza kuchocheana.

Matokeo haya yanahusiana na mawazo ya wataalamu waliorejelewa katika mapitio ya maandishi. Mahalik, Burns na Syzdek (2003) walihusisha mitazamo ya uanaume na jinsi wanaume wanavyokabiliana na maisha. Chaterji (2004) na Crous (2005) walionesha umuhimu wa matarajio ya kijinsia katika uzoefu wa wanaume. Izugbara (2019) alijadili mazingira ya vijana wa kiume na matarajio ya maisha yao. Carney na wenzake (2022) walionesha changamoto za kisaikolojia zinazowapata wavulana katika ujana. Kuhusu uchumi na ajira, matokeo yanaendana na Mwakimako (2019) na Kinyua (2024), waliojadili changamoto za kiajira kwa vijana wahitimu. Rinkanya (2022) pia alionesha jinsi changamoto za vijana zinavyowasilishwa katika riwaya za Kiswahili.

Matokeo haya yanaonesha kuwa changamoto za vijana wa kiume si matatizo ya mtu binafsi pekee. Matarajio ya jamii kuhusu mafanikio, kujitegemea, na uwajibikaji yanaweza kuongeza uzito wa changamoto hizo. Kwa hiyo, lengo la pili la utafiti limejibiwa. Changamoto mbalimbali za vijana wa kiume zimebainishwa na kuhusishwa na mazingira na matarajio ya kijamii.

5.2.3. Nafasi ya Jamii Katika Kuwakuza Vijana wa Kiume

Utafiti ulibaini kuwa jamii ina mchango chanya na hasi katika kuwakuza vijana wa kiume. Mchango chanya unajitokeza kupitia malezi na ushauri. Unajitokeza pia kupitia msaada wa kielimu na utoaji wa fursa. Unahusisha ukuzaji wa vipawa na uwepo wa mifano bora ya kuigwa. Kwa upande mwingine, mchango hasi unahusishwa na uzembe wa malezi na ufisadi. Unahusisha matumizi mabaya ya mamlaka na uhalifu. Unahusisha pia kuwadekeza vijana na kushindwa kuwapa mwongozo. Kwa hiyo, jamii ina nafasi muhimu katika kujenga au kudhoofisha hulka na maadili ya vijana wa kiume.

Matokeo haya yanaafikiana na mawazo ya wataalamu waliorejelewa katika Sura ya Pili. Msanjila na wenzake (2011) walisisitiza nafasi ya jamii katika kujenga mitazamo ya kijinsia. Kanana (2000) alionesha umuhimu wa malezi ya awali katika ujenzi wa majukumu ya kijinsia. Muchiri (2018) alionesha umuhimu wa ushiriki wa jamii katika kuwawezesha vijana. Opunde (2018) alionesha jinsi matarajio ya kijamii yanavyoathiri mienendo ya wanaume. Janvan (2023) alionesha kuwa mazingira ya kijamii yanaweza kuwa chanzo cha ukandamizaji wa wanaume. Hoja hii inaendana na matokeo ya utafiti huu kuhusu mchango hasi wa jamii.

Kwa hiyo, matokeo haya yanaunga mkono mtazamo huu: jamii si mazingira ya pembeni katika ukuaji wa vijana wa kiume. Ni sehemu ya mchakato wa kujenga utambulisho, maadili, na matarajio yao. Lengo la tatu la utafiti limejibiwa. Jamii imeonekana kuwa chombo cha kuwawezesha vijana wa kiume, na pia chanzo cha changamoto zinazoweza kudhoofisha maendeleo yao.

5.3. Hitimisho

Kwa kuzingatia swali la kwanza, "Vijana wa kiume wamesawiriwa vipi katika Njozi Yapata Mtenzi (2018) na Utelezi (2023)?", utafiti umelijibu kikamilifu. Vijana wa kiume wamesawiriwa kwa taswira chanya na hasi. Wamewasilishwa kama wasomi, wenye bidii, na wenye utu.

Wamewasilishwa pia kama wenye ujasiri, mapenzi ya dhati, matarajio na vipawa. Baadhi yao wana uwezo wa kukabiliana na changamoto. Wakati huohuo, wengine wamesawiriwa kama wakatili, wezi, watumizi wa mihadarati na wapenda raha. Hivyo, Mbatia anajenga taswira changamano isiyowaweka vijana katika kundi moja la kitabia. Taswira hii inaeleweka kupitia mwingiliano wa sifa binafsi, mahusiano, mazingira, na matarajio ya kijamii.

Kwa swali la pili, "Ni changamoto zipi zinazowakumba vijana wa kiume katika riwaya teule?", utafiti umebaini changamoto mbalimbali. Changamoto hizi ni za kifamilia, kiuchumi, kielimu, kikazi, kijamii, kisiasa na kisaikolojia. Zinahusiana na mazingira ya vijana na matarajio yanayowekwa juu yao. Baadhi ya changamoto huathiriana na kuzalisha matokeo mengine. Hii inaonesha kuwa uzoefu wa vijana wa kiume ni wa pande nyingi. Hauwezi kueleweka kwa tatizo moja pekee.

Kwa swali la tatu, "Jamii ina mchango upi katika kuwakuza vijana wa kiume?", utafiti umethibitisha mchango wa aina mbili: chanya na hasi. Familia, shule, walimu, marika na taasisi nyingine huwapa vijana malezi, ushauri, elimu, na mifano bora. Kinyume chake, uzembe wa malezi, ufisadi, matumizi mabaya ya mamlaka, na ukosefu wa mwongozo huchangia kudhoofika kwao. Kwa hiyo, jamii ina nafasi muhimu katika kuwawezesha au kuwazuia vijana wa kiume katika kujenga maisha yao.

5.3.1 Ufaafu wa Mihimili ya Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume

Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume imeonekana kuwa mwafaka katika utafiti huu. Iliwezesha kuchanganua uhusiano kati ya taswira ya vijana wa kiume, matarajio ya jamii, changamoto zao, na mazingira yao. Mihimili minne iliyoteuliwa haikutumika kama maelezo ya jumla ya uanaume. Ilitumika kama misingi ya kutafsiri ujenzi wa wahusika na athari za mazingira yao.

Mhimili wa kwanza unasisitiza kuwa sifa za vijana hujengwa kupitia imani, matarajio ya kijamii na mazingira. Ulifaa katika kueleza taswira zilizobainika katika lengo la kwanza. Kupitia mhimili huu, sifa kama usomi, bidii, na ujasiri zilitazamwa katika uhusiano na mazingira. Sifa hasi kama mihadarati, wizi na kupenda raha nazo zilitazamwa hivyo. Mhimili huu uliwezesha utafiti kuepuka kuzichukulia sifa hizo kama tabia za asili za wanaume.

Mhimili wa pili unaonesha kuwa matarajio ya kijamii yanaweza kuzalisha changamoto. Ulifaa zaidi katika lengo la pili. Changamoto kama ukosefu wa ajira na msongo wa mawazo zilifafanuliwa kwa matarajio ya kujitegemea na mafanikio. Shinikizo la marika na changamoto za kifamilia nazo zilihusishwa na matarajio hayo. Mhimili huu ulionesha kuwa matarajio ya kijamii huwa mzigo pale yanapokutana na mazingira yasiyotoa fursa za kuyatimiza.

Mhimili wa tatu unasisitiza mchango wa jamii katika kujenga hulka na maadili. Ulifaa katika malengo yote matatu, hasa katika nafasi ya jamii. Ulieleza namna malezi, familia, shule na marika vinavyochangia mienendo ya vijana. Ulisaidia pia kufafanua sababu za mchango chanya au hasi wa jamii.

Mhimili wa nne unahusu namna jamii inavyogawa majukumu ya kijinsia. Ulisaidia kueleza matarajio ya nguvu, uwajibikaji na mafanikio yanayowekwa juu ya vijana wa kiume. Ulikuwa muhimu katika kueleza changamoto zitokanazo na pengo kati ya matarajio ya jamii na mazingira halisi ya vijana. Uliimarisha pia uchanganuzi wa nafasi ya jamii katika kuwakuza.

Kwa ujumla, mihimili hiyo minne ilifaa kwa sababu kila mmoja uliangazia kipengele tofauti cha ujenzi wa uanaume. Kwa pamoja, iliwezesha utafiti kuunganisha sifa za wahusika, matarajio ya jamii, mazingira, changamoto, na nafasi ya jamii. Kwa hiyo, Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume haikuwa mapambo ya kinadharia. Ilikuwa dira ya uchanganuzi iliyowezesha kutafsiri matokeo ya utafiti.

5.3.2 Hitimisho la Jumla

Kwa ujumla, utafiti umehitimisha kuwa taswira ya vijana wa kiume katika Njozi Yapata Mtenzi (2018) na Utelezi (2023) ni changamano. Inajengwa katika mwingiliano wa sifa binafsi, matarajio ya kijamii, mazingira na mahusiano. Vijana hao hawaonekani kama wenye sifa chanya pekee. Wala hawaonekani kama wanaotawaliwa na changamoto pekee. Wanaonekana kama vijana wanaopitia mazingira yanayoweza kuwajenga, kuwawekea vikwazo, au kuwaelekeza katika mienendo tofauti.

Utafiti umehitimisha pia kuwa changamoto zao haziwezi kutenganishwa na mazingira ya kifamilia, kijamii, kiuchumi, kielimu na kisiasa. Nafasi ya jamii ni muhimu katika kuwawezesha

vijana kujenga mienendo chanya. Hata hivyo, jamii hiyo hiyo inaweza kuchangia kudhoofika kwao. Hii hutokea inaposhindwa kutoa malezi, mwongozo, na fursa zinazofaa.

Kwa msingi huo, utafiti umeonesha kuwa kuelewa taswira ya vijana wa kiume kunahitaji uchanganuzi wa pamoja. Uchanganuzi huu unahusisha usawiri wao, changamoto zao, na nafasi ya jamii katika kuwakuza. Huu ndio mchango mkuu wa utafiti huu katika mjadala wa usawiri wa vijana wa kiume katika Fasihi ya Kiswahili.

5.4 Mapendekezo

Kwa kuzingatia matokeo na hitimisho la utafiti huu, mapendekezo yafuatayo yanatolewa:

Kwanza, watafiti wa Fasihi ya Kiswahili wanaweza kufanya tafiti zaidi kuhusu taswira ya vijana wa kiume katika riwaya za vipindi tofauti. Wanaweza kuchunguza kama usawiri wao umebadilika kutokana na mabadiliko ya kijamii, kiuchumi na kiutamaduni. Tafiti hizo zinaweza kulinganisha riwaya za zamani na za kisasa. Zitasaidia kubaini mabadiliko katika ujenzi wa uanaume na majukumu ya vijana wa kiume.

Pili, tafiti zijazo zinaweza kuchunguza kwa kina kipengele kimoja cha changamoto za vijana. Kipengele hicho kinaweza kuwa ukosefu wa ajira, shinikizo la marika, msongo wa mawazo, mihadarati au changamoto za kifamilia. Utafiti wa aina hii unaweza kutoa uelewa mpana zaidi wa uhusiano wake na matarajio ya kiuanaume.

Tatu, tafiti linganishi zinaweza kufanywa kuhusu watunzi wa kiume na wa kike. Zinaweza kuchunguza kama jinsia ya mtunzi huathiri usawiri wa vijana wa kiume. Zinaweza kuangazia sifa zao, changamoto zao, mahusiano yao na nafasi zao jamiini. Pendekezo hili linaendeleza mjadala wa kijinsia uliojitokeza katika tafiti zilizopitiwa.

Nne, watafiti wanaweza kutumia Nadharia ya Uwezo-Mkuu wa Kiume katika tanzu nyingine za fasihi. Tanzu hizo ni tamthilia, ushairi na hadithi fupi. Utafiti huo unaweza kubaini kama mihimili iliyotumika hapa inatoa maelezo yanayofanana au tofauti.

Tano, tafiti zijazo zinaweza kuchunguza nafasi ya jamii kwa kina zaidi. Zinaweza kuzingatia taasisi mahususi kama familia, shule au marika. Zinaweza kulinganisha mchango chanya na hasi wa taasisi hizo katika kujenga maadili ya vijana wa kiume.

Sita, tafiti zaidi zinaweza kuchunguza uhusiano wa uanaume na mabadiliko ya kijamii katika riwaya za karne ya ishirini na moja. Zinaweza kuangalia jinsi mabadiliko katika elimu, ajira, familia na uchumi yanavyoathiri dhana za uanaume na nafasi ya vijana wa kiume.

MAREJELEO

Akhtar, I. (2016). Research design. In Research in social science: Interdisciplinary perspectives (pp. 68–84).

Anyango, C. (2016). Usawiri wa uovu katika riwaya za Salamu Kutoka Kuzimu na Tutarudi na Roho Zetu [Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi].

Babbie, E. (1999). The basics of social research. Wadsworth Publishing.

Badru, M. (2020). Mfumo dume—chanzo cha ufungwa wa mwanaume: Uhakiki wa semi kutoka jamii za Kiafrika. Jarida la Fasihi ya Kiafrika, 4(2), 45–60.

Bailey, D. (1994). Methods of social research. Scientific Research, 23, 40–55. https://www.scirp.org/

Bayyo, R. (2020). Usawiri wa jinsia ya kiume katika riwaya teule za Shafi Adam Shafi [Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam].

Bly, R. (1990). Iron John: A book about men. Addison-Wesley.

Bowen, J. (2024). Mbinu ya kimajazi katika kuwasawiri wahusika na ukuzaji wa maudhui katika riwaya wa Tumaini. Jarida la Fasihi ya Kiswahili, 18(1), 22–38.

Brown, C. G. (2012). Sampling strategies in qualitative research. Sage Publications.

Bufacchi, V. (2005). Two concepts of violence. Political Studies Review, 3(2), 193–204. https://doi.org/10.1111/j.1478-9299.2005.00023.x

Bwire, T. (2021). Mkanganyiko wa kitambulisho cha vijana wa kiume katika jamii ya sasa. Jarida la Fasihi ya Kiswahili, 8(2), 100–115.

Carney, A., Mulei, T., Kurao, D., Hagstrom, C., & Sommer, M. (2022). “When I woke up I was so worried and ashamed, I thought it was a disease”: Adolescent boys’ transitions through puberty in Kenya. Frontiers in Reproductive Health, 4, 956060. https://doi.org/10.3389/frph.2022.956060

Caudwell, J. (2008). Sport feminism(s): Narratives of linearity? Women’s Studies International Forum, 31(5), 428–436.

Chaterji, S. (2004). Gender role transformations in modern Indian society. Journal of Social Change and Development, 2(1), 15–27.

Cheruiyot, J. (2020). Afya ya uzazi miongoni mwa vijana [Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta].

Chesaina, C. (2019). Uwasilishaji wa vijana katika fasihi ya Kiswahili. Jarida la Elimu ya Kiswahili, 6(1), 77–91.

Chesaina, C. (2020). Fasihi kama jukwaa la kuibua changamoto za kijamii. Eastern African Literary Studies, 7(2), 55–70.

City University of Hong Kong. (2020). Ethics in research—Research methods. Run Run Shaw Library. https://libguides.library.cityu.edu.hk/researchmethods/ethics

Cohen, L., Manion, L., & Morrison, K. (2000). Research methods in education (5th ed.). RoutledgeFalmer.

Colin, R. (2007). How to do a research project: A guide for undergraduate students. Blackwell Publishing.

Connell, R. W. (1987). Gender and power: Society, the person and sexual politics. Stanford University Press.

Connell, R. W. (1995). Masculinities. Polity Press.

Connell, R. W. (2005). Masculinities (2nd ed.). Polity Press.

Creswell, J. W. (2009). Research design: Qualitative, quantitative, and mixed methods approaches (3rd ed.). SAGE Publications.

Crous, M. (2005). Masculinity and literary representation in South Africa. South African Journal of African Literature, 15(2), 112–124.

Duckworth, A. (2016). Grit: The power of passion and perseverance. Scribner.

Enon, J. C. (1998). Educational research, statistics and measurement. Makerere University Press.

Francis, M. M., Wagumba, C., & Ndung'u, V. W. (2025). Exploration of TikTok's masculinity representations in influencing gender attitudes among selected Kenyan male youths in

Nairobi County. International Journal of Recent Advances in Multidisciplinary Topics, 6(6), 69–76. https://journals.ijramt.com/index.php/ijramt/article/view/3087

Githeya, M. (2021). Utambulisho wa vijana katika jamii zenye mchanganyiko wa kikabila. Journal of African Identity Studies, 15(4), 77–95.

Gromov, M. (2022). “Narrating the nation”: Kenya’s past, present and future. Language in Africa, 3(4), 3–23. https://doi.org/10.37892/2686-8946-2022-3-4-3-23

Gwachi, P. (2012). Migogoro ya kisaikolojia katika riwaya za Kiswahili [Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta].

Izugbara, C. O. (2005). The discontents of childhood: Masculinity and the construction of male child sexual identity in southeastern Nigeria. Sexuality & Culture, 9(3), 32–57.

Izugbara, C. (2019). Wanaume wenye kutamani miongoni mwa vijana maskini wa mijini nchini Kenya. Journal of Men’s Studies, 27(1), 22–39.

Janvan, M. (2023). Ukandamizaji wa jinsia ya kiume katika riwaya teule za Kiswahili [Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta].

Joyce, N. (2019). Nafasi ya vijana wa kiume katika jamii ya sasa. Journal of African Cultural Studies, 11(2), 55–68.

Kanana, F. (2000). Gender and societal expectations in Namibia. African Gender Review, 5(1), 71–86.

Kanwa, D. (2022). Usawiri wa kiume katika riwaya za waandishi wa kike na kiume. Journal of East African Literary Studies, 10(1), 34–50.

Kariuki, J. (2021). Nafasi ya fasihi katika kuibua changamoto za vijana wa kiume. Kenya Journal of Literature and Gender, 9(3), 14–27.

Kibera, L. (2005). Changamoto za vijana katika jamii za Kiafrika. Longhorn Publishers.

Kibet, J. O., & Mavisi, R. (2021). Taswira ya mwanamke katika kipindi cha Bi. Mswafari. Jarida la Fasihi na Jamii, 6(2), 44–53.

Kimani, D. (2023). Lugha ya usawiri katika riwaya za Kiswahili za kisasa. Journal of Kiswahili Studies, 22(2), 65–82.

Kimmel, M. (2017). Healing from hate: How young men get into—and out of—violent extremism. University of California Press.

Kinyua, P. (2024). Changamoto za vijana wahitimu katika soko la ajira. Eastern Africa Social Science Review, 9(1), 77–90.

Kiritu, E. W., Mwihia, M. N., & Mwangi, P. M. (2024). A critical analysis of societal expectations for male characters in African feminist literature by two male and two female writers. International Research Journal of Social Sciences, Education and Humanities, 6(2). https://www.irjp.org/index.php/IRJSEH/article/view/289

Kothari, C. R. (2008). Research methodology: Methods and techniques (2nd ed.). New Age International Publishers.

Kurgat, J., Oluoch, F., & Mumo, A. (2022). Lugha na usawiri wa wahusika katika riwaya za Kiswahili. Jarida la Fasihi na Lugha, 11(3), 88–104.

Luyt, R. (2018). Masculinities representations inventory (MRI, English version): A measure of gender (re)presentation. The Journal of Men's Studies, 26(2), 157–183. https://doi.org/10.1177/1060826517736781

Mahalik, J. R., Burns, S. M., & Syzdek, M. (2003). Masculinity and perceived normative health behaviors as predictors of men's health behaviors. Social Science & Medicine, 64(11), 2201–2209.

Makokha, A. (2023). Taswira ya mwanaume dhaifu katika riwaya za Kiswahili. East African Journal of Literary Criticism, 5(2), 99–112.

Masibo, S. (2009). Usawiri wa wahusika wa kiume na wa kike katika riwaya za Ngugi wa Thiong'o na Alice Walker [Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Moi].

Mbiti, J. S. (1990). African religions and philosophy (2nd ed.). Heinemann.

McCombes, S. (2021). Sampling methods: Types and techniques. Scribbr. https://www.scribbr.com/methodology/sampling-methods

McLeod, S. (2019). Sampling in research. Simply Psychology. https://www.simplypsychology.org/sampling.html

Messerschmidt, J. W. (1993). Masculinities and crime: Critique and reconceptualization of theory. Rowman & Littlefield.

Msanjila, Y., na wenzake (2011). Jamii na mitazamo ya kijinsia. Journal of African Studies, 18(3), 200–218.

Muchiri, P. N. (2018). Factors influencing youth participation in the implementation of informal settlement projects in Kenya: A case of community-based projects in Kangemi Sub-County, Nairobi County [Master's thesis, University of Nairobi]. University of Nairobi Repository. http://hdl.handle.net/11295/106297

Mohlala, M. R. (2024). Representations of masculinity in African women's literature and their implications for English FET education: A feminist study of Ama Ata Aidoo's Changes: A love story, Chimamanda Ngozi Adichie's Purple Hibiscus and Sindiwe Magona's Mother to Mother [Master's dissertation, University of the Witwatersrand]. WIReDSpace. https://hdl.handle.net/10539/44987

Mohamed, S. A. (1990). Nyuso za Mwanamke. Longhorn.

Mohamed, S. A. (2001). Kiu. Oxford University Press.

Msanjila, Y. P., na wenzake (2011). Misingi ya taaluma ya Kiswahili. TUKI.

Mulokozi, M. M. (2017). Fasihi ya Kiswahili na maendeleo ya jamii. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI).

Mutuku, P. (2018). Mabadiliko ya kifamilia na athari zake kwa vijana [Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi].

Mutungi, J. (2008). Usawiri wa wahusika wa kiume kama kielelezo cha udume [Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam].

Mwakimako, H. (2019). Changamoto za kiuchumi kwa vijana wa kiume. African Journal of Sociology, 21(2), 133–147.

Mwangi, E. (2014). Fasihi ya kisasa na mbinu za usawiri. Kenya Journal of Literary Studies, 4(1), 44–60.

Mwangi, E. (2021). Changamoto za vijana wa kiume katika karne ya 21. Journal of African Social Development, 9(1), 88–101.

Naliaka, J. (2012). Uhakiki wa hali ya vijana katika riwaya ya Vipanya vya Maabara [Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi].

Nassaji, H. (2005). Qualitative and descriptive research: Data type versus data analysis. Language Teaching Research, 9(1), 5–21.

Newell, S. (2017). Usawiri wa wanaume katika fasihi ya Afrika Magharibi. Journal of African Literatures, 15(2), 77–93.

Ngugi wa Thiong'o. (2009). Decolonising the mind: The politics of language in African literature. East African Educational Publishers.

Njoroge, P., & Mbugua, K. (2020). Utandawazi na nafasi ya vijana wa Kiafrika. African Journal of Contemporary Issues, 13(1), 50–65.

Nkoroi, E., & Murimi, L. (2024). Usawiri wa ukandamizaji wa kijamii katika riwaya za Kiswahili. Kenya Journal of Literary Criticism, 12(2), 55–71.

Nyairo, J. (2019). Vijana wa kiume kama viongozi wa baadaye: Fasihi na jamii. EAEP.

Ochieng', J. (2022). Familia na malezi ya vijana wa kiume. Kenya Journal of Social Research, 12(4), 77–89.

Ochieng', P. (2022). Malezi ya familia na mshikamano wa kijamii. Moran Publishers.

Ogunyemi, C. (2020). Men in African women's writing. Feminist Africa, 16(1), 23–40.

Opunde, G. (2018). Uchunguzi wa masuala ya kijinsia katika nyimbo za Daudi Kabaka na John Amutabi Nzenze [Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi].

Osando, V., na wenzake(2022). Changamoto za uhalifu miongoni mwa vijana wa Kamiti. Kenya Journal of Criminology, 8(2), 33–49.

PubMed. (2020). Malezi na changamoto za vijana wa kiume katika Korogocho. Public Health Research Report, 25(3), 66–82.

Raymond, D. (2016). Usawiri wa wanaume katika methali za Kimeru nchini Kenya [Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta].

Rinkanya, J. (2022). Changamoto za vijana katika riwaya za Moraa Gitaa. Journal of Kiswahili Literature, 17(1), 40–59.

Robert, S. (1961). Kufikirika. East African Literature Bureau.

Rwegira, J. (2017). Ujinsia katika methali za Wakurya. Tanzania Journal of Oral Traditions, 4(1), 56–72.

Scott, L. (2020). Mgogoro wa kisaikolojia katika riwaya ya Mkadume na Unaitwa Nani? [Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta].

Sherman, J., & Wood, R. (1982). Gender roles and society. Harper & Row.

Shitemi, N. (1998). Gender representation in East African fiction. Nairobi University Press.

Silberschmidt, M. (2001). Disempowerment of men in rural and urban East Africa: Implications for male identity and sexual behavior. World Development, 29(4), 657–671.

Sommers, C. H. (2011). The war against boys: How misguided feminism is harming our young men. Simon & Schuster.

Stratton, F. (2019). Gender and African women writers. Journal of Postcolonial Writing, 55(4–5), 499–512.

Suzana, P. (2015). Usawiri wa mwanamke katika muziki wa nyimbo za dansi [Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam].

Wafula, C., & Njogu, K. (2007). Uhakiki wa fasihi ya Kiswahili. Jomo Kenyatta Foundation.

Wamalwa, A. (2013). Uchanganuzi wa changamoto za ujana katika riwaya za Habwe [Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta].

Wamitila, K. W. (2003). Kamusi ya fasihi: Istilahi na nadharia. Phoenix Publishers.

Wamitila, K. W. (2008). Fasihi ya Kiswahili: Nadharia na historia. Focus Publishers.

Wandera, J., & King’ei, K. (2002). Misingi ya isimu jamii. Nairobi University Press.

Wong, Y. (2017). Gender bias in China: A sociological study. Chinese Sociology Review, 10(2), 134–145.

Kiambatisho 1; **Kibali cha Utafiti cha Chuo Kikuu cha Kikatoliki Afrika Mashariki**

THE CATHOLIC UNIVERSITY OF EASTERN AFRICA

AMECEA

22/09/25

To whom it may concern

RE: OPICHO PERPETUA 1062149

It is our pleasure to inform you that Opicho Perpetua is a student in our Department of Languages, Literature and Communication undertaking a Masters of Arts in Kiswahili and Communication. She defended her proposal entitled: **TASWIRA YA VIJANA WA KIUME KATIKA RIWAYA TEULE ZA MWENDA MBATIA; *NJOZI YAPATA MTENZI* (2018) NA *UTELEZI* (2023).** She is due to collect data and l therefore request that she is accorded the necessary assistance.

Yours faithfully

Dr. Rose Mavisi
HoD Languages,Literature and Communication
Catholic University of Eastern Africa

Kiambatisho 3; Kibali cha Utafiti cha NACOSTI



REPUBLIC OF KENYA

NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Ref No: 440725

Date of Issue: 11/November/2025

RESEARCH LICENSE

This is to Certify that Miss.. Perpetua nasimiyu opicho of Catholic University of Eastern Africa, has been licensed to conduct research as per the provision of the Science, Technology and Innovation Act, 2013 (Rev.2014) in Nairobi on the topic: TASWIRA YA VIJANA WA KIUME KATIKA RIWAYA TEULE ZA MWENDA MBATIA; NJOZI YAPATA MTENZI (2018) NA UTELEZI (2023) for the period ending : 11/November/2026.

License No: NACOSTI/P/25/4181740

440725

Applicant Identification Number

Ag. Director General
NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Verification QR Code

NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document, Scan the QR Code using QR scanner application.

See overleaf for conditions

THE SCIENCE, TECHNOLOGY AND INNOVATION ACT, 2013 (Rev. 2014)

Legal Notice No. 108: The Science, Technology and Innovation (Research Licensing) Regulations, 2014

The National Commission for Science, Technology and Innovation, hereafter referred to as the Commission, was the established under the Science, Technology and Innovation Act 2013 (Revised 2014) herein after referred to as the Act. The objective of the Commission shall be to regulate and assure quality in the science, technology and innovation sector and advise the Government in matters related thereto.

CONDITIONS OF THE RESEARCH LICENSE

1. The License is granted subject to provisions of the Constitution of Kenya, the Science, Technology and Innovation Act, and other relevant laws, policies and regulations. Accordingly, the licensee shall adhere to such procedures, standards, code of ethics and guidelines as may be prescribed by regulations made under the Act, or prescribed by provisions of International treaties of which Kenya is a signatory to.
2. The research and its related activities as well as outcomes shall be beneficial to the country and shall not in any way; i. Endanger national security
    ii. Adversely affect the lives of Kenyans
    iii. Be in contravention of Kenya's international obligations including Biological Weapons Convention (BWC), Comprehensive Nuclear-Test-Ban Treaty Organization (CTBTO), Chemical, Biological, Radiological and Nuclear (CBRN).
    iv. Result in exploitation of intellectual property rights of communities in Kenya
    v. Adversely affect the environment
    vi. Adversely affect the rights of communities
    vii. Endanger public safety and national cohesion
    viii. Plagiarize someone else's work
3. The License is valid for the proposed research, location and specified period.
4. Neither the license nor any rights thereunder are transferable.

5. The Commission reserves the right to cancel the research at any time during the research period if in the opinion of the Commission the research is not implemented in conformity with the provisions of the Act or any other written law.
6. The Licensee shall inform the relevant County Director of Education, County Commissioner and County Governor before commencement of the research.
7. Excavation, filming, movement, and collection of specimens are subject to further necessary clearance from relevant Government Agencies.
8. The License does not give authority to transfer research materials.
9. The Commission may monitor and evaluate the licensed research project for the purpose of assessing and evaluating compliance with the conditions of the License.
10. The Licensee shall submit one hard copy, and upload a soft copy of their final report (thesis) onto a platform designated by the Commission within one year of completion of the research.
11. The Commission reserves the right to modify the conditions of the License including cancellation without prior notice.
12. Research, findings and information regarding research systems shall be stored or disseminated, utilized or applied in such a manner as may be prescribed by the Commission from time to time.
13. The Licensee shall disclose to the Commission, the relevant Institutional Scientific and Ethical Review Committee, and the relevant national agencies any inventions and discoveries that are of National strategic importance.
14. The Commission shall have powers to acquire from any person the right in, or to, any scientific innovation, invention or patent of strategic importance to the country.
15. Relevant Institutional Scientific and Ethical Review Committee shall monitor and evaluate the research periodically, and make a report of its findings to the Commission for necessary action.

Innovation(NACOSTI),
Off Waiyaki Way, Upper Kabete,
P. O. Box 30623 - 00100 Nairobi, KENYA
Telephone: 020 4007000, 0713788787, 0735404245
E-mail: dg@nacosti.go.ke
Website: www.nacosti.go.ke